JACKPOT BABA LAO!
TZS. 412,613,570
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## VODACOM na IPP Media kushirikiana kidijitali


Kamanda bodaboda mtawezana kweli?
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe
SARAH PIMA
Mwanamazingira aliyeibukia mkutanoni Misri na bidhaa za malighafi taka, zilizo kamata soko
Mkasa wa Wanigeria watatu kujificha kwenye rada uvunguni mwa meli siku 11


# Nipashe

Ijumaa Desemba 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581147

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


UKURASA 13

## MATOKEO LA VII

# Aliyebadilishiwa namba afaulu, apata daraja 'A'

**WENZAKE** waliokuwa hatarini 'kuchaka-chuliwa' wafaulu, 2,190 wafutiwa matokeo kwa udanganyifu...*Endelea Uk. 2*



Iptisum Slim

## SAMIA AMULIKA MAMBO MATATU MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

UKURASA 3



## Mama na watoto waliofariki dunia kwa ajali wakitoka mahafali wazikwa

UKURASA 4

Majeneza yenye miili ya wanafamilia waliofariki kwa ajali ya gari, Immaculata Byemerwa (mama) na watoto wake, Janeth Byemerwa na Jolista Byemerwa, yakiwa kwenye Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Tabata Kuu jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya ibada kabla ya kusafirishwa kwenda Kibaha mkoani Pwani kuzikwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** **SIMBA: TUTARUDI KILELENI LIGI KUU** UK. 32 **KATUNI** UK. 6




Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athumani Amasi.

# Aliyebadilishiwa namba afaulu, apata daraja 'A'

**Na Romana Mallya**

MTAHINIWA wa darasa la saba mwaka huu Iptisum Slim wa Shule ya Msingi ya Chalinze Modern Islamic Pre and Primary School ya mkoani Pwani, aliyelalamikia kubadilishiwa namba ya mtihani, amefaulu kwa daraja A.

Siku chache baada ya mtihani huo kufanyika kwa siku mbili Oktoba 5 na 6 mwaka huu, ilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii video fupi ya mwanafunzi huyo akilalamika kubadilishiwa namba yake wakati akiufanya na serikali ilifanya uchunguzi na kubaini ukweli huo na kukifutia usajili wa mtihani kituo hicho.

Katika matokeo ya shule hiyo yaliyoko kwenye tovuti rasmi ya Baraza la Mitihani (NECTA) yaliyotangazwa jana, mwanafunzi huyo amefaulu mtihani huo kwa kupata daraja A kwenye Kiswahili, Kiingereza A, Maarifa A, Hisabati B, Sayansi A na Uraia B.

Wanafunzi wengine wanne ambao nao walikumbwa na kadhia hiyo ya kubadilishiwa namba shuleni huko, nao wamefaulu kwa daraja A ambao ni pamoja na Jasmine Mzee aliyepata A katika Kiswahili, Kiingereza A, Maarifa A, Hisabati B, Sayansi A na Uraia A.

Wengine ni Jokha Nassoro aliyepata Kiswahili A, Kiingereza A, Maarifa A, Hisabati B, Sayansi A na Uraia B; Khairat Mohamed aliyefaulu kwa A ya Kiswahili, Kiingereza A, Maarifa A, Hisabati B, Sayansi A na Uraia B; na Khaula Mruma aliyepata A ya Kiswahili, Kiingereza A, Maarifa A, Hisabati B, Sayansi A na Uraia B.

Baada ya serikali kubaini dosari hiyo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda aliagiza watumishi wake pamoja na walimu wa shule hiyo waliohusika katika tukio la mtahiniwa Iptisum Slim na wenzake sita waliobadilishiwa namba za mitihani wa darasa la saba, wafukuzwe.

Katika matokeo ya mtihani wa kumaliza darasa la saba (PSLE) 2022 yaliyotangazwa jana na Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athumani Amasi, inaonyesha ufaulu wa watahiniwa katika masomo yote uko juu ya wastani isipokuwa kwa somo la Kiingereza.

Alisema takwimu za somo la Kiswahili zinaonyesha kuwa jumla ya watahiniwa 403,825 (29.96%) wamepata daraja A, watahiniwa 552,404 (40.92%) wamepata daraja B, watahiniwa 250,194 (18.56%) wamepata daraja C, watahiniwa 104,339 (7.74%) wamepata daraja D na 37,217 (2.76%) wamepata daraja E.

Katika somo la Kiingereza alisema watahiniwa 59,990 (4.45%) wamepata daraja A, 56,569 (4.20%) daraja B, 279,580 (20.74%) daraja C, 912,708 (67.71%) daraja D na 39,086 (2.90%) wamepata daraja E.

Amasi alisema takwimu za somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi zinaonyesha watahiniwa 58,657 (4.35%) wamepata daraja A, 300,708 (22.31%) daraja B, 600,813 (44.57%) daraja C, 353,844 (26.25%) daraja D na 33,951 (2.52%) wamepata daraja E.

"Katika somo la Uraia na Maadili, jumla ya watahiniwa 63,158 (4.695) wamepata daraja A, 582,305 (43.20%) daraja B, 458,169 (33.99%) daraja C, 202,793 (15.04%) daraja D na 41,566 (3.08%) wamepata daraja E," alisema.

Katika somo la Sayansi na Hisabati alisema jumla ya watahiniwa 43,362 (3.22%) wamefaulu kwa daraja A, 133,288 (9.89%) daraja B, 541,623 (40.18%) daraja C, 613,442 (45.51%) daraja D na 16,267 (1.21%) daraja E.

Alisema katika somo la Sayansi na Teknolojia jumla ya watahiniwa 67,071 (4.98%) wamepata daraja A, 287,690 (21.34%) daraja B, 610,839 (45.31%) daraja C, 360,031(26.71%) daraja D na 22,362 (1.66%) daraja E.

Alisema jumla ya watahiniwa 1,073,402 kati ya 1,348,073 wenye matokeo ambayo ni sawa na asilimia 79.62 wamefaulu kwa kupata madaraja A, B na C. Kati yao, wasichana ni 558,825 (asilimia 78.91 ya wasichana wote waliofanya mtihani) na wavulana ni 514,577 (asilimia 80.41 ya wavulana wote waliofanya mtihani).

Alisema mwaka jana watahiniwa waliofaulu walikuwa 907,802 sawa na asilimia 81.97, hivyo kuna kupungua kwa ufaulu kwa asilimia 2.35, japo kuwa idadi ya waliofaulu imeongezeka kwa watahiniwa 165,600 (asilimia 18.24) kulinganishwa na mwaka 2021.

Amasi alisema katika mtihani huo, jumla ya watahiniwa 1,384,186 walisajiliwa kuufanya, wasichana walikuwa ni 723,027 sawa na asilimia 52.23 na wavulana ni 661,159 sawa na asilimia 47.77. Watahiniwa wenye mahitaji maalum walikuwa 4,221 sawa na asilimia 0.3.

Alisema watahiniwa 33,305 sawa na asilimia 2.41 hawakuufanya kwa sababu mbalimbali zikiwamo utoro na ugonjwa na kati yao, wasichana ni 13,471 na wavulana ni 19,834.

## ...2,190 wafutiwa matokeo, vituo vyao vyafutiwa usajili

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani (NECTA) limetangaza matokeo ya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka huu bila kutangaza wanafunzi bora kitaifa wala shule bora, huku likiwataja wanafunzi 2,734 kuhusika kwenye udanganyifu.

Vilevile, wanafunzi 540 wa vituo sita vya mitihani mkoani Dar es Salaam wanachunguzwa na ikibainika walihusika kwenye udanganyifu, matokeo yao yatafutwa, huku vituo 24 vikifutwa kwa kosa hilo hilo.

Akitangaza matokeo hayo jana mkoani Dar es Salaam, Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athumani Amasi, alisema matokeo hayo yamefutwa kwa mujibu wa kifungu 30(2) (b) cha Kanuni za Mitihani 2016, kikisomwa pamoja na kifungu cha 5(2)(i) na (j) cha Sheria ya Baraza la Mitihani Sura ya 107.

Alisema jumla ya wanafunzi 2,194 sawa na asilimia 0.16 wamefutiwa matokeo kutokana na udanganyifu.

Katika mtihani huo uliofanyika Oktoba 5 na 6 mwaka huu, NECTA imefuta matokeo yote ya watahiniwa 2,194 sawa na asilimia 0.16 ya watahiniwa 1,350,881 waliofanya mtihani huo kutokana na kubainika kufanya udanganyifu.

Akitolea ufafanuzi suala la utofauti wa utoaji wa matokeo kwa mwaka huu, Amasi alisema: "Umesema mara nyingi, mmeishi kwa mazoea, ninaomba tuondokane na hilo.

"Taarifa niliyowapatia mtaipitia na muone taarifa hiyo inafaa kuwasilishwa kwenye umma, pengine si hiyo ya mazoea, itawezesha kujua hali yetu kielimu iko wapi, siyo hiyo ya kumtangaza mtu mmoja katika watu milioni 1.3," alisema.

### VITUO 24 VILIVYOFUNGIWA

Amasi alisema NECTA imefungia vituo vya mitihani 24 sawa na asilimia 0.13 ya vituo 17,935 vya mitihani vilivyothibitika kupanga na kufanya udanganyifu katika mtihani huo.

Alisema vituo hivyo vimefungwa kwa mujibu wa kifungu 4(8) cha Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016 hadi hapo baraza litakapojiridhisha kuwa ni salama kwa uendeshaji wa mitihani ya taifa.

"Baraza lina mamlaka ya kufuta matokeo ya mtahiniwa hata kama alishatunukiwa cheti endapo litajiridhisha pasipo shaka alifanya udanganyifu.

"Hata katika vituo tulivyovifuta mwaka huu upo uwekezekano viliwahi kufanya udanganyifu, lakini hatuwezi kuvifutia mpaka tujiridhishe, siku za mwizi ni 40," alifafanua.

### YALIYOZUILIWA

Amasi alisema NECTA limezuia matokeo ya watahiniwa 179 ambao waliugua au walipata matatizo na kushindwa kufanya mtihani kwa masomo yote au baadhi yake ambao wamepewa fursa nyingine ya kurudia.

Pia alisema wanafunzi 540 wa vituo sita ambavyo ni Joyland (PS026131), Castle Hill (PS0204150), Green Acres (PS02033129), Great Vision (PS0206099), Mtendeni (PS0202026) na Maktaba (PS0202058) vyote vya Mkoa wa Dar es Salaam wanatuhumiwa kufanya udanganyifu ambao baraza linafanya uchunguzi na wakibainika matokeo yao yatafutwa.

Kuhusu wanafunzi waliofutiwa matokeo yao, alisema NECTA haifuti usajili wao, hivyo wana nafasi ya kuendelea na mfumo wa elimu lakini si kwa kuchaguliwa kwenda shule za umma.

Akitolea ufafanuzi kwanini mtoto anaadhibiwa wakati mwalimu ndiye aliyesababisha udanganyifu. Kiongozi huyo alisema: "Watoto hawa tumesema hatuwafutii usajili, tunaanza kuwafundisha. Ekaristi wanapata wakiwa na umri gani? Wanafundishwa kwamba kuiba ni dhambi, tumesema hatufuti usajili. Wafundisheni watoto wenu kuanzia wakiwa wadogo."

### SHULE ZILIZOFUNGIWA

Alivitaja vituo vya mtihani na mikoa yake kwenye mabano ni Kadama (Chato-Geita), Rweikiza (Bukoba-Kagera), Kilimanjaro (Arumeru-Arusha), Sahare (Tanga) na St. Anne Marie (Ubungo-Dar es Salaam).

Nyingine Ukerewe (Ukerewe-Mwanza), Peaceland, (Ukerewe-Mwanza), Karume (Bukoba-Kagera), Al-Hikma, (Dar es Salaam) na Kazoba (Karagwe-Kagera).

Pia zimo Mugini (Magu-Mwanza), Jamia (Bukoba-Kagera), Winners (Mwanza), Musabe (Mwanza), Elisabene (Tunduma, Songwe), High Challenge (Arusha), Tumaini (Sengerema-Mwanza) na Olele (Mwanza).

Shule nyingine ni Mustlead (Chalinze-Pwani), Moregas (Tarime-Mara), Leaders (Rorya- Mara), Kivulini (Mwanza) na St. Severine (Biharamulo-Kagera).

Nipashe imebaini baadhi ya shule zilizofungiwa mwaka huu kuwa kituo cha mtihani, katika matokeo ya mwaka jana zilikuwa kwenye 10 bora kitaifa na wanafunzi wake walikuwa kwenye orodha ya wanafunzi bora kitaifa.

Baadhi ya shule hiyo Kadama (Geita) ambayo katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2021, mwanafunzi wake alikuwa miongoni mwa wavulana 10 bora kitaifa na St. Anne Marie (Dar es Salaam) ilitoa wanafunzi bora kitaifa.

## HABARI KITAIFA



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akionyesha tuzo maalum baada ya kukabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Telack (wa pili kushoto), kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Ilulu, mjini Lindi jana. **PICHA: IKULU**

# Samia amulika mambo matatu mapambano dhidi ya UKIMWI

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maagizo matatu kwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) na wadau katika kupunguza unyanyapaa na elimu kwa umma ili kufikia maambukizi sifuri.

Maagizo hayo ni kuweka nguvu zaidi kuzuia maambukizi mpya ya ugonjwa huo, kudumisha huduma za Virusi vya UKIMWI (VVU) na kutokomeza ubaguzi na unyanyapaa kwa wanaoishi na VVU (WAVIU).

Amesema maagizo yanatokana na malengo ya kitaifa ya kufikia sifuri tatu ambazo ni; sifuri katika maambukizi mapya, vifo na unyanyapaa kufikia mwaka 2030 chini ya Mkakati wa Tatu wa Kutokomeza ugonjwa huo, mkakati uliozinduliwa mwishoni mwa mwezi uliopita.

Rais pia amezitaka taasisi za masuala hayo na wadau kuendelea kushirikiana na Wizara ya Afya kutekeleza mpango huo, huku akiitaka jamii kuwajibika kwa kujikinga na kuwakinga wengine ili kupambana na janga hilo.

Alitoa maagizo hayo jana alipohutubia mamia ya wananchi wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yaliyofanyika mkoani Lindi.

Rais alisisitiza kuwapo usawa kwenye utoaji huduma kudhibiti VVU na ugonjwa wa UKIMWI, ili kusiwe na maeneo au makundi ya watu yasiyofikiwa na huduma, hivyo kuondoa ubaguzi na unyanyapaa kwa watu wanaoishi na ugonjwa huo.

"Na hii inatokana na ukweli kwamba kukosekana kwa usawa kunarudisha nyuma juhudi zetu za kutokomeza ugonjwa huu ifikapo mwaka 2030. Hivyo hi muhimu tutumie maadhimisho haya kutafakari kwa kina na kuhakikisha tunaweka mikakati itakayoimarisha usawa ili lengo letu litimie," aliagiza.

Rais alisema kuna kazi kubwa imefanyika kupunguza maambukizi mapya, vifo na unyanyapaa lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kutokomeza janga hilo.

Pia alitaka kasi ya kutoa elimu na kampeni kwa jamii hasa vijana ikizingatiwa utafiti unaonyesha kuna kasi kubwa ya maambukizi kwa vijana.

"Lakini kwa mwendo ule ulioelezwa kwenye ripoti tofauti hapa kwamba kuna maambukizi yanakuwa ya vijana wetu wa miaka 15-24, tusipozuia lile safari yetu ya kutokomeza balaa hili itakuwa ndefu sana. Vijana wale wakiambukizwa leo, tukawapa huduma zote muda wao wa kuishi utakuwa na suala hili tutakwenda nalo kwa muda mrefu," alisema.

Rais alisema kukosekana kwa usawa kulijitokeza pia kwenye ugonjwa wa UVIKO-19 na kuwa maradhi hayo hayana mipaka kwa kuwa yapo dunia nzima, hivyo kunahitajika kazi kubwa ifanyike ili kupata usawa kwenye matibabu na huduma.

"Nchi pamoja na kushirikiana na wadau wengine, ni lazima tufanyie kazi tamko hilo (la Umoja wa Mataifa la kutokomeza VVU ifikapo 2030) kwa kuongeza juhudi na kuweka mikakati madhubiti ya itakayowezesha kutokomeza janga hili," alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema jitihada zimeendelea kufanyika katika kupambana na janga hilo ikiwamo kuwekwa maeneo matatu muhimu ya kimkakati yanayojumuisha utafiti wa viashiria vya hali ya VVU na UKIMWI nchini kwa mwaka 2022/23 uliozinduliwa Septemba mwaka huu.

"Eneo lingine ni lile la mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWI ambao umefanyiwa tathmini ya namna utakavyoweza kuwa na vyanzo endelevu, ili kuhakikisha serikali inakuwa na mchango endelevu katika kuboresha afua za kupambana na VVU na UKIMWI," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya UKIMWI (UNAIDS), Winnie Byanyima, alisema Tanzania inaongoza mapambano dhidi ya ugonjwa huo kwa nchi za Afrika ambapo kwa kipindi cha miaka 12 imepunguza maambukizi mapya kwa takribani asilimia 50.

"Hawa vijana wetu sasa hata hawajui UKIMWI upoje kwa sababu Tanzania imewapatia huduma ya afya asilimia 87 ya WAVIU. Ningependa kumshukuru Rais Dk. Samia kwa ujasiri, unyenyekevu na huruma yake kwa kuziwezesha jamii katika ngazi ya chini na kuhamasisha kuwapo wanawake katika uongozi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko alisema kamisheni hiyo itaendelea kupambana kufuata maagizo ya serikali ili kutimiza adhma ya nchi ya kumaliza kabisa VVU na UKIMWI nchini, akiwashukuru wadau wote waliojitokeza kufanikisha shughuli hiyo.

# Vodacom yaahidi ushirikiano na IPP Media kidijitali zaidi

**Na Mary Kadoke**

MKURUGENZI Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, ameahidi kufanya kazi na Kampuni ya IPP Media kitengo cha kidijitali ili kuongeza uhamasishaji wa huduma zao kwa wateja.

Aliyasema hayo jana katika ziara yake maalum IPP Media, Mikocheni jijini Dar es Salaam, yenye lengo la kufahamiana na kuweka mikakati ya kukuza maeneo ya biashara.

Besiimire alifurahishwa na uwekezaji uliofanywa na Kampuni hiyo upande wa dijitali aliyoitafsiri kama fursa ya uwekezaji itakayosaidia kuunganisha huduma zao kwa wateja nchini.

"Inafurahisha jinsi gani Kampuni ya IPP imewekeza upande wa dijitali. Ukiwa nje huwezi kuona jinsi taarifa zinavyochakatwa na umuhimu wake kwa jamii. Nimeona na nadhani ni fursa kubwa kwa Vodacom kuwekeza katika idara hii," alisema.

"Kampuni hii kwa asilimia kubwa inatoa huduma kwa vijana. Hivyo ni juu yetu kuja na huduma itakayowashirikisha zaidi ambapo kwa kushirikiana na idara ya dijitali ni mategemeo yetu kuwa huduma hiyo itajulikana na kutumiwa kwa wingi zaidi."

Kwa mujibu wa Besiimire, miongoni mwa mikakati yake ni kuongeza chachu kwa huduma zilizopo ili kufikia malengo ya kampuni hiyo.

"Nitahakikisha ninakuwa na utekelezaji wenye mafanikio katika miradi mbalimbali iliyokuwa inaendeshwa na kampuni. Mfano mzuri ni huduma ya M-Pesa ambapo safari hii itajikiza zaidi katika kukopesha wafanyabiashara."

Alisema pamoja na kuwa na mikakati hiyo, itaendelea pia kuhakikisha inaunga jitihada za serikali kupitia huduma za M-Kulima inayorahishisha mawasiliano na malipo kwa wakulima pamoja na huduma ya M-Mama inayosaidia wajawazito kupata huduma stahiki. Besiimire, aliteuliwa rasmi kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom, Oktoba 15, mwaka huu. Alijiunga na kampuni hiyo baada ya kuachana na MTN ya Afrika Kusini aliyoitumikia katika nafasi mbalimbali ikiwamo ya Ofisa mauzo, usambazaji na uendeshaji wa kikanda tangu 2019.

Bessimire ameshika nafasi ya Hilda Bujiku aliyekuwa akikaimu nafasi hiyo baada ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Sitholizwe Mdlalose kuondoka.



# Mama na watoto waliofariki dunia kwa ajali wakitoka mahafali wazikwa

**Na Waandishi Wetu**

VILIO, simanzi na majonzi jana vilitawala katika ibada ya kuaga miili ya Immaculata Byemerwa na wanawe wawili waliofariki dunia katika ajali Novemba 26, mwaka huu, eneo la Kibamba, mkoani Dar es Salaam, baada ya gari lao kupoteza mwelekeo na kutumbukia kwenye bonde.

Ibada hiyo ilifanyika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Tabata Kuu, na kuhudhuriwa na waombolezaji wakiwamo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salalm (UDSM) na Shule ya Sekondari Gili ya Kibaha, walikokuwa wanasoma watoto hao.

Watoto waliofariki katika ajali hiyo ni Jolister Byemerwa na Janeth Byemerwa huku kaka yao aliyekuwa dereva wa gari hilo, Albert Mrema, akiendelea na matibabu Hospitali ya Mloganzila, nje kidogo ya mkoa wa Dar es Salaam.

Akiongea kwa niaba ya familia kaka wa familia hiyo, Prince Byemerwa, alisema mdogo wake Janeth alikuwa mwanafunzi wa mwaka wa tatu fani ya Uhandisi UDSM na Jolister alihitimu kidato cha nne Shule ya Sekondari Gili, Kibaha.

"Mama na wadogo zangu walikuwa wanatoka kwenye mahafali ya mdogo wetu lakini kwa mapenzi ya Mungu hawakurudi nyumbani kama walivyoondoka.

Mama alikuwa na watoto saba sasa ametuacha watano, alikuwa anajishughulisha na ujasiriamali, alikuwa mcha Mungu na mcheshi muda wote alikuwa anatamani kuona tunafanikiwa," alisema.

Akihubiri kwenye ibada hiyo Mkuu wa Jimbo la Kati la KKKT, Mchungaji Frank Kimambo, aliwataka wananchi kuvichukulia vifo hivyo kuwa ni mpango wa Mungu badala ya kuhusisha na imani nyingine.

Alisema watu wanaishi katika dunia ya ahadi kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kumtanguliza Mungu mbele kwa kuwa hakuna anayeijua siku ya kuitwa.

"Katika maisha yangu ya uchungaji kwa miaka hii michache sijawahi kuongoza ibada ya kuwaaga mama na watoto, kwangu hili jambo zito niliumia sana nilipopata taarifa za vifo hivi," alisema.

**WANAFUNZI UDSM**

Akizungumza na gazeti hili, mwanafunzi aliyekuwa anasoma na Janeth, Hansi Suleimani, alimzungumzia kuwa alikuwa mcheshi, mwenye bidii, mcha Mungu na aliyekuwa anapenda kujituma katika kazi zake.

"Kama chuo tumepoteza mtu wa muhimu sana, Janeth alikuwa ni mwananfunzi wa mfano wa kuigwa alikuwa ana akili, anapenda kujituma na alikuwa na ushawishi mkubwa kwa wanafunzi wenzake. Nimeumia sana kwa sababu mimi nimesoma naye kuanzia shule ya msingi tukaachana sekondari baadaye tena tukakutana chuo kwa hiyo kwangu mimi alikuwa kama mwanafamilia kabisa nimeumia sana," alisema.

**MIILI YAZIKWA**

Miili yao ilizikwa jana katika nyumba ya familia eneo la Mwendapole Kibaha, kwa mamia ya waombolezaji kuwasindikiza wana familia.

Geoffrey Frank mwangalizi wa nyumba ya familia hiyo alisema: "Siku ya mahafali mama alinipigia simu akiniambia nimnunulie korosho nimpelekee kwenye mahafali nikafanya hivyo na baada ya hapo nilibaki hadi shughuli ilipoisha."

Kwa mujibu wa Frank, walipotoka kwenye mahafali mama alitaka kufika kwenye nyumba yake, lakini watoto walitaka kurudi Dar es Salaam na alikubaliana na wanawe.

Alisema walifika kwenye nyumba hiyo majira ya saa 11 jioni wakitokea kwenye mahafali, walikagua nyumba na kisha wakampa maelekezo ya kazi halafu wakaondoka.

"Majira ya saa moja nilipokea simu kutoka kwa ndugu wa karibu wa mama ambaye alifika nyumbani akanikosa nilikuwa barabarani, akinitaka nirejee kuna taarifa muhimu anataka kunipa, akanijulisha kwamba mama na wanawe wamefariki," alisema.

Alisema alipopiga namba ya mama ilikuwa inatumika na baadaye ilizimwa ndipo walipoondoka kwenda Mloganzila kuulizia mapokezi ambako walielezwa kuwa mama tayari amefariki na amepelekwa mochwari na binti aliyekuwa anahitimu kidato cha nne mwili wake ulikuwa unatolewa kwenye gari iliyowatoa eneo la ajali huku dada wa binti huyo akiwa anapatiwa matibabu.

"Tulipojieleza mapokezi tuliambiwa tukaangalie kama tunaowaulizia, tukagundua Jolista mwili wake ulikuwa unashushwa kutoka kwenye gari," alisema.

●**Imeandikwa na Halfani Chusi (DAR) na Julieth Mkireri (PWANI)**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 01/12/2022

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 04/12/2022 kampuni ya LIUHE INTERNATIONAL LTD itasafirisha Gari yenye vipimo vikubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Kigoma Gari hiyo yenye namba za usajili:

**T203DQG/T984DMA**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**I.T203DQG/T984DMA** **Urefu - 21m Upana - 4.4m, Kimo-5.2m**

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam hadi Kigoma** Kupitia **Dodoma** gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

17174801


# TASAC yaibuka mshindi uandaaji hesabu kimataifa

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limeibuka mshindi wa kwanza wa uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2021, katika kundi la udhibiti wa hesabu kwa watu wanaotumia mfumo wa hesabu kimataifa na kukabidhiwa tuzo na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo juzi, Mkurugenzi wa Huduma wa TASAC, Rajab Moses, alisema wamepata tuzo hiyo kwa mara ya pili mfululizo huku siri ya mafanikio ikiwa ni pamoja na kuweka kumbukumbu zao vizuri na kwa uwazi.

"Hili ni shirika ambalo limekasimiwa mamlaka na serikali na inategemewa mashirika haya yakusanye fedha, ili zitumike kwenye miradi ya maendeleo, kwa hiyo tuna mifumo mizuri ya udhibiti na uandaaji na ndio maana tumepata mara ya pili mfululizo na tumejipanga kuendelea kubaki katika nafasi hii kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu," alisema Moses.

Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA, Prof. Sylvia Temu, alisema vigezo vilivyozingatiwa katika kutoa tuzo hizo ni vya aina mbili, ikiwamo vya uandaaji wa taarifa za hesabu kimataifa kwenye taasisi mbalimbali za kutengeneza faida na ambazo hazitengenezi faida.

"Katika uandaaji wa taarifa za hesabu, tuna viwango vya kimataifa ambavyo vinahusika na kuhusisha taasisi zile ambazo zina mrengo wa kutengeneza faida, na pia viwango vya kimataifa ambavyo ni kwa ajili ya taasisi za serikali na taasisi ambazo siyo za kutengeneza faida," alisema na kuongeza: "Kwa hiyo tumezingatia hivyo viwango vya kimataifa ambavyo vinatoa uhitaji wa kuonyesha mambo mbalimbali ya muhimu ambayo ni lazima yaonyeshwe kwenye taarifa za hesabu."

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuongeza uwazi, kuwasaidia watumiaji wa taarifa za hesabu kuzielewa kwa kina na pale wanapokuwa na maswali wafanye hivyo. "Kwa mfano kampuni au taasisi zinazohitaji wawekezaji utaratibu huu unasaidia kuwavutia, kwa sababu unapotoa taarifa za ndani, zinazovutia kuonyesha utendaji wako na wanapozielewa ndio zitawasaidia kufanya uamuzi wawekeze kwako au laa."

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Zanzibar, Jamali Kassimu Ali, aliwataka viongozi wa taasisi mbalimbali kuhakikisha wanaweka vizuri taarifa za hesabu katika taasisi zao, ili kurahisisha shughuli mbalimbali ikiwamo za uwekezaji.


TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD

TANESCO

Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/N/39

For

VALUATION OF PROPERTIES FOR COMPENSATION OF GRID IMARA TRANSMISSION LINES LOT 1, 2, 3, 4, 5, AND 6

NOTICE TO THE PUBLIC

Date: 02/12/2022

TANESCO hereby informs the public that, the above mentioned Tender has been advertised on TANePS. Interested applicants can access the Tender Documents through **www.taneps.go.tz**

MANAGING DIRECTOR
TANESCO LIMITED

17175102

# MKURUGENZI MTENDAJI WA VODACOM TANZANIA, PHILIP BESIIMIRE ATEMBELEA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire (kushoto), akikaribishwa na Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, baada ya kuwasili katika ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian, Mikocheni Viwandani, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga (wa pili kushoto), Meneja wa kiwanda cha uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (wa tatu kushoto) na Meneja wa Fedha wa kampuni hiyo, Samwel Orgeness. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (katikati), akitoa maelezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni hiyo.



Meneja wa kiwanda cha uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam, akitoa maelezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, kuhusu uzalishaji wa magazeti.



Mratibu wa Vipindi wa EATV, Sophia Mganya (wa pili kushoto), akifafanua jambo kwa Philip Besiimire (kulia), kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na kituo hicho.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Michezo cha Radio One, Amri Masare (kushoto), alipotembelea studio za redio hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire (kushoto), akifurahia jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile (katikati) na Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga, katika studio ya kusomea taarifa ya habari ya ITV.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rais Samia amestahili udaktari wa heshima

**CHANDA** chema huvishwa pete. Huu ni msemo wa wahenga unaobainisha kuwa kila mtu anayefanya mema, hupewa tuzo maalum ikiwa ni kutambua mchango wake na wema anaoufanya katika jamii husika. Hivyo ndivyo, Rais Samia Suluhu Hassan alitunukiwa shahada ya heshima ya udaktari wa fasihi (Doctor of Letter- Honoris Causa) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tangu aingie madarakani Machi 19, 2021 Dk. Samia amefanya mambo mengi kwa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ambayo Watanzania wengi wamekuwa wakipongeza. Mambo mengi yalikuwapo yakiwamo manung'uniko ya baadhi ya watu hali iliyofikia mahali mpaka akaambiwa na baadhi ya viongozi wa dini kuwa ana wajibu mkubwa wa kutibu majeraha ya Watanzania.

Katika muda ambao haujafika miaka miwili, hakika ameonyesha nuru ya safari ya Watanzania kusonga mbele kimaendeleo katika nyanja mbalimbali. Kabla ya kutunukiwa shahada hiyo, zilisomwa sifa zilizomstahilisha ambazo alipopewa nafasi ya kuzungumza, alikiri dhahiri kwamba zinamfaa kutunukiwa shahada hiyo licha ya kwamba alisema mwanzoni aliona kama hastahili.

Katika wasifu uliosomwa kuhusu Rais Samia na mambo ambayo yamefanya atunukiwe shahada hiyo ni pamoja na kuleta mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na kuleta utengamano na matumaini mapya kwa taifa la Tanzania. Katika hotuba yake ya kwanza kabisa aliyoitoa baada ya kuapishwa, aliwasihi Watanzania kusimama pamoja na kushikamana, kuzika tofauti zetu na kuwa wamoja kama taifa. Pia alisisitiza kuonyeshana upendo, kudumisha amani, kuenzi utu na uzalendo wetu na kwamba umefika wakati wa kutazama mbele kwa matumaini na kuweka nguvu kwa pamoja kujenga Tanzania mpya. Mambo hayo ambayo aliyasisitiza na akiwa amekaa madarakani kwa mwaka mmoja na miezi minane, amefanya mambo ambayo yanaonekana yakiwamo kuinua uchumi wa taifa, kujenga uhusiano wa kiuchumi kitaifa, kikanda na kimataifa. Juhudi zake pia zimewezesha upatikanaji wa mabilioni ya fedha za misaada, mikopo na uwekezaji katika miradi mikubwa kama vile barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, elimu na afya.


Pia ameonyesha dhamira ya kweli ya kukuza uchumi wa nchi hasa kwa kuelekeza nguvu kubwa katika sekta ya kilimo ambayo ni mwajiri wa takriban asilimia 70 ya Watanzania. Ili kufanikisha hilo, serikali yake kwa mwaka 2022/23 imeongeza bajeti hadi kufikia Sh. bilioni 954 na kushusha bei ya mbolea kwa asilimia 50.

Sambamba na hiyo, ameweka juhudi kubwa katika kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji na sekta binafsi ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi wa ndani na nje na kukuza sekta binafsi. Juhudi hizo ni pamoja na kupunguza vikwazo katika upatikanaji vibali na leseni za biashara na kurekebisha kodi mbalimbali.

Katika siasa, ndani ya kipindi kifupi, uongozi wake umeonyesha nia thabiti ya kupanua ushiriki wa vyama vya siasa katika siasa za nchi. Pia utawala wake umepunguza kwa kiasi kikubwa, sintofahamu za kisiasa na kuashiria matumaini mapya ya amani na ushirikiano. Katika azma yake ya kujenga demokrasia na umoja, amechukua hatua za makusudi kuleta maridhiano kati ya vyama vya siasa kwa kuunda Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa.

Pia ameonyesha dhahiri na kusisitiza kwa vitendo umuhimu wa kuzingatia haki za binadamu katika uongozi ikiwamo kuimarisha usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali na kukemea unyanyasaji na ukatili wa kijinsia. Yako mengi ambayo Dk. Samia ameonyesha katika uongozi wake kuwa amestahili kupata shahada hiyo ya udaktari wa heshima na Watanzania wanapaswa kumpongeza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii ijitose kuokoa maisha na afya za makundi haya muhimu

Na Sabato Kasika

**WANAWAKE** na wasichana wanatajwa kuwa wako hatarini zaidi kuuawa majumbani, na kwamba zinahitajika jitihada zaidi za kuwanusuru katika mazingira hayo, ili waendelee kuwa salama.

Ripoti ya utafiti mpya iliyotolewa mwezi huu na Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Wanawake (UN Women) na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Dawa na Uhalifu (UNODC), iliyowekwa mitandaoni, inaeleza kuwa makundi hayo yako katika hatari hiyo.

Inaeleza kuwa wastani zaidi ya wanawake au wasichana watano waliuawa kila saa na wenza wao au jamaa wa familia kwa mwaka 2021, huku ikikumbusha kuwa ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni moja ya ukiukwaji mkubwa zaidi wa haki za binadamu duniani.

Kwa mujibu wa utafiti huo, miongoni mwa wanawake na wasichana wote waliouawa mwaka jana, asilimia 56 waliuawa na wenza wao, jamaa wa familia sawa na watu 45,000 kati ya 81,000, huku ripoti ikieleza kuwa nyumbani sio mahali salama kwa wanawake na wasichana wengi.

Hayo yaliyoelezwa na ripoti hiyo, ninadhani ni vyema yakatusaidia kila mmoja ili kuhakikisha mwanamke au msichana anaondokana na hofu kuhusu usalama wake bali apaone nyumbani kama sehemu salama.

Ninadhani njia nzuri ni jamii kuhusika katika vita ya kukomesha aina zote za mauaji ya kijinsia kwa wanawake na wasichana, kwa kudhibiti vyanzo vya mauaji, ili kuwa na jamii iliyostaarabika.

Hapa nchini wapo wadau mbalimbali wanaopambana kwa hali na mali ili kuhakikisha kunakuwa na usalama, hasa kwa kuzingatia kwamba hakuna binadamu mwenye haki ya kukatisha uhai wa mwenzake.

Wakati huu wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, ninaamini kwamba jamii ikielimishwa vya kutosha, ukatili wa kijinsia unaweza kuzuilika na hivyo kumfanya kila mmoja kuwa na afya njema.

Ikumbukwe kuwa ukatili huo umekuwa ukisababisha vifo au kuacha wengine wakiwa na ulemavu wa kudumu kwa maana kwamba kiafya wanakuwa hawako sawa, hivyo maadhimisho yangekuja na matokeo chanya. Elimu inaweza kusaidia uzuiaji wa msingi kwa kushughulikia sababu kuu za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana ikiwa ni pamoja na kubadilisha tabia mbaya za mfumo dume. Kupitia elimu, jamii inaweza kuondoa tofauti za kimuundo za kijinsia na itikadi kali za kijinsia na hivyo kusababisha kuwa na jamii yenye kuheshimu utu wa mtu mwingine wa jinsi ya kike au ya kiume.

Ukatili una matokeo mabaya kwa wanawake na wasichana au kwa watu wote, kwani madhara yake hudumu katika kipindi chote cha maisha na yanaweza kuharibu fursa ya mtu kuishi maisha mazuri, yenye afya na yenye mafanikio.

Kwa ujumla ni kwamba, ukatili huo una athari kiafya, kimwili, kisaikolojia na kiroho. Unaathiri uwezo wa mtu kushiriki katika masuala ya kiuchumi na kufifisha uwezo wake katika kuboresha maisha ya familia.

Ukuaji wa ubongo wa mtoto huathirika pindi wanapopatwa au kushuhudia vitendo vya kikatili. Nafasi yao ya kukua kimwili na kiafya inaathirika. Watakuwa hawafanyi vizuri darasani na kuna uwezekano wa kusababisha ukatili na kuwa na tabia isiyokubalika katika jamii na shuleni.

Hivyo, ukatili haupaswi kuwa sehemu ya maisha ya kila siku kwa wanawake na wasichana ambao kimsingi ndio wanaotajwa kuwa waathirika wakubwa wa vitendo hivyo ambavyo wakati mwingine vinaondoa uhai wa mtu. Unapotajwa ukatili si wa kipigo tu, bali upo wa kingono ambao huwa unatajwa kuwa ni doa katika mtu na huweza kudumu kwa muda mrefu bila kufutika katika moyo wa mtendewa.

Jamii ijitose katika vita hiyo ikitambua kuwa ukatili wa aina zote ni tishio kwa usalama wetu sote na ni doa katika utu wa mtu, hivyo kwa pamoja tunaweza kukutokomeza iwapo tutakuwa na nia ya dhati.

# Wizara yajivunia matukio ukatili kudhibitiwa nchini

**Na Christina Haule,** MOROGORO

NAIBU Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, amesema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamefanikiwa kupunguza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Akifungua kikao kazi cha kuandaa mpango kazi wa kitaifa wa kutekeleza ajenda ya wanawake, amani na usalama alisema jitihada hizo zina lengo kuyakomboa makundi hayo.

Kikao hicho kilifadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN-Women) kutoka Canada na Ubalozi wa Denmark.

Mpanju alisema serikali inatambua umuhimu wa kutekeleza ajenda ya wanawake, amani na usalama pamoja na kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana, na kwamba kwa kuona umuhimu huo imeamua kuendeleza jitihada za kuwashirikisha wadau wa maendeleo katika kuandaa mpango kazi wa kitaifa ambao utawezesha kutekeleza Azimio la Umoja wa Mataifa (UN) namba 1325 kuhusu wanawake, amani na usalama.

"Msukumo mkubwa unawekwa katika suala la uingizaji wa masuala ya kijinsia katika sera, mikakati na programu za kisekta ikiwemo usawa wa kijinsia nchini, tunazungukwa na nchi nane, sababu nchi nyingi kuna mapigano ya ndani, vurugu za kikabila, vurugu za kisiasa, uhamaji ambao pia una madhara kwenye taifa letu hivyo ni vyema kuwekwa misingi imara ya kulinda amani na usalama wa mwanamke," alisema Mpanju.

Aidha, Mpanju alisisitiza mpango kazi huo ambao ni kwa ajili ya Watanzania ni muhimu ukashirikisha wadau katika majadiliano na uibuaji wa mikakati ya utekelezaji, ili kuwa na mpango unaotekelezeka na kutoa majibu kwa yale ambayo yanaendana na mazingira ya kitanzania.

Mshauri Mbobezi wa Sera na Mipango kutoka UN-Women, Usu Mallya, akizungumzia mpango mkakati wa kitaifa waliokubaliana na walivyojipanga katika kuandaa rasimu ya mpango wa kwanza wa amani na usalama kwa wanawake nchini, alisema rasimu hiyo itakuwa na sura kubwa tano ambazo zitaboreshwa kulingana na mahitaji.

Alisema rasimu hiyo itakuwa na mambo kadhaa ikiwemo historia ya Tanzania katika kujishughulisha na mambo ya usalama na amani kwa mwanamke ndani na nje ya nchi, sambamba na kuangalia sera na sheria zinazohusiana na masuala ya amani na usalama kwa wanawake kwa kuangalia jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali.

"Sura ya pili itaingia zaidi katika kuangalia hali halisi inayotokana na utafiti uliofanyika kwenye mikoa 11 nchini Tanzania, ikiwemo bara mikoa tisa na Zanzibar miwili ambayo iliangalia hali halisi ya utekelezaji wa mikakati na masuala yanayohusu amani na usalama wa mwanamke," alisema Malya.

Mmoja wa washiriki wa mpango mkakati huo kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Reinfrida Mathayo alisema mpango huo unazingatia ajenda kubwa nne ikiwemo ushirikishwaji wa mwanamke katika ngazi zote kutoka ngazi ya vijiji mpaka mikoa, pamoja na mwanamke kulindwa.



Mkurugenzi Mtendaji wa KPMG, Alex Njombe (kushoto), akikabidhi tuzo kwa Dk. Venance Mwasse, kwa kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu Bora namba mbili kwa mwaka 2022 kundi la Mashirika ya Umma, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wana-CCM wamfagilia Mwinyi umakamu M/kiti

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar (CCM), wamesema Dk. Hussein Ali Mwinyi atakapokabidhiwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti visiwani humo atakuwa mwarobaini wa matatizo yanayojitokeza katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi 2020/2025.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti, wanachama wa mikoa tofauti ya Unguja, walisema wanaridhishwa na uwezo wa Rais Mwinyi katika kuiongoza nchi na kuiletea maendeleo ya sekta mbalimbali.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni (CCM) kwa kipindi cha miaka kumi (2000-2010), ParmukHoogan Singh, alisema Dk. Mwinyi ameonesha dhamira ya dhati kuondoa vikwazo vinavyorudisha nyuma maendeleo ikiwamo rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma.

Alisema katika miaka miwili ya uongozi wake amedhihirisha kukerwa na vitendo hivyo pamoja na kuvitaka vyombo vya sheria pamoja na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), vinachukua hatua vinapobaini mtendaji au kiongozi yeyote anajihusisha na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali za serikali bila kumuonea haya.

Singh alisifu utaratibu ulioanzishwa na Rais Mwinyi, kutaka ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kila mwaka isomwe hadharani ili wananchi watambue kila uovu unaofanywa na watendaji wa serikali waliopewa dhamana kutunza na kuzitumia fedha zao kwa maslahi ya taifa.

Alisema maono ya Dk. Mwinyi ni urithi kutoka kwa baba yake, ambaye wakati akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa kiongozi mwadilifu, mkweli, mcheshi na hakuwa na muhali kwa watendaji wazembe na wala rushwa.

Naye Khamis Ali Kaambwa, mkazi wa Mpapa Wilaya ya Kati, alisema Dk. Mwinyi ni tegemeo kubwa la Wazanzibari kwa vile anaongoza kwa Ilani ya CCM na tayari ameonesha ishara njema ya kuifungua nchi na kuiweka kwenye ramani ya dunia kiuchumi, amani na ustawi wa wananchi.

Alisema akipewa kofia ya pili kuwa Makamu Mwenyekiti atakwenda kukiimarisha chama kwa kupanga upya safu ya uongozi kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar na ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Catherine Pascal Mgoli, alisifu utamaduni wa CCM kukabidhiana uongozi, kuwa haukumbatii uchu wa madaraka na chaguzi zilizofanyika katika ngazi tofauti, ni kielelezo cha utawala bora ndani ya chama unaoangalia uwezo wa mgombea badala ya mizengwe na rushwa.

Alisema Rais Mwinyi ameshawekewa misingi mizuri ya kukisimamia chama na mtangulizi wake Dk. Ali Mohamed Shein.

Wanachama na wananchi mbalimbali waliotoa maoni yao, wameeleza matumaini yao kwamba kukabidhiwa kofia ya umakamu wa chama kwa Dk. Mwinyi, kutaongeza nguvu ya mabadiliko ya kiuchumi na kuipaisha dhana ya uchumi wa buluu.

Baada ya kumaliza chaguzi ngazi za matawi, majimbo, wilaya, mikoa pamoja na jumuiya zake na tayari viongozi wamepatikana, Chama Cha Mapinduzi kinatarajia kufanya mkutano wake mkuu taifa Desemba 7 hadi 8, 2022, jijini Dodoma.

Uchaguzi huo utahusisha nafasi ya Mwenyekiti taifa, Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar pamoja na wajumbe 20 kila upande watakaoingia katika Halmashauri Kuu taifa.

Kutokana na mabadiliko makubwa yaliyofanywa ndani ya chama hicho, nafasi za wajumbe sasa zitakuwa 20 kwa Zanzibar na pia Tanzania Bara kutoka 15 za awali, na tayari majina ya wagombea yameshapitishwa baada ya mchujo wa waombaji waliokuwa wamejitokeza.

## KABWELA



# Ofisa afukuzwa kazi, wengine kukatwa mishahara miezi 36

**Na Daniel Limbe,** KAKONKO

KATIKA kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwa watumishi wa umma, Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma limeazimia kufukuzwa kazi Ofisa Ugavi Msaidizi, Msafiri Hiza huku Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Edward Malima akishushwa cheo na mshahara.

Uamuzi huo ulifikiwa juzi kwenye kikao cha dharura kilichoitishwa kwa ajili ya kutoa uamuzi wa ripoti ya uchunguzi uliofanywa na tume ya mkoa huo ambayo ilibainisha makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa maadili ya utumishi ikiwamo ubadhirifu wa fedha za umma.

Akitangaza uamuzi huo kwa niaba ya madiwani wenzake, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Fidel Nderego alisema kutokana na uchunguzi kuthibitisha watumishi hao walihusika kwa namna moja au nyingine na dosari zilizobainika, baraza hilo limeazimia hatua kali kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kumfukuza kazi ofisa ugavi msaidizi.

"Mbali na Msafiri Hiza, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Malima naye ashushwe cheo pamoja na mshahara wake. Ofisa Ugavi Daraja la Pili, Linus Kagoma atakatwa mshahara wake kwa asilimia 15 kila mwezi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo pamoja na Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari, Sebastian Bukombe, naye akatwe asilimia 15 ya mshahara wake kwa kipindi cha miaka mitatu," alisema Nderego.

Pasipo kutaja jumla ya kiasi cha fedha kilichotafunwa na watumishi hao, Nderego alisema uamuzi huo unalenga kuziba mianya ya wizi wa fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi, akisisitiza halmashauri hiyo siyo 'shamba la bibi'.

Akizungumza kwa njia ya simu akiwa jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kakonko, Saamoja Sadock, mbali na kulipongeza Baraza la Madiwani kwa uamuzi wake, aliwatahadharisha watumishi wengine wenye lengo la kuhujumu fedha zinazotolewa na serikali kwamba chama hakitokubali kufumbia macho vitendo hivyo.

"Watumishi wenye maadili tunawapenda lakini wanaohujumu fedha zinazotolewa na serikali, kamwe hatutowafumbia macho, lazima fedha ziende kwenye miradi iliyokusudiwa ili kupunguza adha kwa wananchi.

"CCM ndiyo tunaoisimamia serikali, hivyo mambo yanapoharibika, hasira za wananchi zinakigharimu chama kwenye sanduku la kura," alisema Saamoja.

Alitumia fursa hiyo kuipongeza tume iliyoundwa na Mkoa wa Kigoma kufanya uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa fedha kwenye Halmashauri ya Kakonko kwa kuwa imesaidia madiwani hao kuchukua hatua stahiki.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, wakiwamo Adellina Chabilonda na Andrea Jonathan, walisema hatua iliyofikiwa na madiwani hao siyo ya kupongezwa kwa kuwa watumishi hao wote walipaswa kutimuliwa kazi.

Walisema uamuzi huo wa madiwani unatoa nafasi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

## Wataka lugha alama mikutano ya viongozi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JAMII ya watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi), imeiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, kutoa mwongozo wa kuruhusu kuanza kwa matumizi ya lugha ya alama katika maeneo mbalimbali ya huduma na hotuba za viongozi wa kitaifa.

Matumizi ya lugha hiyo yatasaidia kuwapa nafasi ya kujua kinachoelekezwa na kushiriki shughuli za ujenzi wa taifa.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Viziwi Tanzania, Mch. Joseph Hizza, alisema jana kwamba jamii hiyo ya wenye ulemavu wanajisikia vibaya wanapokosa hotuba za Rais Samia Suluhu Hassan, anapolihutubia taifa au kuzindua miradi mbalimbali.

Aidha, jamii hiyo imeiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, kuonyesha mfano kwa kuanzisha bodi inayosimamia lugha ya alama kama ilivyo kwa bodi nyingine.

"Vikwazo vya mawasiliano au ukosefu wa lugha za alama, unatukwaza na kutuma vikwazo sisi watu wenye ulemavu wa kutosikia. Hebu wavae viatu vyetu, waone Mkuu wa nchi anazungumza halafu hujui anazungumza nini," alisema.

Alisema hata kwa upande wa vyombo vya habari hasa televisheni nyingi hazina watu wa lugha za alama, hivyo nao kukosa haki ya kupata habari.

"Tunaomba muongeze nguvu zaidi katika kuhakikisha inatekeleza sheria zinazozingatia mahitaji na haki za watu wenye ulemavu ikiwamo hii ya mawasiliano kwa kuhakikisha matajiri wakalimani kwa wingi, kurekebisha mapungufu yaliyoko,"alisema.

Aidha, Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Selina Mlemba, alisema hata kwenye matukio ya mijadala muhimu ya kitaifa, imekuwa ikipita bila kuwafikia miongoni mwao.

Alisema tatizo la lugha ya alama kutopewa uzito, limeanza kwa viongozi wa kitaifa na kushuka chini hadi ngazi ya familia.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Jamal Kassim Ali, akimkabidhi tuzo Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo (kulia), baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa mwaka 2021 katika kundi la Taasisi za Fedha kwenye Tuzo za Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) zilizofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Hoteli ya APC jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# CRDB yang'ara Tuzo za NBAA

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara ya tatu mfululizo Benki ya CRDB imetunukiwa tuzo ya uwasilishaji wa taarifa bora za fedha kwa upande wa taasisi ya fedha kwa mwaka 2022 na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Tuzo hiyo ilitolewa juzi wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa NBAA na hafla ya kuadhimisha miaka 50 ya taasisi hiyo iliyofanyika mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wataalamu na wabobezi wa masuala ya uhasibu kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Akikabidhi tuzo hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Jamal Kassim Ali, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuendelea kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa katika utayarishaji wa taarifa zake za kifedha, jambo ambalo limeifanya benki hiyo kuendelea kuibuka kinara.

Waziri Ali alisema kuandaa ripoti za mwaka za mashirika na taasisi za umma kwa viwango vya kimataifa kunazipatia mamlaka za usimamizi pamoja na wawekezaji na wananchi fursa na uwezo wa kupima ufanisi wa utendaji kazi wa taasisi husika na kuona namna inawajibika ipasavyo katika kusimamia rasilimali na mikakati ya uendeshaji.

"Tuzo hii inadhihirisha ni jinsi gani benki hii imewekeza katika mifumo ya kisasa ya uendeshaji ambayo si tu inaongeza ufanisi bali pia inawezesha wadau wenu kupata taarifa za viwango, hongereni sana," alipongeza waziri huyo akizitaka taasisi na mashirika mengine kuiga mfano huo alioutaja ni ishara ya utawala bora.

Akipokea tuzo hiyo, Ofisa Mkuu wa Fedha Benki ya CRDB, Fredrick Nsekanabo alisema benki hiyo inatambua umuhimu wa kuandaa taarifa za fedha kupitia mifumo inayozingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.

Alisema kupata tuzo hiyo kwa mara ya tatu mfululizo kunaifanya benki hiyo kuendelea kuongeza jitihada ili kuhakikisha inatoa taarifa zilizo bora zaidi.

"Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita tumefanya uwekezaji mkubwa katika mifumo ya kidijitali, hii ni pamoja na kuboresha mifumo yetu ya kukusanya na kuandaa taarifa.

"Tumeweza pia kuunganisha mfumo wetu wa utoaji taarifa za fedha na mfumo wa kimataifa wa kuandaa taarifa za fedha (IFRS), hii pia imechangia benki yetu kuwa bora zaidi," alisema.

Nshekanabo aliongeza kuwa ushindi huo pia unatokana na benki hiyo kuwa na mfumo bora wa uongozi unaozingatia misingi ya utawala bora, weledi, uwazi wa taarifa za kifedha, uwajibikaji na kiwango cha juu cha uadilifu wa takwimu.

"Hivi ni vitu ambavyo Mkurugenzi Mtendaji wetu, Abdulmajid Nsekela na sisi kama benki kwa ujumla tumekuwa tukiviwekea mkazo mkubwa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, Pius Maneno alisema Benki ya CRDB imeibuka kinara baada ya kukidhi vigezo vyote vilivyowekwa na taasisi hiyo kwa zaidi ya asilimia 90. Alisema kwa mwaka 2022 taasisi zaidi ya 60 zimeshindanishwa katika tuzo hizo zilizojumuisha vipengele 13.

Mwaka 2022 umekuwa wa mafanikio kwa Benki ya CRDB ambapo mbali na tuzo hiyo ya NBAA, benki hiyo pia imetunukiwa tuzo za Benki Bora Tanzania na majarida maarufu duniani ya fedha na uchumi ya Euromoney na Global Finance.

# PSSSF yatwaa Tuzo ya Umahiri uwasilishaji mahesabu

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umetwaa Tuzo ya Umahiri katika Uwasilishaji wa Taarifa za Mahesabu kwa mwaka 2021, kundi la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya.

Tuzo hiyo inayotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), imepokewa na Mkurugenzi wa Fedha, PSSSF, Beatrice Musa-Lupi, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam, juzi na mgeni rasmi alikuwa ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, CPA. Jamal Kassim Ali.

PSSSF imetwaa tuzo hiyo ya umahiri katika uandaaji wa Taarifa za Fedha ya Mwaka 2021 (Best Presented Financial Statements for the Year 2021 Awards) kwa mwaka wa pili mfululizo.

Akizungumzia ushindi huo, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema, tuzo hiyo itaongeza chachu kwa watumishi wa PSSSF katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia weledi na kuendelea kutoa huduma bora kwa wanachama wa Mfuko.

Aidha, Mkurugenzi wa Fedha PSSSF, Musa-Lupi, alisema ushindi huo ni ishara ya mfuko huo unaandaa mahesabu kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kimataifa, pia inaashiria uwapo wa weledi wa tasnia husika kwa upande wa watumishi.

"Sambamba na hayo niliyoyasema pia inaashiria uwapo wa usimamizi makini wa fedha za wanchama na hii inatupatia heshima kama taasisi," alisema.

Aliwahakikishia wanachama dhamira ya PSSSF ya kuhakikisha usalama wa michango yao unazingatiwa kwa kiwango cha juu wakati wote, ikiwa ni pamoja na kuwapo uwazi kwenye usimamizi na utunzaji wa rasilimali za Mfuko.

"Ushindi huu pia unaashiria uwepo wa kesho ya wanachama wetu kama kaulimbiu yetu inavyosema 'Leo. Kesho. Pamoja.'"



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Jamal Kassim Ali (kushoto), akimkabidhi tuzo ya umahiri katika uandaaji na uwasilishaji taarifa za fedha kwa mwaka 2021, Mkurugenzi wa Fedha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Beatrice Musa-Lupi, wakati wa kilele cha miaka 50 ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu Tanzania (NBAA), jijini Dar es Salaam.

# Mabula ashangazwa utendaji maofisa ardhi

**Na Munir Shemweta,** IRINGA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesikitishwa na watendaji wa sekta ya ardhi katika Halmashauri za Manispaa na Wilaya ya Iringa kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Hatua hiyo imesababaisha halmashauri hizo kushindwa kukusanya maduhuli ya serikali yatokanayo na kodi ya pango la ardhi.

Dk. Mabula alieleza kusikitishwa huko juzi akiwa katika ziara ya siku moja ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kubaini uzembe wa baadhi ya watendaji, wakiwamo maofisa ardhi wateule.

Waziri alisema watendaji hao wameshindwa kusimamia utoaji hati za ardhi na uingizaji miliki za ardhi kwenye mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi kwa njia ya kielektroniki.

Aliwataka maofisa ardhi wateule katika halmashauri hizo kujitathmini kutokana na kushindwa kwenda na kasi ya serikali ya kuhakikisha wananchi wanamilikishwa na kupatiwa hatimiliki za ardhi.

Aidha, Waziri Mabula aliwataka maofisa hao wa ardhi katika halmashauri hizo mbili za mkoa wa Iringa kuhakikisha ndani ya mwezi huu, wawe wamewasilisha taarifa zao za makusanyo ya kodi ya pango la ardhi na hatua walizochukua kwa wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi.

"Maana hata idadi ya viwanja mlivyo navyo hamvijui hilo ni kosa. Unawezaje kukaa bila kujua idadi ya viwanja vyako katika halmashauri yako? Nataka kabla sijaondoka hapa nijue idadi ya viwanja mlivyo navyo ni vingapi na vingapi viko kwenye mfumo na kwa nini havijaingia kwenye mfumo kwa hundred percent (asilimia 100)," alisema.

Dk. Mabula aliongeza kuwa: "Mtendaji wa sekta ya ardhi hajui idadi ya viwanja vilivyoko kwenye mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi, anawezaje kudai madeni? Wamiliki wa ardhi wanapotambulika kwenye mfumo inakuwa rahisi kwa watendaji kudai madeni.

"Huna idadi maalum ya viwanja na hujaingiza kwenye mfumo wa utunzaji kumbukumbu, sasa unawezaje kudai madeni?"

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri katika mkoa wa Iringa kutimiza wajibu wao wa kuzisimamia idara za ardhi kwenye halmashauri zao kwa kuwa idara hizo ni zao na si za wizara huku akibainisha kuwa watendaji wa sekta ya ardhi ni chachu ya kutoa elimu katika masuala ya ardhi.

Katika ziara yake Dk. Mabula alikutana na watumishi wa sekta ya ardhi kutoka ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Iringa na wale wa halmashauri za Manispaa na Wilaya ya Iringa kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa sekta ya ardhi.

Mkoa wa Iringa una halmashauri tano ambazo ni Manispaa ya Iringa, Mafinga Mji, Wilaya ya Iringa, Wilaya ya Kilolo na Wilaya ya Mufindi.

# Serukamba awaonya viongozi ushirika ubabaishaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewataka viongozi wa vyama vya ushirika nchini kuacha ubabaishaji na vikwazo vinavyosababisha baadhi ya wakulima kuogopa kujiunga na vyama hivyo kwa kuhofia kukosa masoko ya uhakika.

Alisema hayo jana wakati akifungua mkutano mkuu wa 27 wa ushirika wa mwaka 2022 unaofanyika mjini hapa.

Serukamba alisema, serikali hairidhishwi na utendaji kazi wa vyama vya ushirika hasa katika kuwatafutia wakulima masoko ya uhakika ya mazao yao na kuongeza ajira kwa vijana kupitia kilimo. Aidha, alisema wakati umefika kwa vyama vya ushirika kutumia njia za kidijitali kutafuta masoko ya mazao ndani na nje ya nchi badala ya njia za kizamani zilizopitwa na wakati. Alisema vyama vya ushirika kwa sasa havina msaada mkubwa kwa wakulima kwa kuwa haviwasaidii kupata pembejeo wala masoko na utaalamu ikilinganishwa na ushirika wa kipindi cha nyuma na wanaushirika waliwasomesha watoto wao kwa kupitia ushirika huo.

"Lazima tutafute msingi wa vyama vya ushirika ili viweze kuwasaidia na kuwakomboa wananchi kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma ambapo uliweza kusaidia kusomesha na ulisaidia kudai uhuru," alisema. Alisisitiza uwazi katika shughuli za ushirika kwa kuwa chombo hicho ni cha hiari kujiunga na ni muhimu wanachama wajue kinachoendelea katika vyama vyao.

Alisema wapo wakulima waliopeleka mazao yao katika ushirika, lakini mpaka sasa hawajaweza kupata fedha zao kutokana na ushirika kushindwa kuwatafutia masoko ya uhakika.

Alisema wakulima kabla ya kutambua aina ya zao analolima ni muhimu kuangalia sokoni ili kujua mahitaji ya soko na ushirika ndiyo chombo pekee kitakachoondoa utapeli na madalali katika kilimo ambao husababisha wakulima kuuza mazao yao yakiwa shambani kwa bei ndogo.

# Waziri ataka kipaumbele matumizi ya takwimu uzalishaji wa chakula

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema matumizi ya takwimu yanapaswa kupewa kipaumbele kipindi hiki ambacho mabadiliko ya tabianchi yameathiri uzalishaji katika kilimo na lishe, pamoja na kutishia usalama wa chakula katika baadhi ya nchi za Afrika.

Dk. Nchemba aliyasema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, katika Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika yanayofanyika mkoani hapa.

"Sekta ya kilimo kwa nchi za Afrika kwa kiwango kikubwa inategemea mvua, hivyo katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, takwimu za kilimo zinazozalishwa kwa wakati na zenye ubora ni muhimu kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya maendeleo ya binadamu," alisema.

Alisema matumizi ya njia za kisasa za uzalishaji wa takwimu hayana budi kupewa kipaumbele hasa ikizingatiwa kuwa sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo barani Afrika.

Dk. Nchemba alisema sekta ya kilimo ni chanzo kikuu cha chakula kwa watu takribani bilioni 1.2 kwa nchi zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara na malighafi zinazotumika viwandani.

Alisema takwimu za Benki ya Dunia (WB) mwaka 2021 zinaonyesha kuwa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa kwa nchi za Afrika ni asilimia 15 na Afrika Kusini ndiyo yenye mchango mkubwa zaidi kwa asilimia 50.

Kwa Tanzania, alisema manufaa ya sekta ya kilimo ni pamoja na kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 26.1 kwa mwaka 2021, chanzo kikuu cha ajira kwa kuajiri zaidi ya asilimia 65 ya nguvu kazi na chanzo kikuu cha fedha za kigeni kwa kuingiza wastani wa asilimia 24.7 ya fedha zitokanazo na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi. "Tanzania imeendelea kuwa nchi ya pili barani Afrika kwa uuzaji wa bidhaa nje ya nchi kwa kuwa na wastani wa ng'ombe 33, 943,183 wakati Ethiopia ikiongoza kwa kuwa na ng'ombe milioni 60.39," alisema.

Dk. Nchemba alisema sekta ya kilimo imeshikilia mustakabali wa maisha ya wananchi na inatoa matumaini kwa Afrika kuondokana na umaskini kwa kuhakikisha usalama wa chakula na lishe pamoja na kuongeza fursa zaidi za ajira.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) wa kuratibu uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi na inaelewa kuwa suala la uzalishaji wa takwimu si jukumu la ofisi hiyo pekee bali ni jitihada za pamoja za wadau wakiwamo watafiti binafsi, taasisi za elimu ya juu, taasisi za kitafiti na taasisi zisizo za kiserikali.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema matumizi ya takwimu yameongezeka nchini katika nyanja mbalimbali kupanga mipango ya maendeleo.

Alisema NBS inatarajia kuanza kutoa machapisho mbalimbali ya matokeo ya sensa kwa kila ngazi, ikiwa ni pamoja na ngazi ya taifa hadi kitongoji kwa lengo la kujua takwimu za maeneo husika zitakazosaidia upangaji wa shughuli za maendeleo.



Mtaalamu wa masuala ya ujasiriamali, Sang'odi Lugesha, akitoa mafunzo ya jinsi ya kufanya biashara kwa waumini wa Kanisa la Waadvesta Wasabato wa Mbezi Luis jijini Dar es Salaam mapema wiki hii na kushauri kila mjasiriamali kuzingatia umuhimu wa nidhamu ya fedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja milioni 5 kuzawadiwa kampeni 'Mchongo ni kuchanja'

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa sikukuu Benki ya Stanbic Tanzania imetangaza kuzindua kampeni 'Mchongo ni Kuchanja na Stanbic Visa' kwa ajili ya kuwazawadia wateja wa benki hiyo. Taarifa iliyotolewa na benki hiyo jana ilisema kwa kutumia kadi ya Stanbic Visa kwenye mashine za kulipa za kielektroniki wateja wanaponunua bidhaa na huduma kwa kutumia kadi hiyo watazawadiwa.

Ilisema kampeni hiyo itaanza leo hadi Februari 2023 na itawawezesha wateja wanaotumia kadi hiyo kujishindia hadi Sh. 250,000 kila wiki mbili na kupata fursa ya kushinda hadi Sh. 5,000,000 kwenye droo ya mwisho. Mkuu wa Kitengo cha kadi na malipo wa benki hiyo, Mwanahamisi Jumanne, alisema; "Msimu wa sikukuu unakuwa na mambo mengi, ndio maana tukaona ni vyema kuwazawadia wateja wetu pesa taslimu za ziada. Unacho takiwa ni kufanya malipo kwa kutumia kadi yako ya Stanbic Visa, pale unapofanya manunuzi ya bidhaa au matumizi ya kila siku."

Alisema uzinduzi wa kampeni hiyo unalenga kuwapa wateja wanaomiliki kadi ya Visa, faida zaidi wanaponunua mtandaoni au katika duka lolote wakati wa likizo.

Vile vile, alisema kampeni hiyo inalenga kuhimiza wateja kutumia mashine za kulipa za kielektroniki (POS) na biashara ya mtandaoni, ili kuondoa hitaji la kubeba pesa taslimu kwa miamala ya kila siku, na kuwawezesha wateja kufanya ununuzi salama na kupunguza usumbufu kwa wauzaji.

Kama benki benki bora Tanzania kwa mara tatu mfululizo, benki ya Stanbic imedhamiria kuendelea kuboresha huduma zake na kufanya ziendelee kukidhi mahitaji ya wateja wao hasa katika kuwahakikishia urahisi na usalama wakati wa malipo.

# Watekeleza agizo la mafunzo kwa wavuvi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BAADHI ya wavuvi wa Manispaa ya Bukoba na Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, wamepewa vifaa na kuongezewa ujuzi wa kuogelea ili kukabiliana na maafa katika maji, kujiokoa na kuokoa wengine.

Mafunzo hayo yaliyojumuisha pia wavuvi walioshiriki katika uokoaji kwenye ajali ya Ndege Shirika la Precision Air iliyotokea Novemba 6, mwaka huu, na kusababisha vifo 19 na majeruhi 24, yalitolewa juzi ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kujenga uwezo wa vikundi vya wavuvi hao.

Wakizungumza baada ya kufanya mafunzo kwa vitendo ndani ya Ziwa Victoria wavuvi hao walisema mazoezi hayo yatawasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali katika ziwa hilo ikiwa pamoja na shughuli za uokoaji katika maeneo ya kazi zao.

"Awali tulikuwa tunaogelea kwa kutumia mavazi yetu ya kawaida hali iliyokuwa ikisababisha kutumia muda kidogo majini na kuchoka kwa haraka lakini kupitia vifaa hivi tutakuwa na uwezo wa kumudu changamoto za majini kwa muda mrefu," alisema Beatus Mweyaga, mvuvi na mkazi wa Nyamkazi.

Naye Justine Goston, mkazi wa Nyamkazi, alisema mafunzo hayo yamekuwa sehemu ya kuowaongezea umakini na usalama pindi wanapokuwa kwenye shughuli zao na hasa nyakati za uokoaji.

Harid Musaa kutoka Wilaya ya Missenyi, alisema asilimia kubwa watu hutumia usafiri wa mitumbwi kwenda kwenye visiwa kutafuta riziki zao hivyo kupitia vifaa hivyo walivyopewa vitawasaidia na kuwapa wepesi wa kukimbia huko na kusaidia wengine ambao wamepata na ajali tofauti na hapo awali.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Toba Nguvilla, alisema eneo kubwa la Ziwa Victoria, takribani asilimia 40 liko upande wa mkoa wa Kagera kwa kuwa na visiwa 32 na kata tano zenye watu 1,050 ambao maisha yao hutegemea safari za majini, hivyo kuwataka wavuvi hao kuwa mabalozi kwa wengine ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kukabiliana na majanga mbalimbali majini.

Mkurugenzi Msaidizi wa Maafa, Luteni Kanali Celestine Masalamado, alisema ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Maafa imeona umuhimu wa vikundi vya wavuvi kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye maokozi pindi majanga yanapotokea.

Aidha, alisema vifaa vilivyotolewa ni vile vitakavyosaidia katika uokozi, mavazi rasmi ya kujiokoa (life jacket), maboya ya kuvaa, kamba na mitungi ya gesi.



# Tanzania yaishawishi UNESCO maeneo yake kuingizwa orodha urithi wa dunia

**Novatus Makunga,** ARUSHA

TANZANIA imepanga kulishawishi Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kuingizwa kwa maeneo yake saba yaliyoko kwenye orodha kwa muda mrefu ya kutambuliwa kimataifa kama maeneo ya urithi wa dunia.

Mkuu wa Kitengo cha Sayansi na Asilia wa UNESCO katika Ofisi ya Dar es Salaam, Kelvin Robert, jana aliiambia Nipashe kuwa wanafikiria kusukuma kuingizwa kwa maeneo ambayo mpaka sasa yako katika orodha ya kutambuliwa na shirika hilo.

UNESCO inatarajiwa kufanya maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa mkataba wa kulinda maeneo ya urithi wa dunia yatakayofanyika jijini Arusha kuanzia Desemba 12, mwaka huu.

Maeneo yanayopiganiwa kuingiza ni Mlima Oldonyo Morwak ulioko Wilaya ya Siha, unaotumika kwa shughuli za mila za jamii ya wafugaji wa Kimasai wa Kenya na Tanzania.

Zimo pia Hifadhi ya Taifa ya Gombe iliyoko mkoani Kigoma na Hifadhi ya Taifa ya Ghuba ya Jozan - Chwaka, Zanzibar. Pia kuna Milima ya Tao la Hifadhi ya Mashariki na Njia ya Kati ya Safari ya Watumwa na Biashara ya Pembe za Ndovu kutoka Bara kwenda Pwani.

Maeneo ya utamaduni ni pamoja na Mji Mkongwe Zanzibar, Magofu ya Kilwa Kisiwani, Songo Mnara na michoro ya mapango ya Kondoa.

Aidha, maeneo ya asili ni Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA), Pori la Akiba la Selous na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Kwa mujibu wa Robert, kufanyika kwa maadhimisho hayo, kutasaidia kuwajengea uwezo wataalamu wa nchi za Afrika katika kuandaa na kuwasilisha maeneo ambayo yana vigezo vya kuingizwa katika orodha ya uridhi wa dunia.

"Afrika pamoja na kuwa na maeneo mengi yenye sifa, lakini kwa upande wa dunia ina asilimia 8.5 pekee kati ya asilimia 100 ya maeneo yote ya urithi wa utamaduni na asili yaliyoingizwa katika orodha ya UNESCO,"alisema.

Alisema Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo kutokana na kukithiri vigezo vya kulinda maeneo ya urithi wa dunia, ambayo yamegawanyika katika sehemu ambazo maeneo ya utamaduni na maeneo ya asili.

Tanzania mpaka sasa ina maeneo saba ambayo yamo katika orodha ya urithi wa dunia ambapo kati ya hayo matatu ni katika kundi la maeneo ya utamaduni na mengine manne katika kundi la maeneo ya asili.

Mkuu wa Idara ya Urithi wa Utamaduni wa NCAA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi (SACC), Joshua Mwankunda, alisema Tanzania imekuwa ikinufaika na mkataba wa urithi wa dunia katika maeneo ya asili na kiutamaduni.

## RC aonya kuhusu ujenzi madarasa

**Na Mary Mosha,** SAME

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema hakuna mtu atabaki salama kama kuna shule ya sekondari iliyopewa pesa za ujenzi wa vyumba vya madarasa, mradi wake utaishia njiani bila kukamilika ifikapo Desemba 5, mwaka huu.

Babu alitangaza msimamo wake jana, alipokwenda Wilaya ya Same, kukagua miradi hiyo katika Kata za Mabilioni, Makanya na Hedaru.

Wilaya ya Same inatekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 32, vilivyoigharimu serikali zaidi ya Sh. milioni 640.

"Katika Mkoa wa Kilimanjaro, ninao uongoza mimi, niwatoe hofu wazazi na walezi kwamba hakuna mtoto atakosa kuingia darasani mwezi Januari mwaka 2023.

"Tuna jumla ya wanafunzi 41,293 waliomaliza darasa la saba mwaka huu. Tunachotaka ni kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa madarasa 125 yanayojengwa kwa gharama ya bilioni 2.5," alisema.

Hadi kufikia sasa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika mkoa huo vimekamilika kwa zaidi ya asilimia 75.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Same, Edwad Mpogolo, alisema walipokea Sh. milioni 640 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 32.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Flora Kessy (kulia), akijadiliana jambo na watumishi wa Idara ya Afya na Maendeleo ya Jamii katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, yaliyofanyika kiwilaya, katika kata ya Mbaramo, wilayani humo jana. Wengine ni Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Neema Mhina (wa pili kulia), Mratibu wa UKIMWI wa wilaya, Dk. Yahaya Mbura (wa pili kushoto) na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya, Anethira Issa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wakulima kiduchu wasajiliwa mbolea ruzuku


**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara, umesajili hadi kufikia sasa asilimia 11.8 pekee ya wakulima wenye uhitaji wa mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali. Idadi hiyo ni sawa na wakulima 60,000 waliosajiliwa.

Akizungumzia hali ilivyo, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa huo anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji, Faraja Ngevageza, alisema jana kuwa wakulima hao ni kati ya 500,000 waliolengwa. "Nia ya serikali ni kuwawezesha wakulima wetu kwa tija na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. "Wakulima hao ni asilimia 11.8 ya waliosajiliwa na katika Mkoa wa Manyara ni wakulima 500,000," alisema. Kwa mujibu wa Ngevageza, iwapo wakulima wataendelea kushindwa kujisajili, watasababisha serikali ishindwe kupeleka mbolea hiyo, wakati serikali imeishatumia Sh. bilioni 160 kununua mbolea ya ruzuku.

Alivitaja vikwazo wanavyokabiliana navyo kwenye kusajili wakulima kuwa ni imani potofu ya wakulima, kuwa huwa wanavuna hata wasipotumia mbolea.

Wakati huo huo, Ngevageza, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mkoa ulipata ziada ya tani 264,819 japo matarajio yalikuwa tani milioni 1,142,819.





## GGML yajivunia kampeni ya kudhibiti VVU/UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu**

KILELE cha Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kilikuwa jana. Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imesema itaendeleza mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi kutokana na msaada inaoupokea kutoka kwa wadau na kuiwezesha Kampeni ya Kili Challenge kupiga hatua kubwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002 hadi kufikia kuwa mfuko wa kimataifa.

Kampeni hiyo iliyozinduliwa na GGML miaka 20 iliyopita ikilenga kuongeza uelewa na fedha za kupambana na maambukizi ya VVU, imekuwa mfuko wa kimataifa wenye kushirikisha wapanda Mlima Kilimanjaro na waendesha baiskeli kutoka mabara yote na zaidi ya nchi 20.

Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti anayesimamia miradi endelevu Ghana na Tanzania, Simon Shayo alibainisha hayo jana alipozungumzia mafanikio yaliyofikiwa kuelekea kilele cha maadhimisho hayo ya Siku ya Ukimwi Duniani.

"Tunafurahia mafanikio haya kwa kutuwezesha kuufanya mfuko huu kuwa endelevu katika kutimiza malengo ya serikali dhidi ya janga hili," alisema.

Makamu wa Rais alisema mwaka huu GGML kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kupitia kampeni hiyo ya Kili Challenge imefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.1, fedha zinazotumika katika kutunisha mfuko wa mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi.

Alisema fedha ambazo zimepatikana hadi sasa zimewezesha taasisi na makundi mbalimbali nchini kuboresha shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Alisema kampeni ya GGM Kili Challenge 2022 iliyoanza Juni 29 na kumalizika Julai 21 mwaka huu, inaunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania kufikia malengo ya sifuri tatu.

Sifuri ya kwanza inalenga katika kupunguza asilimia ya maambukizi mapya, sifuri ya pili katika kupunguza unyanyapaa na sifuri ya mwisho ni kupunguza idadi ya vifo vinavyosababishwa na Ukimwi.

"Mathalani katika kampeni ya mwaka huu jumla ya washiriki 52 ambao 24 kati yao walipanda Mlima Kilimanjaro kwa miguu na 28 waliendesha baiskeli kuzunguka mlima huo kuanzia lango la Machame na kumalizia kwenye lango la Mweka," alisema.

Makama wa Rais alisema kwamba kampeni ya mwaka huu ilikuwa ya mafanikio makubwa ikiambatana na upimaji wa bure wa VVU na kisukari pamoja na chanjo ya UVIKO-19 kwa wakazi wa mjini Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

"Nina furaha kubwa kuwataarifu kuwa katika huduma hizo zilizofanyika Julai 15 hadi 18 mwaka huu, jumla ya watu 463 walipimwa VVU na hakuna hata mmoja aliyekutwa na maambukizi. Hii ni hatua kubwa katika mwitikio wa Watanzania wanaotaka kujua hali zao za kiafya," alisema Shayo.

Aliongeza kuwa katika utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, wataalamu hao walifanikiwa kuwachanja watu 822, wakiwamo wanaume 365 na wanawake 427.

Uchangiaji damu ulikusanya jumla ya uniti 27 za damu, huku mipira ya kiume 9,335 na za kike 200 ikitolewa kwa wananchi waliohudhuria tukio hilo.

"Ili kutoa elimu ya kutosha kwa umma kuhusu VVU, vidonge vya PrEP pia vilisambazwa ili kupunguza makali ya kwa wanaoishi na VVU na kuzuia maambukizi kwa wale waliopima na kukutwa hawana ugonjwa huo, pamoja na vipeperushi 204 kuhusu masuala ya afya ya uzazi," alisema Shayo.

Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko alisema jumla ya Sh. bilioni 1.1 zilipatikana wakati wa kampeni hiyo huku akitoa wito kwa wadau wengine kukaa mezani na TACAIDS ili kwa pamoja kutafuta njia mpya za kutafuta fedha zaidi za kukuza mfuko wa VVU nchini.




Baadhi ya washiriki wa kampeni ya GGM Kili Challenge 2022, waliopanda Mlima Kilimanjaro hivi karibuni, kwa lengo la kukusanya fedha za mapambano dhidi ya VVU. Mwaka huu jumla ya Sh. bilioni 1.1 ilikusanywa na GGML kupitia wadau mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wafugaji wafundwa kuchangamkia soko la ngozi kunufaika kiuchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, amewafunda wafugaji mkoani Manyara, kuchangamkia fursa ya uwepo wa soko la ngozi ambalo lipo ndani na nje ya nchi, badala ya kubaki kwenye nyama na maziwa pekee.

Alikuwa alizungumza jana wilayani hapa wakati wa mkutano mkuu wa 15 wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Mkoa wa Manyara (MVIWAMA).

Twange alisema wafugaji wa ng'ombe wasibaki kwenye nyama na maziwa pekee ila wageukie fursa ya soko la ngozi kwani ni kubwa mno.

"Ndani ya nchi na nje ya nchi kuna soko la ngozi hivyo tugeukie ngozi zina faida tusibaki kwenye maziwa na nyama pekee," alisema Twange. Mratibu wa MVIWAMA, Valentin Ngorisa, alisema wanahudumia vikundi vya wakulima na wafugaji 382 vyenye wanachama 8,497. Ngorisa alisema MVIWAMA walianza shughuli zao wilayani Babati mwaka 2006 kama MVIWATA, ila sasa wapo mkoa mzima wa Manyara.

Alisema kwa sasa MVIWAMA inatekeleza mradi wa DGD-HUSISHA kwa muda wa miaka mitano chini ya ufadhili wa Shirika la TRIAS Tanzania katika wilaya za Hanang', Babati na Kiteto.

"Pia MVIWAMA inatekeleza mradi wa FFF wa radi wa uboreshaji wa ustawi wa wazalishaji wadogo wa mazao ya misitu na kilimo kupitia hifadhi ya mazingira chini ya ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani FAO," alisema Ngorisa.

Mwenyekiti wa MVIWAMA, Paulo Joseph, alisema wanakabiliwa na changamoto za ukosefu wa masoko ya nafaka ya mahindi na mbaazi na matumizi ya vipimo visivyofuata sheria.

"Pia tuna changamoto ya pembejeo duni na bandia za mbegu, mbolea, viuatilifu na zana za kilimo," alisema Joseph.

## Uharibifu mazingira wawaamsha wadau

**Na Mwandishi Wetu,**
HAI

KUKITHIRI kwa shughuli za binadamu na ongezeko la ujenzi wa makazi pembezoni mwa chanzo cha maji cha Magadini, wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kumewaamsha usingizini wadau wa mazingira kuanza kupiga kelele ili mamlaka husika zichukue hatua za kukinusuru kukauka.

Chanzo hicho cha maji ambacho kilikuwa kikitumika pia kama bwawa la ufugaji wa samaki, kiko katika Kata ya Bondeni.

Akizungumzia tishio hilo jana, wakati wa upandaji miti katika chanzo cha maji cha Salehe kilichoko Rundugai, Aziz Simbano, alisema eneo hilo walikuwa wanafuga samaki na kujipatia kipato, lakini sasa chanzo hicho kinatia huruma kwa kuwa kimeanza kukauka.

"Tunaomba sana mamlaka zinazohusika, hasa Bonde la Pangani na Halmashauri ya Wilaya ya Hai, kutafuta mwarobaini wa kukinusuru chanzo hiki kisife na kuathiri uchumi wa wananchi wa bondeni na wilaya yetu kwa ujumla.

"Ni ajabu chanzo hicho kimevamiwa na watu wanajenga nyumba na wengine kulima na hivyo kufanya chanzo kuanza kukauka na kuwa katika hatari ya kupotea kabisa," alisema.

Simbano, ambaye ni Diwani wa Rundugai, aliwasihi viongozi na wanaharakati wa masuala ya mazingira, kufanya tathmini ya kujua idadi ya vyanzo vya maji ambayo vimevamiwa na kuwa katika hatari ya kutoweka.

Katibu wa Kikundi cha Kutunza Mazingira Rungugai (TUMAYA), Haji Msuya, akizungumzia suala la mazingira, alisema kikundi hicho licha ya kujitahidi kutunza na kusimamia mazingira, kinakabiliwa na tatizo la uhaba wa vitalu vya miti, kitu ambacho kinarudisha nyuma jitihada zao.

Kwa mujibu wa Msuya, kikundi hicho kinasimamia vyanzo 36 vya maji vilivyoko ukanda wa tambarare.




Ukurasa 17

Kamanda bodaboda mtawezana kweli?

BUFE

IJUMAA DESEMBA 2, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




**SARAH PIMA**
**Mwanamazingira aliyeibukia mkutanoni Misri na bidhaa za malighafi taka, zilizo kamata soko**

Ukurasa 16

# Mkasa wa Wanigeria watatu kujificha kwenye rada uvunguni mwa meli siku 11

**Na Mwandishi Wetu**

"Hawa ni Wanigeria watatu walio katika umri halali. Watatu hao wameomba hifadhi na mmoja bado amelazwa hospitalini," inaelezwa kutoka Hispania.

Kwa njia hiyo, hatimaye serikali ya Uhispania ilitoa ruhusa kwa meli kuondoka bandarini, ikiwaacha wahamiaji watatu kwenye kisiwa cha Gran Canaria.

Pia ilithibitishwa shirika lisilo la kiserikali la Caminando Fronteras, liliitaka mamlaka kusimamisha kurejeshwa kwa wahamiaji hao watatu wa Nigeria.

"Ukweli wa kupitia safari ya hatari kama hiyo inapaswa kuzingatiwa kama dalili ya kuchambua kibinafsi hali ya kibinafsi ya waathiriwa watatu," ilitamka asasi hiyo katika taarifa yake, ikionya kwamba wahamiaji wawili walikuwa wamehamishwa kurudi kwenye meli siku ya Jumanne.

Vile vile, walikuwa wameomba kukaribishwa katika mojawapo ya vituo vya wahamiaji "ili wapate usaidizi unaohitajika wa kutulia kiakili na kisaikolojia kwa kuzingatia hali ya matukio na safari ya hatari ambayo inaweza kuwa mbaya."

**ILKUWAJE?**

Jinsi walivyofikia rada ya usukani haijulikani. Kinachojulikana ni kwamba Wanigeria hao watatu walizamia meli hiyo katika bandari ya Lagos, Nigeria, kabla ya Alithini II yenye bendera ya Malta. kuanza safari mnamo Novemba 17.



Sehemu ya chini walikojificha wazamiaji hao. PICHA: MTANDAO.

Safari ya kuelekea kisiwa cha Gran Canaria ilidumu kwa siku 11 mfululizo. Mnamo Jumatatu, Novemba 28, Salvamento Marítimo aliwaokoa baada ya kufaulu kufika Las Palmas, baada ya kuonekana katika sehemu ya chini ya meli.

Mahali walipopatikana ni nafasi iliyoko kwenye kile kiitwacho rada au usukani wa nje ya sehemu ya meli, ambayo huwa wazi na inaweza kushambuliwa na pigo lolote kutoka baharini.

Picha iliyosambaa kwa kasi duniani ilipigwa na mlinzi wa chombo cha uokozi ya Salvamar Nunki, Orlando Ramos Alayón, ambaye aliwaokoa.

"Ni kawaida. Huwa tunachukua picha hizo ili kuzihifadhi kama kumbukumbu," Orlando Ramos anaeleza katika taarifa iliyotolewa siku ya Jumatano.

"Ni muhimu kuokoa maisha ya watatu hao, na wengine ambao hufika uhamishoni bila nguvu, wakiwa wadhaifu, na kuathiriwana baridi kali."

"Kulikuwa na wanaume watatu kutoka Kusini mwa jangwa la Sahara waliokuwa wadhaifu baada ya kuathiriwa na baridi kali. Watu wawili kati ya waliokolewa walipelekwa katika Hospitali ... na yule aliyekuwa katika hali mbaya zaidi alisafirishwa hadi Hospitali ya Insular," inasema taarifa kutoka meli hiyo.

Wawili kati yao waliachiliwa muda mfupi baadaye na kurudishwa kwenye meli ya mwanzoni, lakini baadaye walitolewa tena kwenye meli hiyo baada ya kuomba hifadhi.

Mwathiriwa wa tatu bado amelazwa hospitalini, ambako anaendelea kupata matibabu kutokana na upungufu wa maji mwilini, maisha yake hayako tena hatarini, kulingana na mamlaka.

"Ni sehemu ambayo mtu hawezi kukaa, ukizingatia hali ya mazingira ya bahari kuu mtu anaweza kufa kutokana na upungufu wa maji mwilini, kuanguka ndani ya maji kutokana na dhoruba ya bahari.

"Upepo ni mkali unaosababisha hypothermia ... ni hatari kubwa. Eneo hilo linaweza kujaa maji. Kuna uwezekano mkubwa wa hili kutokea, "inaeleza taarifa.

Hasui sasa inaeleza, mamlaka inayosimamia uokoaji imerekodi mikasa mitano kama hiyo katika miaka ya hivi karibuni.

Mnamo Januari 2018, Salvamar Nunki iliokoa watu wanne kwenye meli ya Green Sky waliokuwa wamejificha kwenye rada.

Mnamo Oktoba 2020, wazamiaji wanne walipatikana kwenye gurudumu la meli ya mafuta ya Norway ya Champion Pula, baada ya kusafiri kutoka Lagos hadi Las Palmas.

Mwezi huo huo, Salvamar Nunki iliokoa 7 kwenye rada ya meli ya Andromeda.

Mwezi mmoja baada ya operesheni hiyo, mnamo Novemba, mashua hiyo hiyo iliokoa mtu aliyekuwa amejificha kwenye rada.

Hadi kufika Juni mwaka huu, shirika lisilokuwa la kiserikali la Caminando Fronteras lilisajili vifo 800 kwa namna hiyo na mwaka jana Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM) lilirekodi vifo 1,532 katika njia hiyo.

**Kwa mujibu wa taarifa kimataifa.**

UCHUMI

## YANUIA ‘KUTEKA’ 44% INAYOAGIZWA NJE ...

# Singida inavyojibebesha tenda kumaliza shida mafuta, ikitanua mashamba alizeti

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

KUANZIA Januari mwaka jana, nchi ilikumbwa na tatizo kubwa la uhaba wa mafuta ya kula, hivyo bei kupaa na kusababisha wananchi kupaza sauti.

Changamoto hiyo ya uhaba wa mafuta ya kula ilitokana na upungufu wa uzalishaji na kutegemea uagizaji mafuta ya kula nje ya nchi. Bei ya mafuta ya kula hutegemea soko la bidhaa hiyo kulingana na msimu na mabadiliko ya bei katika soko la dunia.

Serikali ilichukua hatua kukabiliana na tatizo, kwa kuzipatia leseni kampuni mbili za uagizaji wa mafuta ya kula kwa mwaka.

Mahitaji ya mafuta ya kupikia nchini kwa mwaka ni wastani wa tani 600,000 hadi 700,000 wakati kiasi kinachozalishwa nchini kinatajwa kuwa tani 205,000 kwa mwaka.

Singida ni kati ya wazalishaji wakubwa wa mafuta ya kula, katika orodha ya mikoa 11 nchini inayozaliosha bidhaa hiyo, mafuta ya alizeti yaliyo juu zaidi kisoko. Sasa nao umeamua kushiriki kuziba pengo hilo la mafuta ya kula nchini, kwa kuongeza uzalishaji wake.

Mikoa mingine inayolima alizeti kwa wingi ni: Shinyanga, Dodoma, Iringa, Tabora, Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Manyara, na Rukwa inakolimwa kwa ajili ya chakula na biashara.

Miongoni mwa mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ya alizeti iliyowekwa na mkoa wa Singida, ni kuhakikisha uzalishaji wa mafuta hayo unafikia tani 159,110.5 sawa na asilimia 44.2 ya mafuta yanayoingizwa nchini.

Mkakati huo unalenga kuisaidia nchi kuondokana na tatizo la upungufu wa mafuta ya kula ambao utaanza kutekelezwa katika msimu uliopo sasa na mavuno yake kushuhudiwa mwakani.

**MKAKATI MKOA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mkakati ya Kuongeza Uzalishaji wa Alizeti Mkoa wa Singida, Justice Kijazi, anakieleza kikao chini ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipokuwa ziara mkoani hapa.

Kijazi anasema, ili kufikia uzalishaji huo wa mafuta mkoa umepanga kuongeza eneo la kulima alizeti ambazo zitalimwa ekari 631,391 kwa matarajio ekari hizo zitazalisha tani 492,485 za alizeti.

Anafafanua kuwa, ili kufikia uzalishaji huo, mkoa utahitaji tani 1,262.5 za mbegu bora za alizeti aina ya Certified 1.

Hadi sasa anasema, mkoa Singida una jumla ya viwanda 221 vya kusindika alizeti, vinavyohitaji tani 635,465 kwa mwaka. Lakini, kwa kipindi cha miaka mitano sasa, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi msimu uliopita, uzalishaji wa alizeti haujawahi kuvitosheleza viwanda hivyo.

Katika kipindi chote hicho uzalishaji wa juu ulikuwa ni tani 260,064 na msimu uliopita (2021/2022) hali haikuwa nzuri.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, anasema mkoa sasa umetengewa kilo 500,000 za mbegu bora za alizeti ya ruzuku zenye thamani ya Sh. bilioni mbili katika msimu uliopo wa kilimo, ambao sasa wakulima wanaandaa mashamba.

Anasema mbegu hizo aina ya Certified 1 zitauzwa kwa wakulima kwa bei ya Sh.5,000 kwa kilo, badala ya Sh.8,000 kwa kuwa zina ruzuku ya serikali.

Serukamba anasema serikali pia imetoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wote watakaojiandikisha kwenye mfumo maalum wa kupata ruzuku, ambao kwa sasa usajili unaendelea katika halmashauri zote saba za mkoa wa Singida.




Mkuu wa Mkoa, Peter Serukamba akiendesha trekta wakati wa uzinduzi wa msimu wa kilimo wa 2022/2023 uliofanyika wilayani Iramba.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Singida, Dk. Binilith Mahenge, ziarani katika shamba la wakulima wa alizeti, kata ya Mudida, Halmashauri ya Singida Vijijini mwaka jana. PICHA: MAKTABA.

**WAZIRI BASHE**

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anasema katika kuunga mkono kilimo hicho cha alizeti, serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao inatarajia kutenga Sh.bilioni 4.6 kwa ajili ya kununua zana za kilimo za kuunga mkono mkoa Singida, lengo ni kuinua kilimo mkoani hapo.

Anasema, baada ya kununuliwa zana hizo, halmashauri husika zitatakiwa zitenge maeneo maalumu ambako zana itawekwa na kutakuwepo mtu maalum wa kuzisimamia, ambako wakulima watakuwa wakienda kuzikodisha.

Kwa mujibu wa Waziri Bashe, fedha zitakazopatikana baada ya wakulima kukodi zana hizo, zitarudishwa serikalini na kwenda kununua zana kwa ajili ya mikoa mingine.

Kuhusu upatikanaji mbegu za alizeti, Bashe anasema mwelekeo wa serikali sasa ni kuweka nguvu kwenye utafiti na uzalishaji wa mbegu, upatikanaji pembejeo na huduma za ugani.

Anasema, ili kuondoa tatizo la mafuta nchini tunahitaji tuwe na tani 15,000 za mbegu bora ya alizeti, mwaka jana zilizalishwa tani 223 tu na msimu uliopo uzalishaji mbegu zaidi utafanyika kuchochea uzalishaji alizeti shambani.

**KUTOKA TARI**

Kwa mujibu wa Bashe, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imepanga kuanzisha shamba darasa la zao alizeti katika mkoa wa Singida, ambako mbolea za aina zote zitatumika kuleta ufanisi kwenye zao hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, ametangaza mpango huo wakati wa uzinduzi wa msimu wa kilimo mwaka 2022/2023 na ugawaji wa mbegu za alizeti zenye ruzuku zilizotolewa na serikali.

Anasema TARI itaanzisha shamba darasa hilo ili kupima afya ya udongo kwani zipo mbolea za aina mbalimbali ambazo zitatumika katika zao la kimkakati kama alizeti ili kuona zinaleta ufanisi gani kwenye zao hilo.

Dk. Mkamilo anasema TARI kwa kushirikiana na sekretarieti ya mkoa wa Singida na Wizara ya Kilimo, kutoa mafunzo kwa maofisa ugani na wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji wa zao la alizeti.

Kuhusu upatikanaji mbegu, anasema TARI itaendelea kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kuzalisha mbegu za kutosha hususani za zao la kimkakati la alizeti.

“Tayari tumeshakubaliana kiasi cha mbegu ya alizeti kinachohitajika ambacho TARI itazalisha kwa ajili ya kumpa ASA, ili waweze kuzalisha madaraja bora ambayo yatawafikia wakulima ili wakulima waweze kuongeza tija na uzalishaji wa alizeti,” anafafanua.

Dk.Mkamilo anasema suala la viuatilifu, TARI itahakikisha vinaangaliwa kisayansi namna gani vitaondoa wadudu.

UCHUMI

## TPSF IKITAMBA KUNG'ARA...

# Inashuhudiwa safari ya sekta binafsi ikikwea sokoni, viwandani na shamba

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), inatarajia kuadhimisha Siku ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSD22), wiki ya kwanza Desemba 2022, lengo ni kuwaleta pamoja wadau wote na kujadili kwa kina namna ya kuendelea kuimarisha injini hiyo muhimu ya uchumi.

TPSD22 imeandaliwa na TPSF kwa kushirikiana na wadau muhimu wa sekta binafsi na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kuenzi na kutambua mchango wa sekta binafsi katika uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, anasema zaidi ya wajumbe 1,000 ambao ni viongozi wa kisekta, wakurugenzi watendaji na maofisa waandamizi wa serikali watakusanyika kujadili dhima kuu ya 'Kuimarisha Ushindani wa Sekta Binafsi.'

"Lengo la tukio hili ni kutathmini mafanikio ya sekta binafsi kipindi cha 2021-2022, huku tukiangazia mazingira bora ya biashara na uwekezaji ambayo yamechochea ukuaji wa uchumi chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake ya awamu ya sita," anasema Ngalula.




Kikao kujadili dira ya biashara kikiendelea.

Aidha, anabainisha kuwa ongezeko la biashara na Kenya kwa asilimia 95, limechangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania na mwenyekiti huyo anasema, mafanikio mengine muhimu ya sekta binafsi ni pamoja na ukuaji shughuli za uwekezaji, kupanuka wigo wa ajira, kodi, na bidhaa za Tanzania kufikia masoko mapya.

"Maadhimisho haya yatatumika kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo. Tunatakiwa kuueleza ulimwengu fursa za uwekezaji zinazopatikana Tanzania," anasisitiza Ngalula.

Aidha, anasema kilimo ni sekta yenye kuleta faida kubwa kwa watu wenye nia ya kuwekeza, akifafanua: "Hivi karibuni tumesaini mikataba muhimu ambayo imepelekea mazao kutoka Tanzania kuuzwa nchi za nje.

"Kwa mfano, China imeagiza zaidi ya tani 40,000 za maparachichi kutoka Tanzania. Tumeshuhudia makubaliano kama haya yakifanyika baina yetu na Afrika Kusini na India.".

Kupitia Sera ya Diplomasia ya Uchumi, Ngalula anasema fursa za uwekezaji kwenye sekta ya madini zinatangazwa nje ya nchi na matokeo yake sasa yanaonekana.

Anasema mwaka 2021, serikali ilisaini mikataba minne na kampuni ya uchimbaji madini yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 735; na kwamba mikataba hiyo ina thamani kubwa zaidi nchini Tanzania.

Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, kiwango cha ukuaji uchumi baada ya janga la UVIKO-19 kinatakiwa kuwa endelevu ikikua na akisema hivi sasa nchini, uchumi unakua kwa kasi asilimia 5.1.

"Sekta binafsi imekuwa sehemu ya kutoa suluhisho kwa changamoto za uchumi kupitia biashara ndogo na za kati ambazo ni chanzo cha kipato kwa familia na uchumi wa taifa," anasema na kuongeza:

"Familia nyingi Tanzania zinategemea biashara ndogo na za kati; kwa mujibu wa Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA), takribani asilimia 35 ya pato la taifa linatokana na kundi hili. Maongezi yetu (yanayoanza sasa yatajikita katika nafasi ya sekta binafsi kwenye kuisaidia nchi kufikia dira yake ya maendeleo."



Hatua ikipigwa kwenye uzalishaji shambani. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Pia, ni uzinduzi utakaoendana na makongamano ya kikanda ya wauzaji na wanunuzi yaani kitaalamu'Zonal Buyer-Seller Forums', lengo ni kukuza biashara na uwekezaji kuanzia kwenye ngazi za mikoa na wilaya.

"Lengo letu ni kuongeza mauzo baina ya biashara katika kanda zote nchini Tanzania. Kwa kushirikiana na kampuni ya kimataifa ya ushauri, Epvate & Fortune International Consulting (EFIC), TPSF pia itatoa tuzo na kutambua makampuni na mashirika binafsi (PSOs) ambayo yameonyesha utendaji wa kipekee ndani ya mwaka mzima," anasema na kuongeza:

"Tutatoa zawadi kwenye vipengele vya vyama vya biashara vyenye michango maalum kwenye sekta, kampuni yenye shughuli bora zaidi za kusaidia jamii (CSR), kampuni inayochipukia (Startup) yenye ubunifu zaidi, kampuni bora katika utunzaji endelevu wa mazingira na taasisi za serikali zinazowezesha biashara," anasema Ngalula.

**WANAYOJIVUNIA**

Tangu aingie madarakani, Rais Samia amesisitiza umuhimu wa uwepo wa uhusiano wa karibu kati ya serikali na sekta binafsi na kwamba ni muhimu kusherehekea mafanikio makubwa ambayo tasnia ya sekta binafsi imeyaona yakiwemo mambo kadhaa.

Limo, uchumi unavyokuwa kutoka kwenye kishindo cha maradhi Uviko-19, ikimaanisha kwamba ukuaji uchumi nchini unakuwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita licha ya kuwepo janga la uviko 19.

Jingine, ni kufufua sekta ya utalii nchini; Mwenyekiti akisema Filamu ya 'The Royal Tour' inatoa majibu kwa kuongeza watalii , kwani tangu Januari hadi Julai 2022, jumla ya watalii 742,133 walitembelea nchini ikiwa ni ongezeko la watalii 285,867, sawa na 62.7 kwa kulinganisha na mwaka uliopita.

**MAPYA KILIMO, BIASHARA**

Pia, inatajwa suala la kukuza sekta ya kilimo kupitia mikopo nafuu. Hapo Ngalula anasema, baada ya maelekezo ya Rais Samia ya kushusha riba kwenye sekta ya kilimo, kumetoa majibu kadhaa ya kiuchumi.

"Tumeshuhudia benki zetu kushusha riba, kwa mfano CRDB ilishusha kutoka asilimia 20 hadi asilimia tisa, NMB asilimia 10 hadi tisa, TADB asilimia 11 hadi tisa, hali iliyowezesha wadau wa kilimo kupata mikopo kwa unafuu na kukuza sekta ya kilimo sambamba na ajenda 10/30,"anasema.

Jingine ni kuridhia Mkataba wa Kujiunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), akiufafanua kuwa Tanzania imechaguliwa kuwa kati ya nchi nane kuanza kuuza bidhaa zake katika eneo hilo, huku wakinufaika na punguzo za kodi.

Kingine ni kufungua masoko ya kimataifa, Rais amefanya kazi kubwa sana kufungua masoko ya kimataifa.

"Wafanyabiashara wa Tanzania sasa wanasafirisha parachichi kwenda, Afrika Kusini, India na hivi karibuni China. Mpaka 2023 tutaweza kusafirisha tani 15,000 zenye thamani ya Sh.103.5, ukilinganisha na tani 8,000 mwaka 2018.

"Pia tumeona soko kubwa la mbuzi kwenda Oman, Kuwait, Falme za kiarabu ambapo wafanyabishara mwaka 2022, wameweza kuuza zaidi ya Sh.bilioni 8 sawa na ongezeko la asilimia 25," anasema.

Jingine linalojumuishwa ni kudhiti bei za mafuta kupanda kwa kutoa ruzuku, hali iliyosaidia kupunguza makali ya maisha.

BIASHARA

SARAH PIMA

# Mwanamazingira aliyeibukia mkutanoni Misri na bidhaa za malighafi taka, zilizo kamata soko

**Na Jenifer Gilla , aliyekuwa MISRI**

"UKIONA cha nini, wenzio wanasema watakipata lini', ni usemi uliobeba maana kwa ushuhuda ambao Nipashe imejifunza kupitia kwa Mkurugenzi wa Shirika la Utu na Mazingira (HUDEFO) Sarah Pima, lilipokutana naye jijini Sharm el-Sheikh, Misri, wastani wa wiki mbili zilizopita.

Ilikuwa faragha ya ughaibuni, kwenye Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP27) uliofanyika kati ya Novemba 6 hadi 20, mwaka huu.

Wakati wadau wengine wa Mazingira wakihudhuria mkutano kujadili na kufuatilia namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Sarah akawa na lingine la ziada, kujiongezea kipato kwa kuuza bidhaa ambazo ni zao la mikakati ya utunzaji mazingira zikiwamo kofia, begi ya kubebea kompyuta mpakato na madaftari.

Akiwa amezungukwa na wateja kutoka mataifa mbalimbali, Sarah anaiambia Nipashe kuwa ametengeneza bidhaa hizo kwa kutumia mabaki ya vitambaa vya vitenge na batiki, ambavyo anavikusanya kwa mafundi wanaoshona nguo, ili kupunguza utupaji holela wa bidhaa hizo, ambazo huishia kuchafua mazingira .

Anaifafanulia Nipashe: "Ninaifanya hii biashara kwa mwaka wa tatu sasa, lakini hii ni mara yangu ya kwanza kuileta katika mkutano huu. Nashukuru Mungu mwitikio umekuwa mkubwa, nina siku ya tatu, lakini mzigo wa bidhaa 50 wote umeisha leo nimekusanya jumla Sh. milioni mbili, mwakani nitakuja na mzigo mkubwa zaidi."



Mkurugenzi wa Shirika la Utu na Mazingira (HUDEFO), Sarah Pima, akionyesha bidhaa zake katika Mkutano wa COP 27 nchini Misri. **PICHA: JENIFER GILLA.**

**NINI KILIMSHAWISHI?**

Sarah anataja kilichomsukuma kuingia katika biashara hiyo, ni kuwapo vitambaa vingi vinavyozagaa sehemu mbalimbali za mijini na hasa pembezoni mwa fukwe, zikichafua mandhari ya maeneo hayo, ambayo hutumika kwa shughuli za kiuchumi ikiwamo utalii.

"HUDEFO kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira, huwa tunafanya kampeni na kusafisha fukwe kila mwezi na moja ya taka tunazoziona kwa wingi, ni vitambaa vinavyotupwa na mafundi nguo, kwa kweli nilikuwa najisikia vibaya, lakini akili nyingine ikaniambia 'unaweza kufanya kitu' kitakachokuingizia pesa kupitia hivi vitu," anasema.

Kutokana na hali hiyo, mbunifu huyo anasema akaona kuna tatizo kwenye bidhaa za nguo zinazohitaji kutafutiwa suluhisho la ubunifu wa kudumu ili kutunza mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, ndipo akapata wazo la kutengeneza bidhaa hizo.

"Nikiwa mbobezi na mtafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi, ninajua kwa kiasi gani nguo zinatumia nishati kubwa na maji. Kwa hiyo, kwa ujumla kukua kwa viwanda vya nguo kunachangia kwa kiasi kikubwa athari za mabadiliko ya tabianchi, ndio nikaamua nije na hii suluhisho" anasimulia.

Pia, Sarah anataja kingine kilichomshawishi kufanya biashara hiyo, ni hitaji la pesa za kuendesha taasisi yake, hivyo akautumia ubunifu huo umpatie pesa za kuendesha taasisi hiyo, ikiwamo nauli kwenda mikoani kuhamasisha utunzaji mazingira na kupeleka vifaa kwa wahitaji.

"Faida yote tunayoipata hapa, inatumika kwenye shughuli za taasisi, ikiwamo kusafirisha mizigo ya kuwapelekea wahitaji mikoani. Kwa sasa faida si kubwa, kwa sababu gharama za kutengeneza bidhaa ni kubwa ukizingatia kuwa tunatumia mashine. Lakini, tunajivunia tunashiriki katika kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," anasema.

**ALIKOPATA UJUZI**

Sarah anasema, wakati anapata wazo la kuanzisha biashara hiyo, hakuwa na ujuzi wa kushona, hivyo akajifunza taratibu kupitia mtandao wa 'youtube' kuhusu namna ya kukata vitambaa, kuvipanga hadi kushona begi, mchakato uliomchukua takribani miezi mitatu kupata uelewa kamili.

"Baada ya hapo, nikaanza kutafuta wadau wa kuendeleza mafunzo, nikafanikiwa kupata mafunzo ya 'fasheni himilivu' kutoka Ujerumani. Nikapata nyingine kutoka Canada na nyingine Afrika Kusini.

"Pia, ninatamani kupata mafunzo zaidi na mategemeo yangu ni kuwa na kampuni ya kutengeneza nguo itakayotambulika kitaifa na kimataifa" anasema.

**ANAKOPATA MALIGHAFI**

Sarah anasimulia kwamba, baada ya kufanya uchunguzi na kugundua kuwa vitambaa hivyo vinatoka kwa mafundi wanaoshona nguo, akaanza kuwatembelea na kuwaomba wamuuzie vitambaa hivyo, badala ya kuvitupa. Hapo akajiwekea utaratibu kila baada ya siku 10, anaenda kununua vitambaa hivyo.

"Nashukuru mwitikio umekuwa mkubwa, ninapata malighafi za kutosha kutoka kwa mafundi kwa kweli sina shida, na hii imesaidia sana kutunza mazingira. Sasa hivi ile Mitaa ya fukwe za Rainbow ( Mbezi Beach, Dar es Salaam), huwezi kukuta vitambaa vimezagaa kwa sababu mafundi wa maeneo ya kule vitambaa vyao wananipa mimi," anasema.

Aidha, anasema malighafi nyingine wanazipata kupitia nguo zinazotupwa na watu hasa zenye 'matirio' ya jeans, ambazo bado zipo kwenye hali nzuri, ambazo wanazichana vizuri na kutengenezea mabegi ya kuwekea kompyuta mpakato, mashuka, mapazia na mapambo ya hotelini.

Sarah anasema, hivi sasa wameanzisha kampeni ya kukusanya nguo zisizovaliwa kila mwezi, kwa ajili ya kuwapatia wahitaji kutoka sehemu mbalimbali, ikiwa ni namna ya kudhibiti utupwaji wa nguo kiholela.

" Tangu mwezi Juni, mwaka huu tumekuwa tukikusanya nguo hapa Dar es Salaam na kuzipeleka vijijini kuwapa wahitaji. Tumeshakwenda Lindi, Bagamoyo, Bukoba, Ngara, Pwani na mwezi huu wa kumi na mbili tunategemea kwenda Mtwara na Dodoma kwa sababu nguo tunazokusanya ni nyingi sana," anasema.

Sarah anasema kukua kwa soko la mitindo, kumechangia kwa kiasi kikubwa kuzagaa vitambaa kwa jamii, hasa wanawake wanabadilisha nguo kila kukicha ili kwenda na mabadiliko ya mitindo ya mavazi, huku za zamani zikitupwa bila ya mpangilio maalum.

"Jamii hasa wanawake tumezoea kununua nguo bila sababu ya msingi, unakuta mtu anakwenda sokoni Mwenge (Dar es Salaam) hapo kwa lengo la kununua viatu au mafuta.

"Lakini, akakutana na mtu anafungua balo la magauni na yeye anasogea na kununua, wakati haikuwa katika mipangilio yake, bado huko nyumbani ana nguo zimejaa kwenye kabati hadi zinamwagika," anasema.

**MDHARA YALIYOKO**

Sarah anasema kuwa, madhara ya nguo kuzagaa mitaani ni kuchafua mandhari ya maeneo hivyo kupunguza hadhi yake hali inayosababisha hata baadhi ya shughuli za kiuchumi kuzorota ikiwamo utalii.

"Mazingira yakiwa machafu hata shughuli za kiuchumi zinadumaa, mfano pembezoni mwa fukwe, kunapokuwa na vitambaa vichafu hata watalii hawatopenda kutembelea, hapo kabla wazungu walikuwa wamepungua katika fukwe za rainbow na kusababisha shughuli za kiuchumi kusimama" anasema

**WAHUSIKA WAKIRI**

Mmoja ya wafanyabiashara wa urembo wa bahari katika fukwe ya Rainbow, Said Juma, anakiri shughuli za biashara kuzorota katika ufukwe huo kutokana na watalii kupungua hali iliyochangiwa na uchafu uliokuwa umekithiri katika eneo hilo.

"Tunawashukuru sana HUDEFO na wadau wengine wa mazingira kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kurudisha hali ya usafi katika eneo hili, watalii wote walihama. Ilikuwa inapita wiki sijauza hata kitu kimoja. Sasa biashara zimerudi kama kawaida, ilikuwa ukipata hapa unakuta kumejaa taka hasa za vitambaa" anasema .

Mtaalamu wa mabadiliko ya tabianchi kutoka Chuo kikuu Cha Dar es Salaam, Prof, Pius Yanda, anasema kuwa vinavyozagaa vinachochea athari za mabadiliko ya tabianchi hasa vile vinavyokwama kwenye mito na maziwa, vinachangia mafuriko, kwa sababu vinazuia maji kupita.

Shirika la Mazingira Duniani (UNEP), linaeleza mitindo ya nguo inashika nafasi ya tatu kwa uchafuzi wa mazingira baada ya chakula na ujenzi. Ikichangia asilimia 10 ya gesi chafu duniani, ikitoa tani bilioni 1.2 za hewa ya ukaa kwa mwaka.

Aidha, shirika hilo linatahadharisha kuwa, uzalishaji nguo ukiendelea kwa kasi hiyo, gesi chafu katika eneo hilo inakadariwa itaongezeka kwa zaidi ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

**CHANGAMOTO YAKE**

Sarah anasema, changamoto anayokumbana nayo katika biashara hiyo ni uhaba wa vifaa, ikiwamo mashine za kushona bidhaa na kusababisha kutengeneza bidhaa kidogo, tofauti na mahitaji ya soko, akiwaomba wadau wajitokeze kumsaidia.

"Kwa hiyo tunaomba wadau watusaidie mashine za kushonea maana tunayo moja haitoshelezi, lakini pia tuna uhitaji wa usafiri wa kubebea nguo tunazokusanya kwa ajili ya kupelekea mikoani hali inayochangia kukusanya kwa kiasi kidogo na kuwafikia watu wachache, kwa hiyo hata tukipata bajaji au toyo itaturahisishia sana utendaji wetu wa kazi," anasema.



Fundi cherehani akiwa kazini. Mabaki ya vitambaa anavyokata wakati wa kushona, ndio malighafi aina hiyo hutumiwa na fundi Sarah Pima. **PICHA: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Kamanda bodaboda mtawezana kweli?






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

HIVI karibuni, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillius Wambura, alifanya mabadiliko ya makamanda wa polisi wa mikoa, akimwondoa Ramadhan Ng'anzi. Mwanza na kumpa kusimamia Kikosi cha Usalama Barabarani nchini.

Ng'anzi akapokea kijiti cha Wilbroad Mutafungwa, akimwachia kusimamia usalama wa wananchi wa Mwanza, naye akapuyange mabarabarani kupambana na madereva walevi, jeuri, wasiotaka kusikia na wasiotaka kuona.

Siku zote ukihamia mahali fulani, lazima ukasome na kupajua vizuri na kisha uje na mipango yako ya jinsi ya kupaishi hapo na kupadhibiti kimazingira. Kamanda Ng'anzi hakulisahau hilo, akafanya kama atakiwavyo.

Tukamshuhudia siku moja akitoa agizo la siku saba kwa wanaokiuka sheria za usalama barabarani kujirekebisha na kuzitii bila shuruti. Kamanda akaagiza madereva bodaboda katika siku saba alizotoa wawe wamejirekebisha kitabia.

Kamanda akahanikiza kuwa wengi wa madereva hao ni vijana, ambao wamekuwa wakidhani wana ubia na sheria za usalama barabarani. Vijana wa bodaboda, hawavai kofia ngumu, hawajali taa za kuongozea vyombo vya moto barabarani na wala hawajui nini ni kivuko cha pundamilia.

Kamanda Ng'anzi kumbe alishawashitukia, ila sijui akiwa mkoani Mwanza alikuwa akiwaona wakifanya hayo, anayoyasema na kuyakemea! Inawezekana, lakini akajiweka katika mwamvuli wa ukamanda wa mkoa na kumwachia mkuu wa trafiki wa mkoa ademke nao.

Hakuishia hapo, akawagusa na madereva wa serikali ambao wamekuwa kila mara wakilalamikiwa kwa uendeshaji mbovu wa kutojali sheria hizo, wakijimwambafai kuwa ndio serikali na serikali iko mikononi mwao na sheria chini yao.

Akasema hatataka kuona madereva hao ambao ndio walipaswa kuwa mstari wa mbele kuonyesha utii bila shuruti, lakini wao ndio wasiginaji wakubwa wa sheria na kusababisha ajali wakisingizia kuwa na mabosi wao ambao ndio wenye serikali yao.

Kwa kweli sisi tupendao kutii sheria bila shuruti, tukapokea maagizo hayo kwa mikono miwili na kumwombea Kamanda Ng'anzi Mungu ampe wepesi katika hayo ili afanikiwe, tukakumbuka jinsi ajali nyingi zinavyohusisha madereva wa serikali.

Hakika, madereva wa serikali na wa bodaboda ni watoto wa baba na mama mmoja lakini matumbo tofauti. Wawili hawa hawajui kabisa kwamba kuna mahali udereva unatakiwa weledi na maadili. Palipo na kibao cha mwendokasi wa kilometa 50 kwa saa, wao hupita kilometa 100 kwa saa.

Palipo na njia za mabasi yaendayo haraka, wao ndimo kwao, wanataka wapite kwa kisingizio cha haraka, lakini kumbe wanataka kujionyesha tu kuwa vibana vyao vya namba ni tofauti na vyetu sisi pangu pakavu tia mchuzi, ambao ni shabaha ya trafiki barabarani.

Dereva wa kundi letu, akiwa nyuma ya gari la serikali tena kwenye njia ya mabasi hayo wa serikali ataachwa, lakini yeye atokaye nyuma atang'ang'aniwa, akibishana kuhoji mbona yule kaachwa hakukamatwa? Jibu ni rahisi tu: "Usinifundishe kazi!"

Sasa basi napenda kumwambia Kamanda Ng'anzi, kuwa zile siku saba alizotangaza zimepita na sasa zinakuja saba zingine na zingine, atazame kama bodaboda wana kofia ngumu. Akae kwenye mataa kama ataona bodaboda anasimama au hata akiweza kwenye vivuko vya pundamilia.

Ndiyo kwanza bodaboda wanapita wanakotaka na wanavyotaka, ndiyo kwanza wamefunga honi za malori kwenye pikipiki zao, madereva wa serikali nao ndiyo kwanza wanafanya wanayoyajua na kuyatii wao bila shuruti ni shida.

Bila kuficha, ni kwamba suala la usalama barabarani katika nchi hii ni nyimbo tu za funika kombe mwanaharamu apite, hata siku moja upatiwe ufumbuzi katika muktadha huu, ambao baadhi ya wanaotakiwa kusimamia sheria hizo wanamiliki vyombo vya moto vinavyoona poa kuvunja sheria.

Sijui, lakini Kamanda ana kibarua kikubwa cha kuweka mambo haya sawa, kwa sababu watu wameshazoea kukusanya humo barabarani, kwa kupewa na madereva hususan wa mabasi, pia madudu katika ugawaji stika za usalama barabarani.

Inanikumbusha wakati fulani kuna mkubwa mmoja jijini Dar es Salaam alipiga marufuku madereva wa bodaboda kufunga muziki mkubwa kwenye pikipiki zao, lakini baada ya hapo ndipo kwanza zikaingizwa nchini pikipiki zikiwa na muziki kabisa, unafanyaje hapo? Alamsiki!

UCHUMI

WALIKO BARBARA, DC JOKATE ...

# Jarida laangaza mzizi wa kibiashara na kitaasisi ulivyochangia safari zao

**Na Mwandishi Wetu**

KADRI muda unavyosonga kunashuhudiwa dhana 'wanawake hawawezi kuongoza' ikizidi kufa nguvu na kwenye nchi zinazoendelea ikiwamo barani Afrika, hii sasa inatamkwa kwa ukakasi ukakasi wa namna fulani.

Hali kadhalika, pale msamiati uongozi unapochukua nafasi, haimaanishi ngazi ya juu pekee kiserikali. La hasha! Inakuwa kila ngazi ya kiungozi, hadi vijiji na mitaa, kunakuwa na mageuzi kwa ngazi yake.

Pia, upo usemi 'Mcheza Kwao Hutuzwa' unaolenga kuwapa moyo na hamasa waliofanya vizuri, pamoja na kuwahamasisha wasichana wenye ndoto za kuwa mithili ya kinamama hao, waiongoze jamii, kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa.

Ndani yake, inabainika mafaniko hayo, kukishuhudiwa mizizi yake kwenye mifumo ya kitaasisi na kibiashara, ikiendana na michango mikubwa ndani yake.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo

Hapo ndipo taasisi ya kimataifa ya Avance Media inatoa dira hiyo kwamba imewatambua wanawake barani Afrika, kupitia mradi wa kuwawezesha wasichana uitwao 'Be A Girl' wakati wa uzinduzi wa jarida la kila mwaka, likiwa na taarifa kuhusu Wanawake 100 Waafrika Wenye Ushawishi Zaidi (100 Most Influential African Women).

Miongoni mwa waliotambuliwa mchango wao kwenye jamii kupitia vipengele 10 ikiwamo kipengele cha Utawala ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, Martha Karua, aliyekuwa Mgombea Mwenza wa Raila Odinga, kuwania urais nchini Kenya, kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Wengine kwenye kipengele hicho ni, Jaji Mkuu Martha Koome, nchini Kenya na Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Merck Foundation, Seneta Dk. Rasha Kelej, Ellen Johnson Sirleaf, aliyekuwa Rais wa Liberia na Graca Macel, wa Msumbiji.

Waliotajwa kuwapo kwenye orodha ya 'wanawake wenye ushawishi barani Afrika katika kipengele cha Ofisa Mtendaji Mkuu na Wahisani ni Ofisa Mtendaji Mkuu Klabu ya Simba nchini Babra Gonzaleze, na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala.

Taarifa kuhusu wanawake hao 100 wakiwamo wanasiasa, wasomi, wakurugenzi, makamishna zimepata umaarufu kwenye mitandao ya kijamii mwishoni mwa wiki, huku jarida hilo likibainisha lengo la kuwatambua wanawake hao ni kuhamasisha kizazi kijacho barani Afrika, ambao wana shauku ya kuongoza mabadiliko na kupigania utu, haki na sheria.

Jarida hilo la kila mwaka, hutoa simulizi mbalimbali kuhusu Waafrika na kuwaorodhesha kwenye machapisho kusherehekea pamoja na wanawake wengine ambao wana bidii kama wao na kuhamasisha kizazi kijacho cha viongozi barani Afrika.

Chapisho hilo kwenye orodha ya Wanawake 100 wenye ushawishi zaidi 2022, linatoa muhtasari wa wanawake waliopanda ngazi kwenye mashirika, kuanzisha biashara zao wenyewe au ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kufanya maamuzi ndani na nje ya nchi.

Wanawake hao mashuhuri walioangaziwa na jarida hilo ni pamoja na: Marais, Wanadiplomasia, Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi Wakuu, Wasomi, Makansela, Wanasiasa na Wanahisani, lengo ni kuwapa fursa muhimu na kutiwa moyo na pia kuendelea na hatua zao za kuweka viwango na rekodi za kimataifa

Wanawake wengine waliomo kwenye orodha hiyo, ni Waziri Mkuu wa Uganda, Robinah Nabbanja; Waziri Mkuu wa Namibia, Saara Kuugongelwa-Amadhila na Waziri Mkuu Victoire Tomegah Dogbe.

Akizungumza mmoja wa wanawake hao waliotambuliwa na jarida hilo, mara baada ya kutambuliwa kati wa wanawake 100 wenye ushawishi Dk. Rasha anasema:

"Ninaamini kwamba msichana aliyesoma ataongoza vyema kwenye maisha kiafya, ataokoa maisha, atajenga familia imara, atakuwa na kipato kizuri, ataiwezesha jamii yake na kuinua taifa lake na kupigania usawa."

Mwaka jana jarida la Forbes, pia lilimtambua Rais Samia, kati ya wanawake wachache waliowahi kushika wadhifa huo hapa barani Afrika.

Mwishoni mwa mwaka jana katika jarida maarufu la Forbes, 'The World's 100 Most Powerful Women' lililotolewa Desemba 7, Rais Samia alikuwamo kwenye orodha ya wanawake 100 maarufu.

Kati ya hao wenye asili ya kiafrika na kushiriki nyadhifa za juu yumo Makamu wa Rais Marekani, Kamala Harris na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala.

Kwenye jarida hilo la 18 la mwaka jana, lilibainisha viongozi wenye nguvu duniani, wakiwamo wakurugenzi wakuu na wajasiriamali mashuhuri, wakuu wa nchi, wahisani waanzilishi na watunga sera wanaotatua matatizo ya kijamii.

Katika orodha ya viongozi hao wanawake 100, wamo wakurugenzi wakuu wa taasisi na mashirika wapatao 40, pamoja na marais wanawake wachache wakitajwa wawili, akiwamo Samia na Rais Zuzana Caputova wa Slovakia.

Pia, wanawake hao wa nguvu katika jarida la Forbes 2021 walitajwa kuwa na ushawishi mkubwa katika kutoa mapato kutokana na shughuli tofauti, yanayokadiriwa kufikia Dola za Marekani trilioni 3.3 na kutoa ajira kwa wafanyakazi milioni 6.7.

Kadhalika, orodha ya wanawake hao inahusisha waliomo kwenye viwango vya mabilionea duniani, walio na thamani za mali ya Dola za Marekani bilioni 167.

Jarida hilo la Forbes, lilimuelezea Rais Samia kwamba ni rais wa kwanza mwanamke Tanzania, akichukua mamlaka baada ya kifo cha Dk. John Magufuli, Machi 17, mwaka huu.


Awali, pia alikuwa Makamu wa Rais wa Kwanza mwanamke Tanzania, tangu mwaka 2015.

Mnamo, Septemba mwaka jana, alikuwa mwanamke wa tano kutoka barani Afrika, kulihutubia Baraza la Umoja wa Mataifa.

Rais Samia aliangaziwa kwa kuwezesha kufanikisha elimu ya juu na kuwafikia wote, kwa kutenga Sh Bil 70 zaidi ya zilizotengwa ambazo ni bilioni 500, kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mkopo kwa ajili ya elimu ya juu.

Rais Samia, pia alitangaza kuwaruhusu wanafunzi waliokatiza masomo yao kwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata mimba shuleni, kurejea masomoni.

Pia, rais ameongeza vyumba vya madarasa na zimetengwa Sh. Bilioni 125 kwa ajili ya kukamilisha mabomba 10,000.



Mtendaji Mkuu wa timu ya Simba Sports Club; Barbara Gonzalez. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

BIASHARA

# Wauza samaki barabarani wanavyovutana na serikali ajenda ya kuhamia soko Mpanda

**NA NEEMA HUSSEIN,**
MPANDA

SERIKALI imeendelea kuboresha miondombinu ya masoko katika halmashauri mbalimbali nchini, ikiwemo kuongeza masoko, ili wafanyabiashara wadogo waondoke maeneo ambayo sio rasmi na salama kwa biashara zao na kuwahamishia katika masoko hayo.

Hivi karibuni Baraza la Madiwani la Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, lilipitisha ajenda kwa kumuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Mpanda, kuhakikisha anakamilisha ukarabati wa Soko la Samaki Kachoma.

Ni agizo lililotolewa, baada ya madiwani hao kuona samaki wabichi wakiuzwa bila ya mpangilio na wafanyabiashara hao kwa eneo ambalo sio salama katika maisha yao.

Magreth Shitungulu, ni Diwani wa Kata ya Kashauriri aliwasilisha hoja akitaka kuungwa mkono madiwani wengine.

Anaendelea kusema:"Mfano soko kuu ikifika saa tisa madeli yanapangwa kuanzia mwanzo wa barabara mpaka mwisho wa barabara," anasema Magreth

Ni hoja iliyoungwa mkono na Meya wa Manispaa ya Mpanda, Haidary Sumry, akisema "Ni kweli biashara hiyo imekuwa ikifanyika kila sehemu kutokana na soko hilo kushindwa kukamilika kwa wakati."

Kaimu Mkurugenzi Deodatus Kangu, anajibu kuwa soko hilo "tutatoa fedha zilizobaki ambazo ni milioni nne, ili kukamilisha na kupitia vikao vya kamati ya fedha tutaleta mpango wa kuanza kufanyika biashara katika soko hilo," anasema Mkurugenzi.



Soko la Samaki Kachoma, Mpanda linaloendelea kujengwa, linaolalamikiwa liko mbali.

**WAUZA SAMAKI**

Kaitasi Sui, muuzaji samaki wa Mpanda, ambaye ni miongoni mwa wanaouza pembezoni mwa barabara ya Soko Kuu Mpanda kila ifikapo jioni, anasema pamoja na serikali kuendelea kuboresha miondombinu katika Soko la Kachoma, bado kuna changamoto ya kukosa wateja sokoni hapo.

"Tuliwahi kuhamishwa tukapelekwa soko la kachoma lakini biashara kule haipo mazingira yaliyopo na jiografia ya mji kule soko halipo tulikua na mitaji yetu lakini ilikatika kwa kuozesha samaki pale.

"Sisi tupo hapa kama genge la jioni tu na tunafika hapa saa 12 jioni sio kama vile tupo hapa kama soko rasmi, mchana tunakuwa kwenye masoko mengine, kwa hiyo soko lile la kachoma wanalosema limekaa kama mwalo.

"Labda, angalau kama wanataka kutuhamisha wangetuweka katikati ya mji, ili tuendelee kufanya biashara zetu, mfano saa hizi masoko ni mengi mno!" anadokeza na kuendelea:

"Ukienda Nsemulwa kuna soko, Kwalakwacha kuna soko, Mpanda Hoteli soko lipo, sasa Mpanda Hoteli za Kachoma ni jirani sana. Sidhani kama mtu anaweza kuharibu nauli yake kwenda Kachoma kununua samaki wa elfu mbili au elfu tatu, sio rahisi.

"Sisi tunaomba serikali iangalie ni yepi mazingira rafiki watupeleke, ili sisi tuendelee kufanya biashara zetu, ila sio Kachoma. Kwa mfano, kuna maeneo hapa jirani walikuwa wanauza mitumba, kwanini wasituweke hapo sisi tufanye biashara," anahoji muuza samaki huyo.

Mjasiriamali mwingine. Frank Rudovick, ana maono haya:"Zamani watu walikuwa wanafanya biashara soko la kachoma lakini baadae wateja walikata watu wakabaki wanatangatanga.

"Serikali ikaamua tena kuliboresha lile soko, lakini mazingira ya kule yalishakuwa ni magumu sana kufanya biashara. Kule ni mbali, watu hawaji kwa wingi kama wanavyokuja hapa mjini ndiyo maana unakuta watu wengi tunakimbilia sehemu za kati.

"Ingependeza sana serikali ingefahamu kuwa watu wanafanya biashara vizuri kwa sehemu ambayo ni rahisi kufikika na ina mkusanyiko wa watu ikiwa mbali kupata wateja ni changamoto.

"Serikali ingebuni vizuri kuliko kila siku kuvutana na wananchi mara waende huku mara kesho warudi huku inaleta usumbufu,"anasema Frank.

Zainabu Mussa anasema soko hilo jipya liko mbali na lina ukomo wa muda, ndiyo maana akaamua kuuza bidhaa zake pembezoni mwa barabara hiyo, huku akiongeza walijipeleka wenyewe kufuata soko.

"Tulikuja hapa sababu ya changamoto tulizozipata kule samaki ziliharibika, sababu ya kuuza mwisho saa tano. Sisi hatujakataa kwenda kule, ila watutengee eneo ambalo litakuwa karibu na mazingira ya soko. Hili ambalo ni soko kuu au soko kubwa Mpanda,"anasema Zainabu.

**NENO LA MTEJA**

Hawa Kayanda, mteja wa bidhaa hiyo hapa anayetoa hoja "kwa kweli kwa hapa kwa sisi ambao tunahemea jioni, maana tunatoka makazini muda umeenda sasa soko likihamia kachoma ni mbali.

"Mimi nina shida na samaki za shilingi 2000, halafu nitoe shilingi 1000 ya nauli kwenda mpaka Kachoma kwenda na kurudi shilingi 2000 na sasa hivi uchumi ulivyo ni mgumu. Kwa hiyo, sisi wakazi wa Mtaa wa Kotazi na mitaa mingine, tunashindwa halafu hili soko huku ndani linafungwa saa 12.

"Tukitoka kazini tumechoka tunakimbia hapa kuhemea tunaenda kupika, sasa inakuwaje sisi twende hadi Kachoma. Mimi naishauri serikali, kama wamekosea sehemu nzuri ya kuwapeleka wawaache (wauza samaki) hapa hapa, hata sisi wahemeaji wa jioni tufaidike," anasema Hawa.

**KIONGOZI SOKO**

Benedicto Sylvester, Makamu Mwenyekiti wa Soko kubwa Mpanda, anasema wateja wanaokwenda pale wengi ni wafanyakazi wanaotoka jioni na kupitia mboga kwenda kupika.

"Mimi ningeishauri halmashauri wangetafuta eneo la katikati ya mji hata kama ndani ya hili soko kubwa, ili hawa waweze kufanyabiashara zao sababu hawa ni wafanya biashara wadogo wadogo.

"Pia, hata usalama wa hii barabara ni mdogo sana, kwa sababu magari ni mengi, pikipiki ni nyingi wawaache hapa ila wawaweke ndani ya soko, sio hapa barabarani, ili waendelee kufanya biashara zao kwa uhuru na muda wote" alisema



Wauza samakii wakiwa kazini barabarani, ambako wanagoma kuhama. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN..**

BIASHARA

# Ijue siri iliyokamata ujasiriamali wa Kahawa jijini Tanga, mafanikio yake

**Na Boniface Gideon,** TANGA

UKIFIKA katika Jiji la Tanga hususani nyakati za asubuhi na jioni, ni lazima utakutana na vijana wadogo wakiwa wameshika chupa za chai mbili au tatu na ndoo lita nne inatumika kuhifadhia vikombe.

Pia utamaduni wa jiji la Tanga kila siku, bila kuangalia ni siku za wikiendi au za kawaida, kuna magenge ya vikundi vya watu wakinywa kahawa, tangawizi na alikasusi huku wakibishana habari aidha za mpira Simba na Yanga au siasa.

Biashara ya kuuza kahawa, tangawizi na alikasusi kwa asilimia kubwa hapa jijini Tanga inafanywa na vijana wadogo kiumri na kima cha urefu, umri wao ni chini ya miaka 21 na ukiwauliza watakwambia kuwa wamemaliza darasa la saba au kidato cha nne, kupitia biashara hiyo hiyo ukimdadisi anakwambia ameanza kujenga nyumba kijijini kwao au kanunua kiwanja mjini.

Biashara hii haina kituo maalumu, pia haihitaji mtaji mkubwa, gharama kubwa iliyoko ni kununua vifaa vya kuhifadhi kahawa na tangawizi, yaani chupa za chai na angalau mbili au birika mbili, kwa wale wasiopendelea kuzunguka sana kutafuta wateja.

Vingime ni kashata, maaarufu kama kitafunwa cha kahawa na tangawizi.

Wakati kwenye biashara ya kuuza alikasusi kinywaji ambacho kwa mujibu wa wenyeji wa Jiji la Tanga wanadai zuna msaada kwao kiafya, japo hakuna uthibitisho wowote kutoka kwa wataalamu wa afya, kwa sasa ni kinywaji pendwa sana na utawakuta zaidi wanaume hususani vijana wakiwa wamezunguka duara kununua.

Kwa ujumla mtaji mkubwa wa biashara hizi huwa hauzidi Sh.100,000, lakini baada ya hapo huingiza pesa faida kubwa, kikombe kimoja cha kahawa ni Sh.100 ambapo chupa moja hutoa vikombe vidogo vya kahawa zaidi ya 30. Tangawizi kwa sasa inauzwa Sh.200 kikombe chenye ujazo sawa na kahawa na alkasusi ni Sh.500-600.

**VIJANA WATUMIA FURSA**

Ally Saleh kijana mwenye miaka 19, anasema biashara hizo yeye alianza kufanya mwaka 2019, baada ya kumaliza darasa la saba. Hakufanikiwa kwenda sekondari lakini adai kwa sasa 'mambo yanamwendea safi.'

" Unajua mimi na darasani ni tofauti kabisa na nilikuwa naenda shule kusindikiza wenzangu tu, mimi nataka kuwa mfanyabiashara mkubwa na mkulima, kwetu Lushoto. Wazazi wangu wapo hapa mjini ni wafanyabiashara wa vyakula, Mimi mpaka leo hii nimenunua kiwanja huko Pongwe nataka nianze kujenga kidogo kidogo kupitia biashara hii," anabainisha Ally.

Anasema kwa siku ana uhakika wa kulaza Sh.12,000-15000 faida kwa biashara hizo zote kwa ujumla.

"Nashukuru kiukweli hii biashara inakipato japo sio kikubwa sana lakini chatosha kwa umri wangu sina familia inayonitegemea hii ni fursa kubwa sana nashukuru kwa hilo," anasema.

Kijana Mohammed Saleh ( 21) mkazi wa Barabara ya 15 na mfanyabiashara wa vinywaji hivyo, anasema kwa muda mfupi aliyofanya biashara hiyo amefanikiwa kuanza kumjengea nyumba mama yake mzazi huko wilayani Korogwe katika kijiji Cha Kwasunga.

"Mimi nipo hapa mjini tokea mwaka 2020 na nilikuja kufanya kazi ya kusaga nafaka kwenye mashine za Barabara ya 15, lakini bosi wangu alipata matatizo na kulazimika kufunga mashine, hali ilikuwa ni ngumu sana.

"Nilianza kuuza kahawa peke yake nikawa na uhakika wa kuingiza Sh. 4,500 kila siku lakini mimi kwa sasa hivi naingiza hadi Sh.20,000 kwa siku na pia nimeajiri vijana wawili nawalipa kwa mwezi 50,000 kama wengine wanavyolipa mishahara kwa watembeza kahawa." Anabainisha.

Anasema tokea ameanza kazi hiyo amefanikiwa kununua kiwanja huko Kange kupitia viwanja vya gharama nafuu vya halmashauri lakini anamjengea nyumba mama yake mzazi.

**WADAU NA WANANCHI**

Wadau, akiwamo Muya Kayombo, mfanyabiashara anasema biashara wanayoifanya vijana hao ni nzuri na wakijiunda katika vikundi wanaweza kusaidiwa na halmashauri kupitia mikopo isiyokuwa na riba.

"Kama watapata watu sahihi wakuwaongoza basi wanao uwezo wa kupata mikopo halmashauri mimi nimewasaidia baadhi yao kuwapa mitaji ni kama kuunga mkono tu.

"Lakini, kiukweli bado wanahitaji usimamizi wa watu wazima hususani wazazi kwasababu wengi wao umri wao ni mdogo japo wamemaliza shule lakini usimamizi wa matumizi sahihi ya fedha unahitajika," alisema Muya.

Zena Said, mfanyabiashara wa vyakula Barabara ya 15 anasema biashara ya vinywaji hivyo inawaingizia kipato kikubwa sana kutokana na Utamaduni wa Jiji la Tanga watu wake wanatumia vinywaji hivyo kama kiburudisho mbadala wa pombe.

"Unajua hapa Tanga Mjini watu sio wanywaji wa pombe kutokana na mfumo wa kidini, kwa hiyo vinywaji hivyo vinapendwa sana kuliko kitu chochote kile kwa kuwa havileweshi na vinapendwa sana na kinababa kuliko kinamama," anasisitiza Zena.





Biashara ya kahawa ikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

## CHEMSHABONGO NA -00 25 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. hakimu wa mahakama kuu
5. mambo yasiyothibitishwa
8. itikadi ya mtu kwenye dini
10.bwana mheshimiwa
11.desturi 12.nema, jipinda
13.Tehrani ni mji mkuu
17.tendo la kuwia mtu radhi
19.Mke wa Lameki 20.sujudia
21.mdudu jamii ya nzige
22.mafuta 23. ikiwa 24.tendo la kupingua


Chini:
1. mji mkubwa sana
2. utulivu 3. siku iliyopita
4. fanya mtu au kitu kiiname vielekee chini
6. kitu kilichotolewa sadaka
7. misa
9. kifungu cha maneno kamili
14.msitu mkubwa Brazil
15.Mjumbe wa Mungu
16.masalia ya kitu
17.kabla ya wakati uliotajwa
18.tesa mtu



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MUNGU
FUMA
UMATI
JALALA
AMANA
KIINI
AISEE
ELEWA
MLANGO
MALAI
KIGALI
ATAMIA
UBANI
ILANI
ANISE
NEEMA

AGA
AGO
IMA
ALA
NOA
APA
NTI
UMA
WALI
ELI
AGA
ONA
FUJO




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H | A | M | A | K | I | | T | | T |
| A | W | A | L | I | | K | A | K | A |
| B | A | R | A | Z | A | | F | | M |
| A | M | A | | A | | Z | A | H | A |
| R | U | D | I | | | | K | | N |
| I | | H | | T | A | M | A | T | I |
| | S | I | H | A | | A | R | I | |
| M | | | A | B | I | R | I | A | |
| T | A | M | B | I | | A | | | U |
| A | | T | A | B | O | R | A | | Z |
| A | G | O | | U | | A | U | L | A |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| T | U | N | D | A | | T | O | A | |
| A | D | A | A | | M | U | N | G | U |
| N | I | N | I | | A | M | A | A | |
| G | | | M | A | R | A | | | U |
| A | | M | A | D | A | | | | T |
| Z | O | A | | H | I | M | A | Y | A |
| A | | A | N | A | S | A | | | L |
| | | L | | B | | U | H | A | I |
| M | B | U | Y | U | | T | A | W | I |
| | | M | | | K | I | U | A | |



## HABARI MBEYA

# Bilioni 300/- kutumika kwenye mradi wa maji

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka Mto Kiwira ulioko wilayani Rungwe, Mkoa wa Mbeya wenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 125 kwa siku.

Mradi huo tayari umefikia hatua mbalimbali zikijumuisha usanifu wa mradi na upembezi yakinifu na sasa ujenzi umeanza, ukitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 300.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edna Mwaigomole, alisema jana jijini hapo kuwa mradi huo utasaidia kukidhi mahitaji ya wananchi wanaoishi jijini Mbeya na maeneo yanayozunguka mji huo.

Alisema mradi huo pia utasaidia kufanikisha shughuli za kijamii na uzalishaji mali, viwanda vidogo na vikubwa ambavyo hutegemea maji kuendesha mitambo na mahitaji mengine.

"Uwezo wa mamlaka yetu sasa ni kuzalisha maji lita milioni 65 kwa siku huku mahitaji ya Jiji la Mbeya yakiwa ni lita milioni 90, hivyo tuna upungufu wa lita milioni 25," alisema Mwaigomole.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma kwa Wateja, Neema Mangwala, alisema kuna tatizo kubwa la uharibifu wa miundombinu ya maji, hali inayosababisha maji kumwagika na maeneo mengine kukosa huduma.

Kiongozi huyo pia alisema kuna kikwazo kingine kwao kiutendaji cha wateja kutolipa ankara za maji, hivyo kusababisha shida katika utekelezaji miradi mingine ya maji.

Alibainisha kuwa kwa sasa mamlaka hiyo inawadai wateja wake Sh. bilioni 1.9 na inaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha deni hilo linalipwa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Bomba Mbili, Kata ya Mwakibete, Rodrick Mwang'onda, alisema watakuwa mabalozi wazuri kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa ili kuondoka na shida ya uhaba wa maji katika maeneo ya Jiji la Mbeya.

Mkazi wa Mtaa wa Ghana, Rehema Braison, aliiomba mamlaka hiyo kuendelea kufanya usafi kwenye vyanzo mbalimbali vya maji ili wananchi wapate huduma

# Ukatili kijinsia, dawa za kulevya vyachochea maambukizi VVU

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MATUMIZI ya dawa za kulenya na ukatili wa kijinsia vimetajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya Virusi ya Ukimwi (VVU) mkoani Mbeya.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alitoa kauli hiyo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Alisema matumizi ya dawa za kulevya aina ya bangi yanachochea ongezeko la maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 mpaka 49.

Alisema ili kukabiliana na matumizi ya bangi ambayo yamekuwa kichocheo kikubwa cha watu kupata maambukizi vya VVU, aliwataka wananchi kutoa taarifa ya watu wanaotumia au kuuza kwenye maeneo yao ili wachukuliwe hatua za kisheria.

"Matumizi ya bangi yamekuwa kichocheo, yanachangia kwa kiwango kikubwa maambukizi ya VVU, sasa tuna kazi ya ziada katika kuhakikisha tunadhibiti matumizi ya dawa hizo ambazo zinatumiwa na vijana wengi siku hizi, wananchi kwenye maeneo yenu mtakuwa mnawafahamu wanaotumia na kuuza, tupeni taarifa ili tuwashughulikie," alisema. Dk. Chuachua pia aliwahamasisha wanaume kujitokeza kwa wingi kupata huduma za tohara ili kukabiliana na maambukizi ya VVU.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka Septemba mwaka huu, takribani wanaume 40,000 wa mkoa huo wamepata huduma ya tohara.

Alisema idadi hiyo ni ndogo, hivyo aliwahamasisha wanaume ambao hajawapata huduma hiyo, kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata tohara ambayo itawasaidia kujikinga na VVU.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo, alisema utafiti unaonyesha kuwa wanaume ambao hawajafanyiwa tohara, wako katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya VVU.

Alisema utafiti huo unaonyesha tohara inawakinga wanaume dhidi ya VVU kwa asilimia 60, hivyo ni muhimu suala hilo likachukuliwa kwa uzito.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo (wa pili kushoto), akiwasilisha taarifa ya hali ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi mkoani humo, kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, kimkoa kwenye viwanja vya stendi ya Mbalizi jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mauaji ya watu yamshtua RC

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kutoa mafunzo kwa wamiliki wa silaha ili kupunguza wimbi la watu wanaojichukulia sheria mkononi na kugharimu maisha yao na watu wengine.

Homera alitoa maagizo hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari na kutoa kauli ya serikali kuhusu kushamiri kwa vitendo vya ukatili, yakiwamo mauaji.

Alisema mauaji yaliyotokea katika kipindi cha wiki moja, yote yanatokana na matumizi ya silaha, watu kutoa uhai wao na wengine kuwaua wenzao.

Mkuu wa Mkoa alisema katika kukabiliana na ongezeko la watu kujichukulia sheria mkononi kwa kutumia silaha, Jeshi la Polisi linatakiwa kutoa mafunzo maalum kwa wamiliki wote waliosajiliwa, kufundishwa namna bora ya kuzitumia ili kuepuka mauaji.

"Ninaliagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine kutoa mafunzo maalum kwa wamiliki wote wa silaha Mkoa wa Mbeya ambayo yatakuwa ya mwezi mmoja, kila wilaya na halmashauri itafanya katika maeneo yao.

"Ninakemea mauaji yaliyotokea hivi karibuni ambayo yamehusisha matumizi ya silaha ambazo kwa mujibu wa sheria waliziomba kwa ajili ya kujilinda wao wenyewe na sio kugharimu maisha ya wengine, likiwamo tukio lililotokea Novemba 28, mwaka huu ambapo Emmanuel Luhwesha (31), mchimbaji na mnunuzi madini ya dhahabu wilayani Chunya alimuua kwa kumpiga risasi William Mgaya (58), mkusanya ushuru kutoka Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) jijini Mbeya," alisema.

Homera alisema tayari Jeshi la Polisi linamshikilia mtuhumiwa huyo na atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa tukio lingine ni la askari wa Kampuni ya Ulinzi ya Suma JKT, Osea Kashililika (21) ambaye anadaiwa kujiua kwa kujipiga risasi akiwa katika lindo Benki ya Azania jijini Mbeya.


Alisema mauaji yaliyotokea katika kipindi cha wiki moja yanatokana na matumizi ya silaha, watu kutoa uhai wao na wengine kuwaua wenzao.

Baadhi ya wananchi wa Jiji la Mbeya walisema miongoni mwa sababu zinazochangia watu kujichukulia sheria mkononi ni msongo wa mawazo.

Boaz Asangalwisye alisema idadi kubwa ya wanaofanya vitendo vya mauaji ni wanaume, akidai wanafanya hivyo kutokana na tatizo la afya ya akili ambalo linatokana na msongo wa mawazo.



## HABARI DODOMA



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax (katikati), akiwa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Christine Musisi (wa pili kulia) na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (wa pili kushoto), wakizindua mfumo maalum utakaotumika kuonyesha fursa mbalimbali za uwekezaji zilizoko nchini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# 'Haki za binadamu zisiwe maficho ndoa jinsia moja'

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

MRATIBU wa Idara ya Elimu Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma ameiomba serikali kutokukubali vitendo vinavyopingana na mpango wa uumbaji wa Mungu, zikiwamo ndoa za jinsia moja, kwa kisingizio cha haki za binadamu.

Padri Chrisant Mganga alitoa rai hiyo jana alipozungumza kwenye mahafali ya saba ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mt. Crala wilayani Kongwa.

Alisema kwa sasa wapo baadhi ya viongozi katika nchi za kiafrika wamerubuniwa na kuruhusu vitendo vya ushoga na usagaji kwenye mataifa yao ili kutimiza alichokiita masharti ya misaada wanayopokea kutoka katika mataifa yaliyohalalisha vitendo hivyo.

"Tunawaomba viongozi wetu wawe na hofu ya Mungu, kuna mambo ya ushoga ambayo yanaendelea mitaani na kwenye taasisi zetu, tunajifanya kama hayapo hivi lakini yapo yanayotumong'onyoa na yanatumaliza.

"Usagaji upo, hatutaki kusema, matendo haya yanaendelea kwa siri na ni mitandao kuna watu wanaofanya hayo kwa kigezo cha haki za binadamu, wanatengeneza mitandao na watoto wetu wanaingia humo," alisema. Aliwaasa Watanzania kutoyapa nafasi mambo yanayoharibu utamaduni na maadili ya kiafrika.

"Wanatumia kivuli cha nyota za kijani na haki za binadamu kutimiza azma yao na pasipo kujua watu wetu wananaswa na mambo hayo. Kanisa Katoliki linakataa kuhusu matumizi ya vidonge na vipandikizi vya kuzuia mimba lakini watu wanachangamkia na hayo ndiyo yanawaharibu na wengine wanatetea kabisa kwamba hii 'ni haki yangu'," alisema.

Akizungumzia mmomonyoko wa maadili, Padri Mganga alisema vitendo viovu vinavyotokea katika jamii ya sasa ni kwa sababu ya uzembe wa malezi na maadili.

"Yanayoendelea sasa hivi ukisikia baba kazaa na mtoto wake wa kumzaa, mama ameolewa na mtoto wake, mtawa amevunja ndoa ya mtu au padri amefanya mambo ya ajabu kwa watoto ni kwa sababu ya uzembe wa malezi na maadili," alisema. Kiongozi huyo wa kiroho pia alitahadharisha kuhusu utitiri wa makanisa na wahubiri wa kila aina wanaojivisha vyeo na kutangazia watu injili ya mafanikio.

"Kuna kitu kinaitwa injili ya mafanikio, sasa hivi kuna madhehebu yanaibuka kila mahali watu wanaanzisha makanisa na wanajipa na vyeo. Kwa sasa hadi wasanii wa nyimbo za kidunia wengine wamekuwa na makanisa yao na tunawafahamu watu wanatafuta namna ya kuishi," alisema.

# CCM yataka wafanyakazi wajikinge majanga kazini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Christina Mndeme, amewataka wafanyakazi nchini kujikinga na majanga wanapokuwa kwenye maeneo ya kazi.

Alitoa rai hiyo juzi alipofungua semina ya masuala ya fidia kwa wafanyakazi iliyoandaliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Mndeme pia alitaka taasisi zote kulipa michango ya nyuma zinayodaiwa katika mfuko huo.

"Mfuko wa kulipa fidia upo lakini ni muhimu sana kujikinga na majanga, msichukulie mfuko upo utalipwa, lakini unapata janga la aina gani, unapata janga ambalo linakupa ulemavu.

"Taasisi lipeni michango ya sasa na yale mnayodaiwa ili taasisi hii iwe na ukwasi wa kutosha, taasisi hii ikifa wengi tutaathirika, na uimara wa mfuko unategemea michango ya waajiri, ni jukumu la kila mmoja kulipa," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema jukumu kuu la mfuko huo ni kuhakikisha Watanzania hawapati madhara na kuingia kwenye wimbi la umaskini pale wanapopata matatizo sehemu za kazi.

Dk. Mduma alisema wanatambua Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 ibara ya 30(d) inaelekeza suala hilo.

# Zungu aonya vijana maambukizi ya VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu, amesema Bunge la Vijana la mwaka 2022 lipaswa kuwaasa vijana kujiepusha na ngono zembe zinazosababisha kuwa hatari ya kupata maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

Takwimu zinaonyesha asilimia 40 ya maambukizi hayo yapo kwa vijana.

Zungu alibainisha hayo jana alipohutubia Bunge la Vijana linalofanyika Ukumbi wa Msekwa bungeni jijini hapo likiwa na kaulimbiu ya 'Nafasi ya Vijana katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi'.

"Desemba Mosi kila mwaka ni Siku ya Ukimwi Duniani, maambukizi yamepungua lakini kwa kundi la vijana yameongezeka, fungueni masikio na akili zenu, vijana wengi mnafanya ngono isiyo salama, kwanini ufanye ngono wakati huna mume wala mke? Vitabu vya dini vimekataza uzinifu," alionya.

Zungu alisema Bunge hilo linapaswa kutumika kuwaasa vijana wanaojiingiza kwenye ngono wakiwa na umri mdogo.

Alisema uandaaji wa Bunge la Vijana unalenga vijana kuelewa taratibu za uendeshaji wa Bunge, kuwaandaa kuwa viongozi bora wa baadaye, kuwafundisha kuvumiliana, kubishana kwa hoja na kuheshimu mawazo ya wengine.

"Bunge hili pia linalenga kuelimisha vijana juu ya matatizo yanayozikabili jamii na taifa kwa ujumla na kuwafundisha umuhimu wa kufikia uamuzi baada ya mjadala wa pamoja," alisema.

Kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira, Zungu alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akihimiza umuhimu wa kutunza mazingira wakati ambao dunia inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira.

"Hivi karibuni Rais Samia alishiriki mkutano ambao viongozi walikuwa wakizungumza juu ya kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi na kutoa mfano kuongezeka kwa ukame, kuyeyuka barafu, kuongezeka joto, ninaamini kupitia Bunge hili mtakuwa mmejifunza namna ya kushughulikia miswada ya serikali," alisema.

Aliwaomba kuweka maazimio kwenye vikao vyao ikiwamo ya kupongeza kama tukio la Rais Samia kupewa udaktari wa falsafa ya mchango wake kwa taifa na jamii.

Spika wa Bunge hilo, Antipas Pamba aliwaasa vijana kama wana ndoto ya kufika mbali, hawana budi kulinda afya zao.



# Taasisi ya usimamizi serikali kuzinduliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar inatarajia kuzindua Taasisi mpya ya Ofisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi Serikalini (PBD) hafla itakayofanyika leo Ikulu, Zanzibar.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Ikulu Zanzibar, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Charles Hillary, alisema uzinduzi huo utafanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika viwanja vya Ikulu.

Hillary alisema lengo la taasisi hiyo ni kuhakikisha utendaji wa serikali na matokeo yake yanaonekana kwa wananchi.

Alisema taasisi hiyo ni mpya na baada ya kuundwa italeta mabadiliko makubwa ya kiutendaji na usimamizi serikali.

"Tunategemea kuwa baada ya kuundwa kwa taasisi hii, utendaji na usimamizi utabadilika kwa sababu kutakuwa na chombo ambacho kitasimamia kila idara na wizara na taasisi kufanya kazi zake kwa ubora na usahihi," alisema.

Aidha, alisema katika uzinduzi huo wageni 250 watahudhuria wakiwamo mawaziri, naibu mawaziri wa SMZ, makatibu wakuu, viongozi wa taasisi za serikali na mabalozi 20 wanaowakilisha nchi zao Tanzania na maafisa wanaosimamia taasisi hiyo kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Mkurugenzi huyo alisema baada ya kumalizika kwa uzinduzi huo, uelewa wa wananchi utakuwa mkubwa kwa kutegemea waandishi wa habari kupeleka taarifa kuhusu uzinduzi huo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar Fedha na Mipango, Jamal Kassim (wa pili kushoto), akikabidhi tuzo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu, baada ya benki hiyo kuwa miongoni mwa benki tatu bora katika uandaaji wa taarifa za fedha ya Mwaka 2021, zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), mkoani Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA, Prof. Sylivia Shayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yahadharisha uwapo wa UVIKO- 19

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema bado ugonjwa wa UVIKO-19 upo, hivyo ni vyema wananchi wakachukua tahadhari dihidi ya ugonjwa huo ambao unaathiri nguvu kazi ya taifa.

Asha Ussi Khamis, kutoka Wizara ya Afya Kitengo cha Kuratibu na Kukabiliana na Dharura za Kiafya, alisema tokea Machi mwaka jana hadi Novemba, mwaka huu, watu 87 wameshafariki dunia visiwani hapa kwa ugonjwa huo na watu 780 wamepata maambukizi.

Ofisa huyo aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu UVIKO-19 yalioandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) kwa kushirikiana na Shirika la Internews chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID) yaliofanyika mjini Zanzibar.

Alisema waandishi wa habari wana umuhimu katika kusaidia kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mlipuko ikiwamo UVIKO-19, hivyo ni vyema kuendelea kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa chanjo ya ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Asha, bado baadhi ya wanajamii wanakataa kupima ugonjwa wa UVIKO-19 na wanakataa chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo ambayo ni salama kwa afya ya binadamu.

Alisema changamoto za chanjo zinarudisha nyuma kufikia malengo ya kuchanga watu asilimia 70 ifikapo Desemba, mwaka huu, na watu waliochanja hadi sasa ni asilimia 43.

Licha ya juhudi mbalimbali za kuwafikia wananchi kwa ajili ya kuchanja, alisema bado baadhi ya wananchi hawana mwamko kwa sababu chanjo zipo za kutosha, hivyo watu wakubali kuchanja ili kupunguza kasi ya ugonjwa huo.

Alisema baada ya uwapo wa chanjo hizo, ugonjwa umepungua na wale walioachanja na kupata ugonjwa hawajaathirika tofauti na wale ambao hawajachanja na kupata ugonjwa huo.

Pia alisema hivi sasa kuna mlipuko wa homa kali ya mafua inayofanana na UVIKO-19, hivyo Wizara ya Afya inafanya uchunguzi wa sampuli za vimelea vya ugonjwa huo ili kujua vimelea hivyo , vinalingana na vya UVIKO-19.

"Tayari tumeshachukua sampuli ya vimelea na kuvipeleka Tanzania bara kwa ajili ya kupata majibu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa ZPC, Abdallah Abrahman Mfaume, aliwataka waandishi wa habari kuhakikisha wanafuata maadili ya taaluma yao wakati wanapotekeleza wajibu wao wa kuelimisha jamii kuhusu mambo mabalimbali.

"Waandishi wa habari kazi yetu kubwa ni kuwasemea wale wasio na sauti lakini pia kuelimisha jamii hivyo ni vyema kufanya habari za uchunguzi ili kuibua maovu na mamlaka husika kuchukua hatua katika kuondosha changamoto zilizoko," alisema.

Alisema wako baadhi ya waandishi wa habari wakaacha chanjo ya UVIKO-19 wakati ndio kioo cha jamii, hivyo ni vyema kupata chanjo hiyo huku wakielendelea kuhamasisha jamii kupata chanjo.

Waandishi wa habari waliopatiwa mafunzo hayo waliitaka Wizara ya Afya kuwa wazi hasa pale waandishi wanapotaka taarifa kwa lengo la kuelimisha jamii.

# Mwinyi asema serikali imefungua milango uwekezaji kukuza uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali imefungua milango kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi katika kukuza na kuimarisha uchumi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, katika uzinduzi wa Jukwaa la Biashara na Uwekezaji lililofanyika katika hoteli ya Golden Tulip.

Alisema kuongezeka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya Zanzibar kutasaidia kufikia maendeleo jumuishi kiuchumi na kijamii, ikijumuisha eneo la biashara huria katika Bara la Afrika ikiwa ni miongoni mwa miradi mikuu katika mfumo wa maendeleo wa Afrika.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, serikali inafanya kazi kwa karibu na sekta binafsi ili kutoa fursa katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na ni dhahiri uwekezaji unaofanywa unaotoka katika taasisi za fedha za Afrika, una tafsiri kwa vitendo azma ya serikali.

"Lazima nikiri kuwa nina shauku kubwa sana ya kuona mawazo yenu, ufahamu wenu pamoja na mapendekezo yenu yanaweza kutumika katika kuboresha zaidi mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hapa Zanzibar," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema suala la kukuza uwekezaji limekuwa moja ya misingi na ajenda ya maendeleo kwa serikali ikiwa inaenda sambamba na sera ya kitaifa ya kukuza uwekezaji hasa kupitia uchumi wa buluu.


Alisema serikali imeanza kutekeleza mradi wa kimkakati wa uchumi, mradi wa nishati mbadala, ujenzi wa bandari ya Mangapwani pamoja na miundombinu ya barabara.

Pia alisema serikali inaendelea kulinda amani na utulivu uliopo nchini kwa kuwa na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa misingi ya utawala bora imedhamiria kukuza uwekezaji kwa maslahi ya wananchi wake wote.

Hata hivyo, alisema licha ya kukumbwa kwa mlipuko wa maradhi ya UVIKO- 19 bado Zanzibar inaendelea kuimarika katika sekta ya uwekezaji na biashara ambapo miradi mbalimbali imeanzishwa na kuzalisha ajira nyingi kwa vijana.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema Afrika inapanua wigo wa soko la kukuza biashara na uwekezaji hatua ambayo inasaidia kukuza seka hiyo barani humo.

Naye Mwakilishi wa Afrexim Bank, Dk. Gainamore Zanamwe, ameonyesha kufurahishwa kwake kwa fursa nyingi za kiuchumi zilizoko Zanzibar na kuahidi kutoa kipaumbele katika mipango yao ya mikopo nafuu katika kuunga mkono miradi mbalimbali Zanzibar.






Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Bulyanhulu, wilayani Msalala, mkoani Shinyanga, wakisoma vipeperushi vyenye kuelimisha jinsi ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia wakati wa mafunzo ya kupinga vitendo hivyo, yaliyoandaliwa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadaiwa kusitisha masomo siku za hedhi

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

BAADHI ya wanafunzi wa kike kutoka Shule ya Msingi Lyamidati, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamedaiwa kusitisha masomo kwa muda pindi wanapoingia katika mzunguko wa hedhi kutokana na ukosefu wa elimu ya hedhi salama kwa wanafunzi hao.

Shule hiyo yenye wanafunzi 954 ikiwa kati yao wanafunzi wa kiume ni 473 na wa kike ni 451, imeelezwa idadi yao kupungua shuleni kipindi cha hedhi hasa kwa wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kununua taulo za kike, hivyo kulazimika kubaki nyumbani mpaka mzunguko wake ukiisha.

Hayo yalibainishwa na wanafunzi wa shule hiyo wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Sauti za Kayana Vyombo vya Habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga (SPC) kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Happiness James, mwanafunzi wa darasa la sita, alisema licha ya kupewa elimu ya namna ya kujisitiri wakati wa hedhi na mwalimu wao, bado hawana uwezo wa kununua taulo za kike. Badala yake, alisema wanaendelea kutumia vitu ambavyo si salama kwao wakati mwingine uchukua uamuzi wa kubaki nyumbani kabisa hadi kuisha kwa mzunguko wao.

Alisema vitu ambavyo wamekuwa wakitumia mara kwa mara nipamoja na magazeti, karatasi za madaftari yao, vidaso, vitambaa pamoja na vipande vya magodoro ambavyo wanavitoa kwenye magodoro wanayotumia majumbani mwao na inawafanya kupata miwasho sehemu ya mara kwa mara.

Naye Mariam Wilson, alisema licha ya kuwa na changamoto hizo, wanajiepusha kuingia kwenye vishawishi vya kupata taulo za kisasa za kike kutoka kwa vijana waharibifu na kuiomba serikali kuwasaidia kutenga bajeti ya kununua taulo za dharura shuleni ili wasiendelee kukosa masomo yao.

Mwalimu msimamizi wa klabu za wanafunzi wa kike kwenye masuala ya usafi wa hedhi shuleni, Dorice Njogopa, alisema shule imeweka utaratibu wa kukutana na wanafunzi wenye lika balehe kila wiki na kuwapatia elimu ya matumizi ya taulo, usafi na madhara pale wanapotumia vidaso au magazeti.

Alisema wanazo taulo za dharura na mwanafunzi wasiokuwa na uwezo wa kununua wanapoingia katika mzunguko wake hasa akiwa darasani hutoa taarifa na kumpatia na changamoto waliyonayo ni ukosefu wa chumba maalumu cha kubadilishia taulo hizo kwani wanahofia wanafunzi kuzitupa ovyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Lyamidati, Irene Mchuma, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali ya Heneriko na Red Cross yalifika shuleni na kuwapatia wanafunzi taulo za kike, nguo za ndani, mabegi, viatu na madaftari lengo likiwa ni kutatua changamoto hasa kwa wanafunzi wakike na kuhakikisha wahaingii kwenye vishawishi.

# RC ataka mazingira rafiki ukusanyaji kodi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, ameitaka Mamlaka ya Mapoto Tanzania (TRA) Mkoa wa Geita, kuweka mazingira rafiki ya ukusanyaji wa mapato ili kuweka ufanisi mkubwa.

Shigela alisema hayo juzi mjini hapo wakati akitoa vyeti kwa walipakodi waliofanya vizuri kwa kulipa kodi bila shuruti mkoani hapo. Alisema ili serikali ifikie malengo yake lazima kuwapo na mazungumzo na wafanyabiashara pamoja na kuwapatia elimu badala ya kutumia nguvu katika kukusanya mapato.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Mambo ya Ndani wa TRA, Ndositwe Haonga, akizungumza kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa TRA, alisema kupitia elimu ambayo wamekuwa wakiitoa kwa wafanyabiashara, kila mara imeonyesha mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa kodi.

Ndositwe alisema mamlaka hiyo imejipanga kuboresha matumizi ya mashine za kielektroniki na ujenzi wa vituo vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kusajili walipakodi na kubuni vyanzo vya mapato. Meneja wa TRA Mkoa wa Geita, Hashim Ngoda, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 walikusanya asilimia 97 na kwa kipindi cha Julai - Oktoba, mwaka huu, wamekusanya Sh. bilioni 25 sawa na ufanisi wa asilimia 208 kwa lengo la kipindi hicho huku lengo likiwa kukusanya Sh. bilioni 35 kwa mwaka 2022/23.

Baadhi ya wafanyabiashara waliopatiwa vyeti hivyo akiwamo, Mkurugenzi wa Blue Cost Investment, Athanas Inyasi, waliishukuru serikali kupitia TRA kwa kutoa motisha kwao na kuahidi kuendelea kulipa kodi bila shuruti.

Katika hatua nyingine, TRA mkoani Geita, imetoa msaada wa taulo za kike kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nyankumbu na msaada wa vitu mbalimbali vikiwamo vifaa vya shule kama madaftari, sabuni, miswaki, mafuta ya kujipaka, unga na mchele kwenye vituo vya watoto wenye mahitaji maalumu. Vitu vyote hivyo vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni sita.

## Mshtakiwa mauaji ana kesi ya kujibu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemwona mkazi wa Kijiji cha Nyashimba, Wilaya ya Mbogwe, Joseph Masolwa (40), kuwa na kesi ya kujibu baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Mshtakiwa huyo ameshtakiwa kwa kosa la mauaji ya kumuua Mbula Mbweso kwa kumcharanga mapanga kichwani na shingoni na kumsababishia kifo papo hapo.

Awali, mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Kamana Stanley na kupelekwa mahabusu kutokana na kesi inayomkabili kutokuwa na dhamana.

Akitoa uamuzi mdogo, Jaji Kamana alisema mahakama imetilia maanani ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na kuona ni mzito, hivyo mshtakiwa anayo kesi ya kujibu.

Jaji Kamana alisema upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Gisela Alex, alipeleka mashahidi sita na vielelezo vitano ambavyo vilionyesha kuwa mshtakiwa anayo kesi ya kujibu.

Pia Jaji Kamana alimuuliza Wakili wa Kujitegemea, Erick Lutehanga, ambaye anamtetea mshtakiwa huyo kwamba mteja wake anajitetea kwa namna gani na kujibu kuwa atajitetea kwa kiapo na atatoa utetezi peke yake na hana shahidi wala kielelezo.

Baada ya mshtakiwa huyo kumaliza kujitetea peke yake hakuwa na shahidi wala kielelezo, Jaji Kamana aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 15, mwaka huu, kwa ajili ya hukumu.

Awali, ilidaiwa kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 19, 2017 katika Kijiji cha Nyashimba Wilaya ya Mboghwe mkoa wa Geita, kwa mshtakiwa kumuua Mbula Mbweso kwa kumcharanga mapanga kichwani na shingoni hatimaye kufariki dunia, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

HABARI KIMATAIFA

## Russia yailaani Ujerumani

**MOSCOW, Russia**

RUSSIA imesema kuwa kitendo cha Bunge la Ujerumani cha kuchukua uamuzi wa kuitambua janga la njaa ya Holodomor iliyoikumba Ukraine miaka 1932 hadi 1933 kama mauaji ya halaiki yaliyoendeshwa na Utawala wa Kisovieti, ni uchochezi dhidi yake.

Pia ilisema uamuzi huo ni jaribio la Ujerumani kufuta historia yake ya Unazi.

Mnamo Novemba mwaka 1932, kiongozi wa muungano wa Soviet wakati huo Josef Stalin, chini ya sheria ya kujumuisha mali kwa serikali, aliwatuma polisi kuwapokonya raia wa Ukraine nafaka, mifugo, mashamba na hata mbegu za mazao.

Mamilioni ya wakulima wa Ukraine walikufa kwa njaa katika miezi iliyofuata kwa kile wanahistoria wanasema ni mauaji ya watu wengi na ya kudhamiria.

Russia imekataa madai kwamba hayo yalikuwa mauaji ya halaiki na kusema mamilioni ya watu katika maeneo mengine ya uliyokuwa Umoja wa KiSoviet ikiwa ni pamoja na Russia pia waliteseka na njaa hiyo.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky aliisifu hatua hiyo ya bunge la Ujerumani.

*DW*

## WHO yabaini maambukizi yaongezeka barani Ulaya

**BERLIN, Ujerumani**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) pamoja na ofisi ya shirika hilo katika Umoja wa Ulaya yamesema kuna watu zaidi wanaishi na virusi vya UKIMWI barani Ulaya, bila ya kupimwa wala kugundulika.

Kwa mujibu wa WHO, mwaka 2021, takribani watu 300 waligundulika kuwa na VVU kila siku katika nchi 46 kati ya 53 za Ulaya.

Ripoti hiyo inaonyesha pia kuwa bado kuna unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, na kwamba suala hilo linapaswa kukemewa.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO barani Ulaya, Hans Kluge alisema wanapaswa kuwa na wasiwasi mkubwa kutokana na takwimu za upimaji wa VVU, matibabu na huduma. Kluge alisema kuendelea kuenea kwa unyanyapaa dhidi ya VVU kunawazuia watu kupima na kunawafanya wasifikie lengo lao la mwaka 2030 la kuumaliza kabisa ugonjwa wa UKIMWI.

*DW*

# Kagame amjia juu Tshisekedi kutaka huruma ya wananchi

**KIGALI, Rwanda**

RAIS wa Rwanda Paul Kagame, amemshutumu kiongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kujaribu kutafuta njia ya kuahirisha uchaguzi ujao kwa kuihusisha Rwanda katika mgogoro wa mashariki mwa Congo.

Hata hivyo, serikali ya DRC haijajibu kauli ya Kagame ambaye bila kuthibitisha alisema rais wa Congo hakushinda uchaguzi wa kwanza.

Katika hotuba yake ndefu ya nadra ya siku ya Alhamisi katika Bunge la Rwanda, Rais Kagame alisema ni aibu kwamba vyama vingi na nchi zinadai kutaka kutatua tatizo hilo, lakini hazijapata suluhu kwa miongo kadhaa.

Kagame alizionya nchi zenye nguvu, akitaja Marekani, Uingereza, Ufaransa, na Umoja wa Mataifa kwa kushutumu au kuamini kwamba Rwanda ndiyo inayohusika na machafuko mashariki mwa Congo, huku akishutumu vikosi vya Umoja wa Mataifa kwa kushindwa kulitokomeza kundi la waasi la Rwanda la FDLR na wengine.

Pia alikanusha madai kwamba Rwanda ilikuwa ikiiba madini kutoka DRC,

"kitu kimoja ambacho sisi sio, sisi sio wezi" alisema.

Alisema madini mengi ya Congo yalisafirishwa kwa magendo au kupitia njia sahihi kupitia Rwanda hadi Dubai, Brussels, au Tel Aviv na Urusi.

"Wanatutuhumu kwa kuiba madini ya Congo vipi kuhusu sehemu yalikowasilishwa? " alihoji.

Kagame alisema Rwanda haiko katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kwamba waasi wa M23 sio Wanyarwanda bali ni Wacongo, akilaumu uasi wao kwa serikali ya Kinshasa kwa kutoheshimu makubaliano ya awali na kundi hilo.

Kwa kuihusisha Rwanda, Kagame alimshutumu Tshisekedi, kwamba alikuwa akitengeneza visingizio vya dharura ili uchaguzi mwaka ujao usifanyike.

"Sawa, si kwamba alishinda uchaguzi wa kwanza kama tunavyojua, kama anajaribu kutafuta njia nyingine ya kuahirisha uchaguzi ujao basi ni afadhali atumie visingizio vingine sio sisi", aliongeza bila kuwasilisha ukweli wa madai yake.

Kiongozi huyo alisema Rwanda inaweza kusaidia katika kushughulikia tatizo la M23 na makundi mengine ya waasi mashariki mwa Congo kwa sababu ina nia ya kuwa na ujirani mwema.

*BBC*



Treni ya mvuke ya Father Frost, ambayo husafiri nchini kote Russia kabla ya msimu wa sikukuu ya Mwaka Mpya na Krismasi, ilipowasili katika kituo cha Omsk juzi. **PICHA: REUTERS**

# Rais Ramaphosa atuhumiwa utesaji, kuwahonga wezi

**CAPETOWN, Afrika Kusini**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, anakabiliwa na tishio la kuondolewa madarakani kwa kura ya kutokuwa na imani naye kutokana na kashfa ya kuwahonga wezi.

Rais ameshutumiwa kwa kuficha wizi wa dola milioni 4 kutoka shambani kwake mnamo 2020, ikiwa ni pamoja na utekaji nyara na kuwahonga wezi hao ili wanyamaze kimya.

Ripoti iliyofichuliwa kutoka kwa jopo huru imegundua kuwa Ramaphosa alitumia vibaya nafasi yake na huenda alivunja sheria ya kupambana na ufisadi.

Hata hivyo, rais huyo amekana kufanya makosa, na kusema pesa hizo zilitokana na kuuza nyati ambao wanafugwa shambani kwake.

Matokeo ya uchunguzi huo yamekabidhiwa bunge ambalo linatazamiwa kuyachunguza na kuamua iwapo litaanzisha mchakato wa kujadiliwa kwa hoja hiyo.

Rais Ramaphosa amebakiza mwezi mmoja kabla ya kongamano litakaloamua iwapo anaweza kuwania muhula wa pili na chama chake, African National Congress (ANC), mwaka wa 2024.

Tukio hilo linaweza kuwa baya katika hatma yake akiwania wadhifa huo.

ANC itafanya mkutano na watendaji wake siku ya Alhamisi, inatarajiwa kuwa suala hilo litajadiliwa.

Kashfa ya Farmgate ilizuka mwezi Juni, wakati mkuu wa zamani wa ujasusi wa Afrika Kusini, Arthur Fraser, alipowasilisha malalamiko kwa polisi akimshtumu kiongozi huyo kwa kuficha wizi wa pesa hizo kutoka shamba lake la Phala Phala lililoko kaskazini-mashariki mwa nchi hiyo mnamo 2020.

Fraser, ambaye ni mshirika wa karibu wa Rais wa zamani Jacob Zuma, alidai kuwa pesa hizo zingeweza kuwa mapato ya utakatishaji fedha na ufisadi, na kumshutumu rais kwa kuwateka nyara na kuwahonga wezi hao.

Kushikilia kiasi hicho kikubwa cha fedha kunaweza kukiuka sheria za udhibiti wa fedha za kigeni.

Ramaphosa amethibitisha kuwepo kwa wizi, lakini alisema kiasi kilichoibiwa kilikuwa kidogo kuliko kile kinachodaiwa, na akakana kujaribu kuficha.

*BBC*

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SETHI SIGA KAGIZE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye usajili namba **T121 DFX , CHASSIS NAMBA: SCP13Q0009335** na **ENGNE NAMBA:2SZEAA9335** . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/327407/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KEEY WAY MOTOR TANZANIA LIMITED ANATANGAZA** KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI CHASSIS NAMBA **IBBPEK9H81BB79821** ENGINE NAMBA **QJ162FMJ2B0240203.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI**
**MBE/MBE/RB/461533/2022**

## KUPOTEA KWA PASPOTI YA KUSAFIRIA



**NICO PIUSI MLASU** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 358614** iliyotolewa **DAR ES SALAAM PCO** septemba mwaka **2020.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**TAARIFA POLISI : RUJ/TR/RB/62/2022**

## KUPOTEA KWA PASPOTI YA KUSAFIRIA



**ERIC KASIRA MGALLA** anatangaza kupotea kwa paspoti ya kusafiria yenye namba **TAE 459205** iliyotolewa **DAR ES SALAAM PCO** Machi mwaka **2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**TAARIFA POLISI: KIG/RB/632/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi na 233|2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MUHAMED ATHUMANI YAKUBU**
**KATIKA SAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIOLETWA NA SHAFII ALLY NURU**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa
Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 6 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetotewa leo tarehe 28 Mwezi 11 mwaka 2022

WHITEMIRACLES (T) LIMITED

*02-12-2022*

## NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) /TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MTEJA WETU **FIKIA FINANCE LTD** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA MDAIWA, MNADA UTAFANYIKA MAHALI DHAMANA ILIPO KAMA INAVYOONESHWA KWENYE JEDWALI HAPO CHINI, TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA TANGAZO HILI AMBAYO NI 2-12-2022

| JINA LA MKOPAJI | DHAMANA MAHLI ILIPO | TAREHE YA MNADA | AINA YA DHAMANA |
|---|---|---|---|
| **SEBASTIAN WESTON KYENGULA** P.O.BOX 308 MAFINGA, TANZANIA | WHITEMIRACLES (T)LIMITED OFISINI P.O.BOX 12744, PLOT NO 3D BULDING, MAGOMENI, USALAMA DAR ES SALAAM, TANZANIA | 17-12-2022 KUANZIA SAA NNE NA KUENDELEA | GARI NAMBARI **T616 DZM**, TOYOTA CROWN RANGI NYEUPE |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA SIKU HIYO HIYO ASILIMIA 25% YA BEI
2. ASILIMIA 75% ITALAZIMIKA KULIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14)
3. ENDAPO MNUNUZI ATASHIDWA KULIPA 75% ATAPOTEZA MALIPO YAKE YA AWALI YA 25% NA MNADA UTARUDIWA TENA

**KWA MAELEZO ZAIDI PIGA NAMBARI 0684-937-219 / 0754-916-444**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 31/2022**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 41/2021, Mahakama ya Wilaya Chunya)**
**JAMHURI................................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JUMA TANGANYIKA.........................MJIBU RUFAA**

KWA BWANA: **JUMA TANGANYIKA**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe **20/12/2022** siku ya Jumatatu saa **3.00** asubuhi bila kukosa.
**ELEWA KWAMBA,** ukikosa kufika Mahakamani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **07/11/2022**

NAIBU MSAJI MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 61/2022**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 158/2021, Mahakama ya Wilaya Chunya)**
**JAMHURI................................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**OBED MWANIJEMBE LAZARO...............MJIBU RUFAA**

KWA BWANA: **OBED MWANIJEMBE LAZARO**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe **05/12/2022** siku ya Jumatatu saa **3.00** asubuhi bila kukosa.
**ELEWA KWAMBA,** ukikosa kufika Mahakamani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **21/11/2022**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

OFISI ZA MATANGAZO,
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB:
+255 - 0782253676

Uza, Chenye
Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI

# HARMONIZE KUELEZEA BANGI



NYOTA wa Bongofleva, Rajab Kahali maarufu kama Harmonize amesema atatunga wimbo kuhusu bangi.

Harmonize ambaye kwa muda mrefu amekuwa wazi kuhusu mapenzi yake kwa bangi ameahidi kuachia wimbo unaohusu mihadarati hiyo haramu kabla ya mwisho wa mwezi huu.

"Desemba hii, nisipotengeneza wimbo kuhusu bangi .. nipigeni risasi," alisema kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Aliambatanisha ujumbe wake na emoji ya kikohozi, ambacho huwa anatumia kama utambulisho wake katika nyimbo zake nyingi.

Kikohozi pia huhusishwa na matumizi ya bangi kwani watumiaji wengi hukipata wakikohoa baada ya kuvuta.

Konde Boy kwa kawaida huwa hafichi kwamba yeye ni mtumiaji wa mihadarati hiyo.

Katika video za nyimbo zake nyingi ameonekana akivuta kinachoaminika kuwa bangi. Pia amewahi kurekodi video zingine nyingi akivuta.

Bosi huyo wa Konde Music Worldwide pia ametangaza ataanza kutoza milioni 100 ili kufanya collabo na wasanii wengine.

"Naanza kutoza kwa collabo, TZS 100M. Sharti ngoma iwe kali. Siwezi kusubiri kumtoza mtu fulani TZS 500," alisema.

# KANYE WEST KUMLIPA KIM

KANYE West ametakiwa kumlipa, Kim Kardashian, Dola za Marekani 200,000 kwa mwezi kama matunzo ya watoto katika makubaliano ya talaka.

Rapa huyo wa zamani na nyota wa televisheni atashiriki malezi ya pamoja ya watoto wao wanne.

Kardashian aliomba talaka mnamo 2021, baada ya miaka minane na West, ambaye amebadilisha jina lake kihalali na kuwa Ye.

Hii inakuja wiki chache tu baada ya kampuni kadhaa kukata uhusiano na Ye juu ya maoni ya chuki.

Masuala kuhusu mgawanyo wa mali na malezi ya watoto wao yalitatuliwa katika hati za mahakama zilizowasilishwa mapema wiki hii.

Pande hizo mbili zinapaswa kushauriana na kila mmoja juu ya uamuzi kuhusu ustawi wa watoto wao, nyaraka zinasema.

Gharama za usalama wa watoto, shule na chuo zitagawanywa kwa wazazi hao wawili.

Kwa kuongeza, Ye anatarajiwa kulipa kiasi hicho cha fedha kwa mwezi kama msaada wa watoto - ambayo New York Post iliripoti ni kwa sababu watatumia muda wao mwingi na Kardashian.

Katika taarifa kadhaa zilizowasilishwa hapo awali, Kardashian mwenye miaka 42, alisema "alitaka sana" ndoa hiyo ivunjwe, akiongeza "itamsaidia Kanye kukubali" kwamba uhusiano huo umekamilika.

Ye mwenye miaka 45 amekumbana na utata katika miezi ya hivi karibuni, na ameachwa na kampuni kadhaa, zikiwamo Adidas, Gap na Balenciaga.

Rapa huyo alizua shutuma nyingi mapema mwaka huu baada ya kuhudhuria Wiki ya Mitindo ya Paris akiwa amevalia t-shirt yenye kauli mbiu ya "White Lives Matter" - msemo unaotumiwa mara nyingi na watu weupe.

Kisha alidai wakosoaji wake walikuwa wanalipwa na kikundi cha siri cha watu wa Kiyahudi, kikundi cha kawaida cha kupinga Uyahudi.



# MOBETTO
## AFICHUA BABA WA MTOTO WAKE

MSANII Hamisa Mobetto amemsuta mtangazaji wa radio hapa nchini, Mpoki Mjuni, aliyedai mtoto wa kiume wa video queen huyo si wa Diamond Platnumz.

Mpoki alisema mtoto wa Mobetto, Dylan si wa bosi huyo wa WCB bali ni Billnass.

Mobetto alikereka na madai hayo na kuandika kwenye instagram ni mwanamke tu anayefahamu baba ya mtoto wake.

"Yaani sipendi mtu amzungumzie mtoto wangu!! Sipendi!!Sipendi na sipendi tena jamani. Na wala sijawahi elewa watu wazima wanakaaje chini wanaanza kumzungumzia mtoto wa miaka mitano ni kama walikuwapo nikijifungua. Binadamu mkoje nyinyi, au mnataka nini haswaa niwasaidie?!" Mama huyo wa watoto wawili aliandika.

Aliwaomba watu kuacha kumhusisha Dylan kwa mambo yake kwani hawajawahi kukutana naye.

Mobetto aliwaambia watu wamzungumzie yeye iwapo wana jambo linalowatatiza kumhusu ila wasimhusishe mwanawe.

"Sidhani kama nimewahi kumwomba mtu yeyote msaada wa kulea watoto wangu. Sipendi kero na mtu na mimi si mtu wa kuropoka, chonde chonde tusije onana wabaya. Yaani mmekosa vya kuongea au ni nini.

"Yaani mtoto wangu nyie ndio mumpangie baba? Nyie kama nani haswa?! Binadamu mnapenda sana kujipa mamlaka kwenye maisha ya watu wasiowahusu!" Aliendelea.

Mpoki alikuwa amemzungumzia Mobetto huku akijaribu kuficha jina lake ila alitaja mambo yaliyomhusisha mwanamuziki huyo.

"Kuna msichana anajulikana sana hapa Tanzania, ana followers wengi, ni zaidi ya milioni tisa. Alikuwa video vixen, akapata mtoto wa kiume, ana watoto wawili, wa kwanza wa kike. Kuna jamaa mmoja hapa alitoa wimbo ukavuma sana, naye alikuwa video vixen kwenye huo wimbo. Sasa alipojifungua, hadi kwenye Instagram akaweka jina la huyo jamaa. Jamaa akakubali, akampa hadi jina, hadi walienda mahakamani ," Mpoki alisema.

Alisema Dylan anafanana na Billnass masikio, mdomo, nyusi, komwe na hata macho.

# AZAM YAANZISHA MSAKO POINTI TISA LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

AZAM FC imedhamiria kuvuna pointi tisa za ugenini katika michezo yake mitatu inayofuata na kutimiza malengo ya kushinda mechi 10 za awali katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mechi hizo haijalishi wanacheza nyumbani au ugenini, imeelezwa.**

Matajiri hao wa Chamazi walipata ushindi katika mechi zake saba mfululizo kuanzia walipoifunga Simba bao 1-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Azam FC itashuka tena dimbani Desemba 5, mwaka huu kuvaana na Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema wachezaji wao walipewa mapumziko ya siku chache na sasa wamerejea kuendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi dhidi ya Maafande hao.

Ibwe alisema malengo yao ni kuvuna pointi tatu na kutimiza malengo na mipango ya kushinda mechi 10 mfululizo.

"Tayari tumefanikiwa kushinda michezo saba, sasa malengo yetu na nguvu ni kutafuta pointi tisa katika michezo mitatu iliyosalia kati ya saba ambayo tayari tumekusanya pointi 21, mechi tatu zilizosalia ni kumfunga Polisi Tanzania siku ya Jumatatu na kurejea nyumbani na alama tatu.

Baada ya mechi yetu na Polisi Tanzania tutarejea nyumbani kwa ajili ya mchezo wetu wa hatua ya pili ya Kombe la Shirikisho la Azam dhidi ya Maliamo FC, katika mchezo huo pia tunahitaji ushindi ili kufikia yale malengo yetu ya kutwaa kombe hilo," alisema Ibwe.

Aliongeza baada ya hapo wataendelea kujipanga kwa ajili ya michezo miwili ya ugenini kwa kuwakabili Kagera Sugar ifikapo Desemba 16, mwaka huu na siku tano baadaye itawavaa Geita Gold FC.

Aliongeza wamejipanga kukutana na ushindani hasa katika mechi za ugenini ambapo kila timu wanayokutana nayo inahitaji kubakisha pointi zake nyumbani.

Azam FC yenye pointi 32 iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo nyuma ya vinara Yanga yenye kiporo cha mechi moja wakati Simba yenye pointi 31 iko katika nafasi ya tatu.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mipeko iliyoko katika Wilaya ya Mkuranga, Pwani, wakionyesha vipaji vya kucheza muziki katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani (ngazi ya kata), yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# JKU, Jamhuri dimbani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

RAUNDI ya 15 Ligi Kuu Zanzibar inatarajia kuanza leo kwa JKU kuwakaribisha Jamhuri kutoka Pemba huku usiku Dulla Boys ikiwavaa KVZ, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Amaan.

Baada ya raundi hiyo kukamilika, tayari mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ya juu Zanzibar utakuwa umemalizika na kusimama kwa muda kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa JKU, Sheha Khamis, alisema timu yake imejipanga vizuri kusaka ushindi katika mchezo huo na kumalizika mzunguko wa kwanza kwa furaha.

Khamis alisema anajua anacheza na timu ngumu ambayo katika msimu huu pia imejipanga kurejesha heshima yake waliyokuwa nayo miaka ya nyuma na hivyo wachezaji wake watajilinda zaidi. "Licha ya timu yao kupitia kipindi cha misukosuko kwa kupoteza mechi mfululizo lakini hivi sasa imerejea katika kasi yake na anaamini atashinda mchezo huo kama ilivyo mipango yake," alisema Khamis.

Kocha huyo aliongeza msimu huu hakuna mechi rahisi kwa sababu kila timu inahitaji kupata zawadi na vile vile kila mchezaji anahitaji kujituma ili apate nafasi ya kuitwa kwenye timu ya taifa.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU ipo kwenye nafasi ya nane ikiwa na pointi 21 sawa na wapinzani wao Jamhuri ambao wenyewe wapo katika nafasi ya tisa.

## Ihefu SC, Kagera Sugar kibaruani

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi chake kikijiandaa kuivaa Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo, Kocha Mkuu wa Ihefu SC, Juma Mwambusi, amesema anahitaji kusajili wachezaji wapya wawili ili kuiongezea nguvu timu yake.

Mwambusi aliliambia gazeti hili nyota hao wapya wakipatikana wataziba nafasi ya ushambuliaji na umaliziaji ambazo zimeonekana kuwa na mapungufu msimu huu.

"Safu ya umaliziaji ina mapungufu, mara nyingi wachezaji wangu wanapata mipira lakini wanashindwa kufunga, inanipasa nifanye usajili mzuri ili kuhimili ushindani," alisema Mwambusi.

Kocha huyo alisema mastraika wake wanakosa utulivu wanapofika katika lango la wapinzani na kupelekea kupoteza michezo iliyopita ya ligi hiyo.

Aliongeza amejipanga vizuri kuwakabili Kagera Sugar na anaamini wachezaji wake wataendelea kujituma kusaka ushindi na kujiondoa kwenye nafasi waliyopo kwenye msimamo.

## Kumekucha semina ya Shotokan Karate Dar

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Kimataifa la Shotokan Karate linatarajia kuendelesha semina ya mafunzo ya mchezo huo itakayofanyika kuanzia leo hapa jijini, Dar es Salaam, imefahamika.

Mafunzo hayo yataongozwa na Rais wa West Coast Shotokan Karate (W.C.S.K.K.A.I na W.F.K.O) na Mkufunzi wa Kimataifa, Shihan Shalom Avitan, kutoka Israel ambaye aliendesha semina nyingine huko Zanzibar.

Mwenyekiti wa West Coast Shotokan Karate Tanzania, Anastasius Liwewa, alisema maandalizi ya semina hiyo yamekamilika na imepangwa kufanyika kwenye Ukumbi wa Starlight Arena uliopo Masaki.

"Mafunzo hayo yatajumuisha washiriki kutoka mataifa manne, (Zambia, Zimbabwe, Jordan na Kenya), ambao tayari wako Dar es Salaam kusubiri semina hiyo itakayoambatana na mitihani ya kupanda daraja," alisema Liwewa ambaye yuko daraja la tano.

Aliongeza lengo kubwa la kutoa mafunzo hayo ni kuendelea kuutangaza mchezo huo na kuhakikisha unakuwa sehemu ya mipango ya serikali katika kuwapa vijana fursa ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALDO MKWANJA MNONO**

CRISTIANO Ronaldo mwenye miaka 37, amepokea ofa kutoka kwa klabu ya Al-Nassr FC ya Saudi Arabia baada ya kuondoka Manchester United, ambayo itamfanya apate pauni milioni 150 kwa msimu. ***(Telegraph)***

**RONALDO BADO HAJAAMUA**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristian Ronaldo, inadhaniwa bado anataka kucheza soka la Ligi ya Mabingwa Ulaya na bado hajakubali kutoka kwa klabu ya Saudi Arabia. ***(Mail)***

**GAKPO ATAKUWA UNITED**

KLABU ya Manchester United inawasiliana na mawakala wa PSV Eindhoven na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Cody Gakpo, kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ifikapo Januari. ***(Fabrizio Romano)***

**GILMOUR NJIA MOJA**

KIUNGO wa kati wa Brighton na Timu ya Taifa ya Scotland, Billy Gilmour mwenye miaka 21 anaweza kuhamia Villarreal kwa mkataba wa mkopo ifikapo Januari. ***(Times)***

**BUSQUETS KUONDOKA BARCA**

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Busquets mwenye miaka 34 ana nia ya kujiunga na Inter Miami ya Marekani mara baada ya mkataba wake wa Barcelona utakapomalizika ifikapo Juni, mwakani. ***(Mirror)***

**HATIMA YA BALE FEBRUARI**

MSHAMBULIAJI wa Los Angeles FC, Gareth Bale, mwenye umri wa miaka 33, atafanya uamuzi kuhusu mustakabali wa klabu yake ifikapo Februari, mwakani baada ya kuwaambia Wales yuko tayari kuendelea kucheza nao. ***(Mirror)***

**MISLINTAT ANUKIA ARSENAL**

LIVERPOOL inamtaka aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Ajira ya Arsenal, Sven Mislintat, ambaye alifanya kazi na Jurgen Klopp, katika klabu ya Borussia Dortmund, kama mgombea wa kuchukua nafasi ya Julian Ward kuwa mkurugenzi wa michezo huko Anfield. ***(Sky Sports Germany)***

**JESSIE AIGOMEA MILAN**

WAKALA wa kiungo wa kati wa Ivory Coast Franck Kessie, ambaye alihama kutoka AC Milan kwenda Barcelona Julai, mwaka huu amekataa uwezekano wa kurejea Italia huku kukiwa na ripoti za Inter Milan kuwasilisha ombi la kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Calciomercato)***

**KINDA WYLIE AGOMBEWA**

KLABU ya Machester United imeungana na Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Scotland, Jack Wylie, mwenye umri wa miaka 15 kutoka Rangers. ***(Mirror)***

**KUDUS ATAJWA BARCA**

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Jordi Cruyff, amesema miamba hao wa Hispania wamekuwa wakimfuatilia kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ghana na Ajax, Mohammed Kudus, mwenye miaka 22. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AWAPIGIA SALUTI WENZAKE

●●● Asema sasa wachezaji wa Argentina wameimarika na kutahadharisha...

**DOHA, Qatar**

LIONEL Messi aliwasifia wachezaji wenzake wa Argentina, akisisitiza "wameimarika" kufuatia kukosa penalti na kupata ushindi wao muhimu wa 2-0 wa Kombe la Dunia dhidi ya Poland, Jumatano.

Kikosi cha Kocha, Lionel Scaloni, kilikata tiketi ya kuingia hatua ya 16 bora, baada ya kipa, Wojciech Szczesny kuokoa penalti, lakini wakapata mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Alexis Mac Allister na Julian Alvarez na kuwafanya wamalize wakiwa kinara katika Kundi C.

La Albiceleste hao ambao walipata kichapo cha kushangaza cha mabao 2-1 kutoka kwa Saudi Arabia katika mechi yao ya kwanza, sasa wamefuzu kwa hatua ya mtoano ya Kombe la Dunia kwa mara ya 13 na watacheza na washindi wa pili wa Kundi D ambao ni Australia hapo Jumapili.

"Timu ilitoka kwa nguvu baada ya kosa langu hilo," alisema Messi, ambaye alimzidi Diego Maradona kwa kuichezea Argentina mechi nyingi zaidi za Kombe la Dunia (22).

"Tulifahamu goli la kwanza likiingia ndio litabadilisha mchezo, mchezo uliopita ulitupa utulivu mkubwa na tukatoka uwanjani tukifikiria tushinde.

"Mchezo na Australia utakuwa mgumu sana. Mtu yeyote atashinda, kila kitu ni sawa. Tunapaswa kujiandaa kwa mchezo kwa njia bora tunayofanya kila wakati.

"Lazima tuwe watulivu na kwenda mchezo baada ya mchezo. Sasa, kombe lingine la Dunia linaanza, na tunatumani tunaweza kuendelea kudumisha kile tulichofanya leo (juzi)."

Nicolas Otamendi alikubaliana: "Hii ni timu ambayo inaimarika chini ya shinikizo, ilionyeshwa. Leo (juzi) tulikuwa na fainali, na hatukupoteza mwelekeo kamwe."

Huku Rodrigo De Paul akipongeza "utu" ulioonyeshwa na kikosi, Mac Allister anaamini uchezaji wao utaongeza imani yao kuelekea hatua ya mtoano.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,054,9
MECHI KALI
SINGIDA BS FC
VERSUS
NAMUNGO
1 | 2.04
X | 2.92
2 | 3.74
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MENDES AIPA PIGO URENO



**DOHA, Qatar**

MLINZI wa Ureno, Nuno Mendes, atakuwa nje kwa muda wa miezi miwili ijayo baada ya kuumia paja kwenye mchezo wao wa Kombe la Dunia ambapo timu yake ilikuwa ikiumana dhidi ya Uruguay.

Mechi hiyo iliisha kwa Ureno kuitwanga Uruguay mabao 2-0, na kujihakikishia nafasi ya kufuzu kwa hatua ya 16 bora kwenye michuano hii ya Kombe la Dunia.

Ripoti zinasema Nuno atabakia na timu hadi mwisho wa Kombe la Dunia kwani madaktari wa PSG watamtembelea Qatar hataweza kucheza michezo yote iliyosalia na atakuwa nje hadi Januari, 2023.

Mendes mwenye umri wa miaka 20 amekuwa na kiwango bora kabisa katika michuano hii amepata jeraha la paja na hataweza kupona kwa haraka hivyo timu ya Ureno imeamua kumuondoa kwenye kikosi moja kwa moja ili akafanyiwe matibabu.

Mechi ya mwisho ya Ureno itakuwa ni dhidi ya Korea Kaskazini ambapo timu hiyo ya Son Heung min ndio itakuwa ikihitaji sana kupata

# Senegal wanachunguzwa na FIFA

**DOHA, Qatar**

WAWAKILISHI wa Afrika, Senegal wamejitupa katika 'maji moto' kabla ya mechi yao dhidi ya kikosi cha England kilichoko chini ya Kocha Mkuu, Gareth Southgate kwa kutofuata kanuni za Kombe la Dunia.

Kabla ya mechi yao na Ecuador siku ya Jumanne, Kocha wa Senegal, Aliou Cisse, alihudhuria mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mechi bila mchezaji wake mmoja.

Sheria za FIFA zinasema lazima anatakiwa aambatane na mtu kutoka kwenye kikosi chake, katika vyumba vya mkutano na waandishi wa habari katika kituo kikuu cha habari huko Doha.

Lakini Cisse alichagua kuzungumza na vyombo vya habari akiwa peke yake mapema wiki hii, huku FIFA ikisema hatua sasa itachukuliwa dhidi ya FA ya Senegal.

Taarifa iliyotoka mapema jana ilisomeka: "Kamati ya Nidhamu ya FIFA imefungua kesi dhidi ya Shirikisho la Soka la Senegal kutokana na uwezekano wa ukiukaji wa kifungu cha 44 cha kanuni za Kombe la Dunia la FIFA Qatar 2022, kifungu cha 2.7.2 cha kanuni za vyombo vya habari na masoko na kifungu cha 8.5.3 cha mwongozo wa timu.

"Ukiukaji unaowezekana unahusiana na mkutano wa lazima wa waandishi wa habari ambao ulifanyika Novemba 28 kabla ya mechi ya Ecuador dhidi ya Senegal Kombe la Dunia la FIFA."

Kuna uwezekano mkubwa kwamba Senegal itapewa faini ya kuilipa paundi 8,800 kwa kosa hilo.

938,985/-

# TWANGA PEPETA KUZINDUA ALBAMU MPYA DESEMBA 17

**Na Mwandishi Wetu**



BENDI kongwe ya muziki wa dansi nchini, African Stars maarufu Twanga Pepeta imepanga kufanya onyesho la uzinduzi wa albamu yake ya 15 ifikapo Desemba 17, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Gwambina Lounge ulioko Chang'ombe, Dar es Salaam.

Kiongozi Mkuu wa Twanga Pepeta, Lwiza Mbutu, alisema uzinduzi huo umepewa jina la Twanga Pepeta Forever na unatarajiwa kuwa wa aina yake.

Mbutu alisema siku hiyo mbali ya kutambulisha nyimbo zao mpya tano, wamepanga kufanya shoo ya kiwango cha juu akiweka wazi wacheza shoo wamejipanga imara lakini pia watafanya utambulisho wa wanamuziki chipukizi wenye vipaji.

Alizitaja baadhi ya nyimbo zilizoko katika albamu hiyo mpya ni pamoja na Shobo, Dr Rubi, Chombo ya Fundi na Mmbeya.

Alisema maandalizi ya onyesho hilo linalotarajiwa kuwa la kihistoria kuwahi kutokea hapa nchini yamekamilika.

"Lengo la onyesho hilo ni kuonyesha mapitio waliyopitia tangu kuanzishwa kwa bendi miaka 24 iliyopita na tulipo sasa, kuna maingizo ya wanamuziki kibao chipukizi ambao ndiyo nguzo ya bendi hii kwa hivi sasa.

"Kabla ya onyesho hilo, tutafanya onyesho maalum la kuwaonyesha wadau wetu nini tumekifanya na tunachotarajia kukifanya. Onyesho hili maarufu kwa jina la 'Listening Party' itakayofanyisha Desemba 6, mwaka huu kwenye Ukimbi wa Meridian Lounge, " aliongeza Mbutu.

Naye Kiongozi Msaidizi wa bendi hiyo, Msafiri Saidi (Msafiri Diouf), alisema wamefanya mabadiliko makubwa katika muziki wao na kuweka vionjo vya kisasa ambavyo siku ya utambulisho mashabiki wao watavisikia kwa mara ya kwanza.

"Bendi kwa sasa imepanua wigo wake kwa kuchanganya damu kongwe na changa. Hii damu changa ni muhimu kwa maendeleo ya bendi kwani sisi sasa tunakuwa nyuma ya wanamuziki ho," alisema Diouf.

Mwenyekiti wa bendi hiyo, Asha Baraka, alisema wamejiandaa vyema na wameamua kufanya mambo yao kisasa zaidi.

"Wigo wa bendi umekuwa mkubwa sana ambapo kwa sasa tuna mashabiki ndani na nje ya nchi, hivyo tumeamua kwenda kisasa zaidi na mashabiki wetu watarajie mambo makubwa zaidi," alisema Asha.

# Yanga kufurahia

INATOKA UK. 32

mapato ya mlangoni, ndiyo maana unaona timu inaweza kuwa na makazi Dar es Salaam, lakini ikapeleka mechi yake Kigoma, inachotaka ni kupata mashabiki wengi kwa sababu mikoani watu wengi wanajazana viwanjani kuziona timu kubwa, pointi tatu huwa ni lengo lao la pili," alisema kiongozi huyo.

Aliwataja wachezaji walikosekana katika mechi hiyo ambao ni Bernard Morrison na Feisal Salum 'Fei Toto' tayari wameshapona na wanachofanya sasa ni kufanya mazoezi ya utimamu wa mwili, ili warejee kwenye majukumu yao baada ya ripoti ya madaktari kuwaruhusu.

"Wale waliodhania baada ya kufungwa tutachanganyikiwa au wamepata pa kusemea wanajidanganya, tunakwenda kufanya sherehe kwa ajili ya kucheza mechi 49 bila kupoteza. Tuna sababu ya kujivunia, tuna sababu ya kusherehekea. Kutakuwa na keki siku ya Jumapili kwenye mechi dhidi ya Prisons, kutakuwa na wasanii watakaotumbuiza," Kamwe aliongeza.

Mara ya mwisho Yanga kupoteza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa Aprili 25, mwaka jana na ilichapwa bao 1-0 na Azam FC.

Viungo wa Never Tegere na Lenny Kissu wa Ihefu ndiyo waliohitimisha 'unbeaten' hiyo.

# SIMBA: TUTARUDI

INATOKA UK. 32

amini ya sisi kurejea kileleni yamerudi. Tuliwapa furaha baada ya kuifunga Polisi Tanzania, tunataka furaha hiyo iendelee, tunahitaji kuendeleza ushindi huu, tunatakiwa kujituma na kujitoa," aliongeza kiongozi huyo.

Alisema pia taarifa njema ndani ya kikosi chao ni kuimarika afya kwa baadhi ya wachezaji waliokuwa majeruhi wakiwamo, Jimmyson Mwanuke na Mohammed Hussein (Zimbwe Jr).

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kimefika salama Tanga na wanatarajia kuendelea na mazoezi kwa ajili ya kukamilisha kazi iliyowapeleka.

Rweyemamu alisema wanatambua mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu Coastal Union walipoteza mchezo uliopita wakiwa kwenye uwanja na hivyo wataingia kurekebisha makosa.

"Kila mechi ni ngumu kwetu, tunajua kila timu inazihitaji pointi ili kujiimarisha, walifungwa mechi iliyopita, haitakuwa rahisi tena kupoteza, watapambana kutafuta pointi lakini pia kuwapa furaha mashabiki wao," alisema Rweyemamu.

Wakati huo huo, Kagera Sugar inatarajia kuikaribisha Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba wakati Singida Big Stars itawaalika Namungo FC kutoka mkoani Lindi.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 03/12/22 | 18:00 | Accrington vs Oxford Utd | 3.08 | 3.42 | 2.23 |
| 2. 03/12/22 | 18:00 | Northampton vs Tranmere | 2.25 | 3.18 | 3.28 |
| 3. 03/12/22 | 18:00 | Cove Rangers vs Partick Thistle | 2.78 | 3.53 | 2.37 |
| 4. 03/12/22 | 18:00 | Arbroath vs Morton | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 5. 03/12/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Erzurum BB | 2.30 | 3.48 | 2.88 |
| 6. 03/12/22 | 20:00 | Cagliari vs Parma FC | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 7. 03/12/22 | 20:30 | Mirandes vs Albacete Balompie | 2.50 | 3.06 | 2.96 |
| 8. 03/12/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs Las Palmas UD | 2.64 | 3.04 | 2.79 |
| 9. 03/12/22 | 21:00 | Deportivo La Coruna vs Cordoba | 2.26 | 3.02 | 3.02 |
| 10. 03/12/22 | 23:00 | Villarreal B vs Leganes | 2.45 | 3.02 | 3.07 |
| 11. 04/12/22 | 13:30 | Manisa BBSK vs Keciorengucu | 2.34 | 3.46 | 2.82 |
| 12. 04/12/22 | 14:30 | Spal vs Modena | 2.33 | 3.12 | 3.17 |
| 13. 04/12/22 | 15:30 | Wycombe vs Portsmouth | 2.42 | 3.39 | 2.79 |
| 14. 04/12/22 | 16:00 | Adanaspor vs Goeztepe | 2.63 | 3.38 | 2.53 |
| 15. 04/12/22 | 17:00 | Sudtirol vs Frosinone | 3.37 | 3.03 | 2.28 |
| 16. 04/12/22 | 17:00 | Cosenza vs Perugia | 2.94 | 3.09 | 2.49 |
| 17. 04/12/22 | 17:00 | Brescia vs Reggio Calabria | 2.54 | 2.98 | 2.98 |


MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 02/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1175 | Shukura vs Metalurgi R | 1.31 | 4.86 | 7.58 |
| 12:30 | 2534 | Gareji vs FC Spaeri | 2.72 | 3.35 | 2.30 |
| 12:30 | 4854 | Merani Martvili vs WIT Georgia | 1.55 | 4.01 | 4.89 |
| 14:00 | 3632 | Churchill Brothers vs Aizawl FC | 2.17 | 3.25 | 3.01 |
| 14:00 | 4592 | Onduparaka FC vs Kampala City Council | 5.07 | 3.61 | 1.60 |
| 14:00 | 5293 | Chernomorets Odessa vs FC Kryvbas Kriviy Rih | 2.54 | 2.98 | 2.69 |
| 15:00 | 1794 | Kustosija vs Rudes Zagreb | 3.55 | 3.35 | 1.92 |
| 15:45 | 1653 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 3.19 | 2.85 | 2.44 |
| 15:45 | 5914 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.35 | 2.98 | 3.18 |
| 16:00 | 1771 | Express FC vs Dove All Stars | 2.27 | 2.92 | 3.16 |
| 16:00 | 2383 | Bul FC vs Wakiso Giants FC | 1.74 | 3.06 | 5.05 |
| 16:00 | 4573 | Singida BS FC vs Namungo | 2.04 | 2.92 | 3.74 |
| 16:30 | 3062 | UTA Arad vs Sepsi Osk | 3.77 | 3.03 | 2.06 |
| 17:00 | 5503 | Al-Bourj FC vs Al-Nejmeh | 2.44 | 2.83 | 2.97 |
| 17:30 | 1033 | Al Ahli Manama vs Al Hala Muharraq | 2.18 | 2.96 | 3.30 |
| 18:00 | 1130 | Ghana vs Uruguay | 4.52 | 3.66 | 1.74 |
| 18:00 | 5680 | South Korea vs Portugal | 4.60 | 3.95 | 1.67 |
| 18:30 | 2154 | Al Shabbab vs Manama Club | 4.10 | 3.32 | 1.80 |
| 20:00 | 1637 | Gasogi United vs APR FC | 3.65 | 2.95 | 2.18 |
| 20:00 | 2672 | Doxa Katokopia vs Akritas Chlorakas | 2.09 | 3.40 | 3.35 |
| 20:00 | 3591 | EN Paralimni vs AEK Larnaca | 5.38 | 3.84 | 1.60 |
| 20:00 | 4379 | Eyupspor vs Tuzlaspor | 1.46 | 4.17 | 5.63 |
| 20:00 | 5104 | Petrolul Ploiesti vs Universitatea Cluj | 2.53 | 2.97 | 2.87 |
| 20:00 | 5275 | Al Ahly Cairo vs Talaea El Gaish | 2.07 | 3.24 | 3.54 |
| 20:00 | 5310 | Neftchi Baku vs Karabakh | 4.38 | 3.70 | 1.66 |
| 20:00 | 5829 | Marines FC Gisenyi vs Mukura | 3.80 | 3.10 | 2.07 |
| 20:30 | 5826 | AL Khalidiyah vs East Riffa | 1.90 | 3.05 | 4.07 |
| 21:30 | 2039 | Concarneau vs Avranches | 1.48 | 4.15 | 5.92 |
| 21:30 | 2142 | Orleans vs Le Puy | 1.80 | 3.41 | 4.25 |
| 21:30 | 2582 | Bastia Borgo vs Red Star | 3.96 | 3.56 | 1.81 |
| 21:30 | 2994 | Nancy vs Paris 13 Atletico | 1.94 | 3.35 | 3.69 |
| 21:30 | 3504 | Dunkerque vs FC Martigues | 2.27 | 3.31 | 2.92 |
| 21:30 | 4288 | Le Mans vs Bourg Peronnas | 2.28 | 3.25 | 2.96 |
| 21:30 | 4435 | Cholet vs Villefranche Sur Saone | 2.75 | 3.30 | 2.39 |
| 22:00 | 1170 | Cameroon vs Brazil | 7.61 | 4.90 | 1.36 |
| 22:00 | 4007 | RSC Anderlecht Futures vs Jong KRC Genk | 2.14 | 3.74 | 2.86 |
| 22:00 | 4192 | Serbia vs Switzerland | 2.49 | 3.29 | 2.74 |
| 22:45 | 1366 | Haverfordwest vs Penybont | 2.60 | 3.40 | 2.60 |
| 22:45 | 1824 | Airbus UK Broughton vs Gap Connahs Quay | 9.60 | 6.20 | 1.24 |
| 22:45 | 2514 | Glenavon vs Larne | 5.04 | 4.17 | 1.51 |
| 22:45 | 2554 | Charlton vs Cheltenham | 1.70 | 3.61 | 4.65 |
| 22:45 | 2834 | Ipswich vs Fleetwood Town | 1.34 | 4.75 | 8.31 |
| 22:45 | 2910 | Plymouth vs Port Vale | 2.06 | 3.47 | 3.27 |
| 22:45 | 3918 | Peterborough vs Barnsley | 2.10 | 3.42 | 3.22 |
| 22:45 | 4820 | Caernarfon Town vs Newtown AFC | 1.80 | 3.65 | 4.20 |
| 22:45 | 4868 | Bala Town vs Flint Town United | 1.54 | 4.18 | 4.76 |
| 22:45 | 5250 | Morecambe vs Exeter | 3.52 | 3.57 | 1.94 |
| 22:45 | 5352 | Pontypridd Town vs Cardiff Met Uni. | 2.49 | 3.75 | 2.49 |
| 22:45 | 5519 | Bolton vs Bristol Rovers | 1.71 | 3.67 | 4.46 |
| 23:30 | 3278 | Granada vs Alaves | 2.12 | 3.08 | 3.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Desemba 2, 2022
Nipashe



UKURASA 29

**Messi awapigia saluti wenzake**

# SIMBA: TUTARUDI KILELENI LIGI KUU

## ●●●Yasema ni suala la kusubiri muda tu, mikakati zaidi yaimarishwa ili kufikia...

**Na Saada Akida**

KICHAPO cha bao 1-0 walichokipata watani zao, Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu ni faraja kwa Simba ambayo imetamba kesho itaendelea kuwapa furaha mashabiki na wanachama wake kwa kupata ushindi dhidi ya wenyeji, Coastal Union, imeelezwa.

Hata hivyo, Yanga ambao ni mabingwa watetezi na wana mechi moja ya kiporo, bado wako kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 32, sawa na Azam FC huku Simba yenye pointi 31 ikiwa kwenye nafasi ya tatu.

Endapo Yanga iliyoko chini ya Mtunisia, Nesreddine Nabi, ingepata matokeo mazuri katika mechi hiyo, ingeendelea kuwaacha mbali watani zao, Simba.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana, kupoteza kwa watani zao kumekuwa ni faraja kwao na imewarejesha kwenye mbio za kuwania taji hilo ambazo bado ziko wazi.

Ahmed alisema sasa kuna taswira nzuri na kupata mwanga wa kurejea kileleni hasa wachezaji wa wekundu hao aa Msimbazi wakiendelea kujitoa kutafuta matokeo michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyopo mbele yao.

Ofisa huyo alisema benchi la ufundi linaendelea kukiandaa vizuri kikosi chao na wanafurahi kuona kila mchezaji wa Simba yuko tayari kupambana na hatimaye kufikia malengo yaliyowekwa na timu hiyo iliyoko kwenye hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema wanafahamu na wanatambua mchezo dhidi ya Coastal Union utakuwa mgumu na wenye ushindani, hivyo wamejipanga kucheza kwa nidhamu muda wote.

"Hakuna mechi rahisi msimu huu, tena kwetu sisi kila mchezo ni zaidi ya fainali, tutaingia uwanjani kuwakabili Coastal Union kwa kuwaheshimu, ni wapinzani ambao wako imara na wao dhamira yao ni kupata pointi tatu," alisema Ahmed.

Aliongeza haitakuwa maana ya kushinda mchezo uliopita ambao uliwapa furaha mashabiki na baada ya kupita siku chache wakapoteza mechi, wakati wanahitaji kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo ya juu nchini.

Alisema kila mchezaji anajua wanakutana na timu yenye wachezaji wazoefu na wanaofahamu vyema falsafa za kocha (Juma Mgunda), ambaye alitoka kwenye kikosi hicho, hivyo kila upande unatakiwa kuongeza utulivu.

"Tunahitaji kupata matokeo chanya katika mechi ya Coastal Union, haitapendeza kwa sababu matu-

INAENDELEA UK. 31




Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kulia), akiwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa timu hiyo, Moses Phiri katika mazoezi ya kujiandaa kuikabili Coastal Union yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Mo Arena ulioko Bunju, Dar es Salaam jana asubuhi. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga kufurahia Unbeaten 49 J'pili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeandaa sherehe ya kuadhimisha kucheza mechi 49 bila kupoteza itakayofanyika keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati ikiwakaribisha Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu, imefahamika.

Hatua hiyo imekuja ikiwa na machungu ya kupoteza mechi yake dhidi ya Ihefu SC iliyochezwa Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya na kushindwa kufikisha 'Unbeaten' ya 50.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kulikuwa na vitu viwili au vitatu ambavyo vilisababisha wakapoteza mechi hiyo huku akifunguka kabla ya mchezo huo, dalili za kufungwa zilianza kuonekana mapema.

Kamwe alisema licha ya Ihefu kutokuwa na msimu nzuri, lakini 'Walima Mpunga' hao wana kikosi imara kinachopambana lakini hakina bahati ya kupata ushindi.

"Kwanza ni uchovu, pili ni hali ya majeruhi, wachezaji wetu wengi wana fatiki, ulikuwa ukiwaona tu hata wanavyokimbia unaona hawaendi inavyotakiwa. Watu wengi hawajui idadi kubwa ya wachezaji wa Yanga ni majeruhi ambao wako nje na wengine wanacheza, unawaota tu uwanjani lakini hawako fiti kwa asilimia zote," alisema Kamwe

Alimtaka mshambuliaji, Fiston Mayele ni mmoja wa wachezaji ambao hawako fiti lakini analazimika kupambana ili kuisaidia timu kufikia malengo.

"Hata Salum Aboubakar 'Sure Boy' hivyo hivyo, Khalid Aucho naye pia ni majeruhi, walijituma kwa sababu tu wanaipenda Yanga na wanapenda mashabiki wapate burudani, walipambana ili timu ipate matokeo, lakini hawakuwa fiti," alisema Kamwe.

Aliitaja sababu nyingine ambayo iliwakosesha ushindi ni namna Ihefu ilivyodhamiria kupata ushindi katika mechi hiyo kutokana na mikakati waliyokuwa nayo kuelekea mchezo huo.

"Unajua hizi timu ndogo zikiwa zinataka kucheza na timu kubwa, lengo lao la kwanza huwa ni

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >